
# Kiswahili

## Shule za Sekondari

## Kitabu cha Mwanafunzi

Kidato cha Tatu



Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Kiswahili

## Shule za Sekondari

# Kitabu cha Mwanafunzi

## Kidato cha Tatu



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 526

Jina la Chapisho: Kiswahili Shule za Sekondari Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tatu

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-269-7

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 10 Juni, 2021 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Kidato cha Tatu katika ngazi ya Elimu ya Sekondari nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa mwaka 2005.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

Taasisi ya Elimu Tanzania

Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 1 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

@ Taasisi ya Elimu Tanzania 2021

Kimechapishwa 2021

ISBN: 978-9987-09-269-7

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam - Tanzania

Simu: +255 735 041 168
+255 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

FOR ONLINE USE ONLY

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa sehemu ya kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 2 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

**Orodha ya Majedwali** .......... v

**Orodha ya Vielelezo** .......... vi

**Vifupisho** .......... vii

**Shukurani** .......... ix

**Dibaji** .......... x

**Sura ya Kwanza:** Ngeli za nomino .......... 1

Upatanisho wa kisarufi .......... 3

O-rejeshi katika ngeli .......... 11

Zoezi la marudio la 1 .......... 14

**Sura ya Pili:** Tungo .......... 16

Tungo neno .......... 19

Tungo kirai .......... 20

Tungo kishazi .......... 28

Tungo sentensi .......... 33

Uchanganuzi wa sentensi .......... 41

Zoezi la marudio la 2 .......... 51

**Sura ya Tatu:** Maendeleo ya Kiswahili .......... 54

Asili ya Kiswahili .......... 55

Chimbuko la Kiswahili .......... 62

Zoezi la marudio la 3 .......... 66

**Sura ya Nne:** Kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania wakati wa ukoloni .......... 68

Kukua na kuenea kwa Kiswahili enzi za Waarabu .......... 71

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kukua na kuenea kwa Kiswahili enzi za Wajerumani............................74
Zoezi la marudio la 4..........................................................................79

**Sura ya Tano:** Uhakiki wa kazi za fasihi andishi ..........................................80
Uhakiki wa riwaya.....................................................................................94
Uhakiki wa tamthiliya ...............................................................................97
Uhakiki wa ushairi.....................................................................................99
Zoezi la marudio la 5..........................................................................100

**Sura ya Sita:** Utungaji wa kazi za fasihi andishi .........................................103
Utungaji wa hadithi fupi...........................................................................103
Utungaji wa riwaya....................................................................................107
Utungaji wa tamthiliya .............................................................................111
Zoezi la marudio la 6..........................................................................115

**Sura ya Saba:** Uandishi wa insha na matangazo ........................................117
Uandishi wa insha.....................................................................................119
Uandishi wa matangazo ...........................................................................124
Zoezi la marudio la 7..........................................................................132

**Sura ya Nane:** Ufahamu na ufupisho ..........................................................134
Kusoma kwa ufahamu ...............................................................................134
Kufupisha habari .......................................................................................140
Zoezi la marudio la 8..........................................................................143

**Faharasa**..................................................................................................146

**Bibliografia** ..............................................................................................150

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 4 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY

# Orodha ya Majedwali

1.1: Mgawanyo wa ngeli za nomino kwa kigezo cha kisintaksia au upatanisho wa kisarufi ..... 7

1.2: Matumizi ya o-rejeshi katika ngeli za upatanisho wa kisarufi ..... 13

3.1: Baadhi ya lahaja za Kiswahili na maeneo zinakozungumzwa ..... 64

4.1: Baadhi ya maneno ya Kiswahili yaliyopokelewa kutoka lugha za kigeni ..... 78

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Orodha ya Vielelezo

2.1: Mjengo wa tungo ....18

3.1: Hali ya kutokea kwa Pijini....57

3.2: Ramani ya Afrika kuonesha msambao wa Wabantu....63

3.3: Ramani ya Afrika kuonesha baadhi ya lugha za Kibantu....65

4.1: Ramani ya Tanzania kuonesha misafara ya utawala wa Wajerumani.... 77

5.1: Vipengele vya uhakiki wa kazi za fasihi andishi....83

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 6 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| A | Kiarifu |
| BK | Baada ya Kristo |
| CH | Chagizo |
| CKD | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |
| βE | Kishazi tegemezi kielezi |
| βV | Kishazi tegemezi kivumishi |
| DUCE | Dar es Saalam University College of Educaton |
| E | Kielezi |
| Hs | Kihisishi |
| H | Kihusishi |
| JUCO | Jordan University College |
| K | Kiima |
| KE | Kirai kielezi |
| KH | Kirai kihusishi |
| KHr | Kishazi huru |
| KN | Kirai nomino |
| KT | Kirai kitenzi |
| Ktg/β | Kishazi tegemezi |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | |
|---|---|
| KV | Kirai kivumishi |
| MUCE | Mkwawa University College of Education |
| N | Nomino |
| P | Prediketa |
| S | Sentensi |
| SH | Shamirisho |
| t | Kitenzi kishirikishi |
| T | Kitenzi kikuu |
| Ts | Kitenzi kisaidizi |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| U | Kiunganishi |
| UDOM | University of Dodoma |
| UDSM | University of Dar es Saalam |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| V | Kivumishi |
| W | Kiwakilishi |
| Ø | Kapa |
| $ | Alama ya mpaka wa silabi |

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 8 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki waliofanikisha uandishi wa kitabu hiki. Pia, TET inatoa shukurani kwa taasisi zote za umma na binafsi zilizoshiriki kwa namna moja ama nyingine katika kufanikisha uandishi wa kitabu hiki. Taasisi hizo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (CKD - DUCE), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (CKD - MUCE), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo Kikuu Kishiriki Jordan (JUCO), na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Vilevile, TET inatoa shukrani kwa Vyuo vya Ualimu, Shule za Sekondari, na ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule.

Kipekee, TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao:

| | |
|---|---|
| **Waandishi:** | Bw. Samwel M. Magutu, Bi. Maria J. Nguruwe na Bi. Asia M. Akaro (TET) |
| **Wahariri:** | Dkt. Arnold B. G. Msigwa (CKD), Dkt. Rose Mbijima (CKD - DUCE), Dkt. Pendo Mwashota (CKD - MUCE), Bi. Sikitu E. Luvanda (CKD), Dkt. Zabron Philipo (UDOM) na Bw. Ambrose Mghanga (BAKITA) |
| **Msanifu:** | Bi. Pamela S. Makusi |
| **Mpiga picha:** | Bw. Chrisant A. Ignas (TET) |
| **Wachoraji:** | Bi. Rehema Maganga, Fikiri A. Msimbe (TET) na Alama Art and Media Production Co. Ltd. |
| **Mratibu:** | Bi. Maria J. Nguruwe |

Pia, TET inatoa shukurani kwa walimu na wanafunzi wa shule za sekondari walioshiriki katika hatua ya ujaribishaji wa muswada wa kitabu hiki. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandishi na uchapaji wa kitabu hiki.



Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 9 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Dibaji

Kitabu hiki ni cha tatu katika mfululizo wa vitabu vinne vya Somo la Kiswahili kuanzia Kidato cha Kwanza hadi cha Nne, kilichoandaliwa mahususi kwako mwanafunzi wa Kidato cha Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kitabu hiki kimeandaliwa kwa kuzingatia Muhtasari wa Somo la Kiswahili wa mwaka 2005 uliotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Maudhui yaliyomo katika kitabu hiki ni mwendelezo wa yale yaliyomo katika kitabu cha Kiswahili Kidato cha Pili. Kitabu kimegawanywa katika sura nane: Ngeli za nomino, Tungo, Maendeleo ya Kiswahili, Kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania wakati wa ukoloni, Uhakiki wa kazi za fasihi andishi, Utungaji wa kazi za fasihi andishi, Uandishi wa insha na matangazo, na Ufahamu na ufupisho.

Maudhui ya kitabu hiki yamewasilishwa kwa njia ya matini, kazi za kufanya, vielelezo, na picha ambazo zote zinachochea ujenzi wa umahiri unaokusudiwa kwa kila sura. Vilevile, katika kila sura yapo mazoezi yenye lengo la kupima na kujenga uelewa pamoja na ujuzi katika somo hili. Hivyo, unapaswa kufanya mazoezi na kazi zote zilizomo kwenye kitabu hiki na kazi nyingine utakazopewa na mwalimu.

FOR ONLINE USE ONLY

**Taasisi ya Elimu Tanzania**



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 10 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kwanza

## Ngeli za nomino

### Utangulizi

*Nomino huweza kugawanywa na kupangwa kwa kuzingatia kigezo cha upatanisho wa kisarufi au kisintaksia, kimofolojia na kisemantiki. Katika sura hii, utajifunza maana ya ngeli, ngeli za nomino, kugawanya ngeli za nomino kwa kutumia kigezo cha upatanisho wa kisarufi au kisintaksia na matumizi ya viambishi vya o-rejeshi katika vitenzi. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kugawanya nomino katika makundi yake na kuwasiliana kwa kutumia Kiswahili sanifu.*

FOR ONLINE USE ONLY

### Kazi ya 1.1

**Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Ninajitanua kwa lugha, zilo tamu za Kibantu,
Kwenye kila uwanja nipo, sayansi na insia,
Mwenzangu nimesikia, watu wakiulizana,
Kuhusu jina la ngeli, mabishano hayakomi,
Hunikuti kwa wageni, ni kwa Wabantu wenzangu tu.

Wauliza ngeli? Hilo nimetoa kwa wenzangu,
Wenzangu wepi? Nimetoa kwa Wahaya,
Ndege wafananao, huruka pamoja,
Nomino, kama ndege, huruka pamoja pia,
Hunikuti kwa wageni, ni kwa Wabantu wenzangu tu.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 1 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Ngeli za nomino zifananazo, muungano hudumu,
Viumbe hai na visivyo hai, nominoze haziungani,
Ngeli sikai kiholela, mpango nazingatia,
Kisintaksia napangwa, kulingana na viambishi,
Hunikuti kwa wageni, ni kwa Wabantu wenzangu tu.

Ukitaka kunielewa, kiambishi usikosee,
Ukikosea dhahiri, maana taiharibu,
Utaleta utata, kwa watumiaji wa lugha,
Ukitaka tuendane, vitu na watu sichanganye,
Hunikuti kwa wageni, ni kwa Wabantu wenzangu tu.

Kisintaksia uhusiano, wa vipashio zingatia,
Maneno yanapendana, upatanisho ni mshenga,
Ukinipanga bila mpango, maana taiharibu,
Anisikilizaye na kunisoma, atapata tabu sana,
Hunikuti kwa wageni, ni kwa Wabantu wenzangu tu.

Kiswahili najidai, sifa zangu mzomzo,
Wauliza urejeshi, bila ngeli hujinadi,
Uhusiano murua, wa vipashio zingatia,
Ukisahau urafiki wa ngeli, urejeshi kupotoa,
Hunikuti kwa wageni, ni kwa Wabantu wenzangu tu.

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

1. Unafahamu nini kuhusu asili ya neno ngeli? Fafanua.
2. Katika shairi ulilolisoma, mshairi anaeleza kuhusu nini?
3. Toa maana ya ngeli za nomino kwa mujibu wa mshairi.
4. Ili kubainisha ngeli za nomino ni mambo gani ya msingi yanayotakiwa kuzingatiwa?
5. Katika kituo cha shairi, mwandishi anakusudia kusema nini?

## Upatanisho wa kisarufi

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kazi ya 1.2

**Chunguza picha zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.**



### Maswali

1. Kwa kila picha, na kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi, tunga sentensi mbili kuonesha umoja na wingi.
2. Bainisha ngeli za nomino kwa kila sentensi uliyotunga.

### Kazi ya 1.3

**Chunguza orodha ya maneno hapa chini, kisha jibu maswali yanayofuata.**

| | | |
|---|---|---|
| kiti | sahani | ubani |
| jiko | ukuta | kuku |
| meno | ufa | ng'ombe |
| sufuria | mtoto | Mungu |
| kikombe | karai | uzi |
| kalamu | dirisha | nyumba |
| pembe | gari | ndege |
| debe | tunda | uchaguzi |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Andika maneno hayo katika umoja na wingi.
2. Orodhesha viambishi vya umoja na wingi vya maneno hayo.
3. Bainisha maneno yanayofanana, kisha yapange katika ngeli.

### Kazi ya 1.4

**Chunguza mifano ya sentensi zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

(a) Mtoto anacheza.

(b) Mbuzi yumo zizini.

(c) Mti umeanguka chini.

(d) Changu kizuri kimenunuliwa.

(e) Yule mwembamba ameinama.

(f) Msichana mrembo amewasili.

(g) Mtoto mzuri anacheza.

(h) Mti mfupi umekatwa.

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

1. Bainisha viambishi vya upatanisho wa kisarufi wa nomino na vitenzi katika sentensi ulizopewa.
2. Je, sentensi ulizopewa zina viambishi vya upatanisho wa kisarufi wa aina moja? Fafanua.
3. Badili sentensi hizo kuwa katika wingi.
4. Bainisha viambishi vinavyoonesha upatanisho wa kisarufi, kwa kuweka pamoja sentensi zenye viambishi vya upatanisho wa kisarufi unaofanana.
5. Kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi, unda sentensi 20 zenye nomino tofautitofauti, kisha panga nomino hizo katika ngeli.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 4 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zingatia

Makundi ya majina ya wanyama, watu, vitu, na mahali kwa kuzingatia sifa zake, huitwa ngeli za nomino. Kisarufi, ngeli za nomino hufafanuliwa kwa kutumia kigezo cha kisintaksia ambacho huangalia upatanisho wa kisarufi baina ya majina na vitenzi.

Upatanisho wa kisarufi hutambulisha ngeli za nomino kwa kuangalia viambishi awali vya umoja na wingi katika nomino au viwakilishi, vivumishi na vitenzi katika sentensi. Kwa mfano:

(a) Mvuvi yupo hapa - Wavuvi wapo hapa.

(b) Mtoto analilia wembe - Watoto wanalilia nyembe.

Viambishi vya upatanisho wa kisarufi ni [yu-] na [a-] katika umoja, na [wa-] katika wingi. Hivyo, ngeli ya nomino katika mfano huo ni [yu-a-/wa-].

Mfano mwingine wa sentensi za umoja na wingi ni kama ifuatavyo:

(a) Kisu hiki kina makali - Visu hivi vina makali.

(b) Kinanda hiki kinalia vizuri zaidi - Vinanda hivi vinalia vizuri zaidi.

Viambishi vya upatanisho wa kisarufi ni [ki-] katika umoja, na [vi-] katika wingi. Katika mfano huo, ngeli ya nomino ni [ki-/vi-].

Hivyo, uainishaji wa ngeli za nomino kwa kigezo cha upatanisho wa kisarufi huzingatia viambishi awali vya nomino au viwakilishi, vivumishi na vitenzi.

### Kazi ya 1.5

1. Kwa kutumia majina kumi ya watu na vitu unavyovifahamu, tunga sentensi kumi zenye umoja na wingi.
2. Kwa kuzingatia mfanano wa viambishi awali vya vitenzi, panga sentensi ulizozitunga katika swali la kwanza kwenye ngeli inayohusika.

FOR ONLINE USE ONLY

### Kazi ya 1.6

**Chunguza sentensi zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

1. Mvuvi wapo hapa.
2. Uchaguzi zimeahirishwa.
3. Kisu hiki vina makali.
4. Ukuta zimejengwa kwa matofali.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 5 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Ubao huu imechorwa.
6. Kiti itafaa zaidi kukalia.
7. Kinanda hiki vinalia vizuri zaidi.
8. Mikeka hii zimenunuliwa.
9. Mipapai yake yanakatwa.
10. Mihogo zilipikwa.
11. Miti mikubwa una matunda.
12. Madaftari mazuri imechanika leo.
13. Mbwa wakali imepotea.

## Maswali

1. Bainisha makosa ya upatanisho wa kisarufi kwa kila sentensi uliyopewa.
2. Rekebisha makosa hayo, kisha andika upya sentensi hizo kwa usahihi.

### Kazi ya 1.7

Zungumza na watu mbalimbali au sikiliza mazungumzo yao, kisha orodhesha sentensi ulizozisikia katika mazungumzo hayo. Bainisha makosa ya upatanisho wa kisarufi yaliyojitokeza. Andika sentensi hizo kwa usahihi, kisha wasilisha kazi hiyo darasani.

FOR ONLINE USE ONLY

### Zoezi la 1.1

1. Kwa kuzingatia umoja na wingi, tunga sentensi kumi kwa kila ngeli zifuatazo:
   (a) YU-A-WA
   (b) KI-VI
   (c) U-ZI
   (d) I-ZI
   (e) LI-YA
2. Kwa kutumia mifano ya nomino 20, zigawe katika aina nyingine za ngeli tofauti na ulizopewa katika swali la kwanza.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 6 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zingatia

Kwa kutumia kigezo cha kisintaksia au upatanisho wa kisarufi, nomino za Kiswahili hugawanywa katika ngeli kumi na mbili. Jedwali lifuatalo linaonesha mgawanyo wa ngeli hizo.

**Jedwali la 1.1:** Mgawanyo wa ngeli za nomino kwa kigezo cha kisintaksia au upatanisho wa kisarufi

| Na. | Aina ya ngeli | Viambishi | Mifano | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Umoja | Wingi |
| 1. | YU/A-WA | YU-, A- } umoja<br>WA-wingi | Mgeni **yu**mo ndani<br>Mgeni **a**mekuja<br>Ng'ombe **a**mechinjwa asubuhi | Wageni **wa**mo ndani<br>Wageni **wa**mekuja<br>Ng'ombe **wa**mechinjwa asubuhi |
| 2. | U-I | U- umoja<br>I -wingi | Mkutano **u**meanza mchana<br>Mgomba **u**mekatika | Mikutano **i**meanza mchana<br>Migomba **i**mekatika |
| 3. | LI-YA | LI - umoja<br>YA - wingi | Jembe **li**mepotea<br>Papai **li**meiva | Majembe **ya**mepotea<br>Mapapai **ya**meiva |
| 4. | KI-VI | KI - umoja<br>VI - wingi | Kijiko **ki**nang'aa<br>Kitabu hiki **ki**nasomwa | Vijiko **vi**nang'aa<br>Vitabu hivi **vi**nasomwa |
| 5. | I-ZI | I - umoja<br>ZI - wingi | Kazi hii **i**natosha<br>Suruali **i**tashonwa kesho | Kazi hizi **zi**natosha<br>Suruali **zi**tashonwa kesho |
| 6. | U-ZI | U - umoja<br>ZI - wingi | Uzi **u**mekatika<br>Ukuta **u**mebomoka | Nyuzi **zi**mekatika<br>Kuta **zi**mebomoka |
| 7. | U-YA | U - umoja<br>YA -wingi | Uovu **u**mezidi nchini<br>Ugonjwa **u**meenea | Maovu **ya**mezidi nchini<br>Magonjwa **ya**meenea |
| 8. | I-I | I- | Chai **i**memwagika<br>Sukari **i**mepanda bei | Chai **i**memwagika<br>Sukari **i**mepanda bei |
| 9. | U-U | U- | Uongo **u**mekithiri<br>Unga **u**mevunda | Uongo **u**mekithiri<br>Unga **u**mevunda |
| 10. | YA-YA | YA- | Maziwa **ya**meuzwa<br>Maji **ya**mejaa sana | Maziwa **ya**meuzwa<br>Maji **ya**mejaa sana |
| 11. | KU- | KU- | Kusoma **ku**na manufaa<br>Kucheza **ku**nafurahisha | |
| 12. | PA-MU-KU | PA-<br>MU-<br>KU- | Hapa petu **pa**mejaa<br>Humu ndani **m**na giza<br>Kule **ku**naonekana vizuri | |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya 1.8**

1. Orodhesha majina ya vitu vitano vinavyopatikana katika mazingira yako, kisha weka kila jina katika ngeli inayohusika. Hakikisha viambishi vya upatanisho wa kisarufi kama vinakubaliana na ngeli hiyo.
2. Chunguza nomino za ngeli ya nne, ziorodheshe, kisha ziwasilishe darasani.

**Kazi ya 1.9**

**Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Tanzania ni nchi yenye majira mbalimbali ya mwaka yakiwamo masika, kiangazi, vuli na kipupwe. Masika ni kipindi ambacho mvua nyingi hunyesha sehemu kubwa ya nchi. Kipindi hiki huwa ni lele kwa wanyama na wakulima. Wakulima hupiga vigelegele vya nderemo na vifijo. Wakulima huwa na ari ya hali ya juu kwani hutifua ardhi kwa jembe la mkono, plau na matrekta ili kupanda mbegu na hutegemea kupata mazao. Wahenga hawakukosea waliposema, "Jembe halimtupi mkulima." Wakulima huona fahari kutekeleza kauli mbiu isemayo: "Kilimo ni uti wa mgongo wa taifa letu." Licha ya vigelegele na furaha inayotokana na mvua, pia zipo hasara kwani baadhi ya wakulima mambo huenda mrama. Hii ni kutokana na madhara yanayotokana na mvua ambayo ni mafuriko yanayosababisha balaa na maafa.

Mafuriko huleta adha kubwa kwa jamii, kwani nyumba hubomoka, mashamba hujaa maji, mazao na miundombinu huharibika na hufanya watu wengine kuhama makazi yao. Pia, husababisha njaa, magonjwa ya mlipuko na vifo. Kila chenye faida hakikosi kuwa na hasara, ndio maana wahenga walisema "Hakuna masika yasiyo na mbu." Kipindi hiki, huwapo mazalia ya mbu ambayo ni tatizo kubwa kwa binadamu kwani vifo vingi hutokea kutokana na malaria.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



Mwezi uliopita wakati wa usiku, Juma akiwa amelala usingizi alishitushwa na kelele za watu. Baada ya kuamka, aliona maji mengi yamejaa ndani ya chumba alichokuwa amelala. Watu wengi walikuwa wamelala fofofo. Ghafla kelele na mayowe vilisikika, maji! Maji! Maji! Nakufaaa! Uwiii! Msaaaada! Watu walitapatapa wakikimbia huku na huko. Mafuriko yaliathiri watu, wanyama, na kuharibu makazi, mashamba, na miundombinu, mfano: barabara na madaraja. Pia, yalikata mawasiliano baina ya pande mbili za kijiji. Shughuli za uchumi zilizoroteshwa. Wakazi wa eneo hilo hawakuamini macho yao jinsi mto ulivyojaa na kufurika hadi kufikia makazi yao, hata kwa wale wanaoishi mbali kidogo na mto. Usiku huo kulikuwa na patashika nguo kuchanika. Kila mmoja alipambana kunusuru maisha yake.

Kesho yake, serikali na watu binafsi, walifanya jitihada za kuokoa waathirika wa mafuriko. Vijana na wapigambizi walikuwa bega kwa bega kusaidia kuokoa watu na mali zao. Waathirika wengine walibebwa mgongoni, mabegani na wengine kwenye chombo maalumu. Mimea iliyokuwa ikinesanesa usiku na mchana kwa shukurani, ilionekana kupoteza matumaini kwani yote ilikuwa imemezwa na maji. Mazao mengi mashambani yaliharibika na kufanya hali ya uchumi kudorora. Hivyo, wananchi walikuwa na wakati mgumu sana kimaisha. Methali isemayo, "Jembe halimtupi mkulima," haikufua dafu. Wananchi waliomba msaada kutoka serikalini na kwa watu binafsi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Haya yote yalisababishwa na baadhi ya wananchi kuvunja sheria ya mazingira kwa kujenga makazi karibu na vyanzo vya maji hasa mito. Kile walichokipuuza sasa kimetokea. Walikumbuka maneno yenye hekima yaliyowahi kusemwa na wahenga, "Mdharau mwiba mguu huota tende" na "Sikio la kufa halisikii dawa." Pamoja na juhudi zilizofanyika kuokoa maisha ya wananchi serikali ilifanya kazi bega kwa bega na wananchi kukarabati miundombinu iliyoharibiwa kwa mafuriko.

## Maswali

1. Neno "wakulima" lipo katika ngeli ipi?
2. Ainisha ngeli zilizomo kwenye vifungu vya maneno "mambo huenda mrama," "yowe limepigwa."
3. "Mimea iliyokuwa ikinesanesa." Kifungu hiki cha maneno kipo katika aina ipi ya ngeli?
4. Kwa kutumia habari uliyoisoma, andika kifungu cha maneno chenye ngeli ya I-ZI.
5. Kwa kutumia vifungu viwili vya maneno katika aya ya pili, onesha ngeli ya kwanza.
6. Onesha ngeli za nomino zilizojitokeza katika aya ya mwisho.
7. Kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi, andika ngeli sita za nomino zinazotokana na habari uliyoisoma.

FOR ONLINE USE ONLY

### Kazi ya 1.10

1. Kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi, andika habari yenye maneno yasiyozidi 250 na yasiyopungua 200 katika mojawapo ya mada zifuatazo:
   (a) Usalama barabarani
   (b) Haki za mtoto
   (c) Utunzaji wa mazingira ya shule
2. Kwa kuzingatia kigezo cha kisintaksia, andika majina ya vitu mbalimbali vinavyopatikana shuleni, darasani, nyumbani au mtaani kwenu, kisha panga majina hayo katika ngeli inayohusika.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 10 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya 1.11**

1. Orodhesha majina ya vitu vitano ambavyo vinapatikana darasani, shuleni au nyumbani, kisha panga majina ya vitu hivyo katika ngeli inayohusika.
2. Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.

Baba yake Zawadi ni mkulima mkubwa katika Kijiji cha Tuungane. Yeye hulima aina mbalimbali za matunda katika shamba lake, yakiwamo mapapai, mapera, machungwa na maembe. Pia, ana bustani kubwa ya mbogamboga ambayo inaweza kulisha kijiji kizima. Wanakijiji huenda kwake kununua mchicha, kabichi, bamia, nyanya na biringanya. Pamoja na kilimo, pia hujishughulisha na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, mbuzi, na kuku. Aidha, Baba Zawadi ana punda watatu anaowatumia kubebea mizigo kwenda sokoni. Wakati wa kurudi nyumbani, punda hao humsaidia kubeba mahitaji mbalimbali ya nyumbani. Hakika, Baba Zawadi ananufaika sana na shughuli za kilimo na ufugaji.

## Maswali

1. Orodhesha majina ya mbogamboga, wanyama na matunda yaliyojitokeza katika kifungu cha habari ulichokisoma kwenye ngeli inayohusika.
2. Andika ngeli za majina hayo. Umewezaje kupata ngeli hizo ? Fafanua.
3. Kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi, andika habari yenye maneno yasiyozidi 250 na yasiyopungua 100, kisha ainisha makundi ya ngeli za nomino yatakayojitokeza katika habari hiyo.

## O-rejeshi katika ngeli

**Kazi ya 1.12**

**Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Masopano alikuwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Mtengeshari. Yeye ni miongoni mwa wanafunzi waliofanya vizuri mtihani wa taifa mwaka jana. Walimu waliomfundisha mwanafunzi huyo, walijigamba kwa kuwa shule yao ilitoa mwanafunzi bora. Kila shule iliyofanya vizuri kitaifa ilipata zawadi ya kikombe na shilingi milioni tano zilizoahidiwa. Waziri aliyetoa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

hotuba siku hiyo, alizitaka shule zingine kuiga mfano wa walimu hao. Waziri aliahidi kuwa mwanafunzi atakayefanya vizuri mtihani wa taifa mwaka ujao atasomeshwa hadi chuo kikuu. Walimu na wazazi waliokuwapo kwenye hafla hiyo, walimshangilia Masopano. Pia, wazazi waliipongeza shule yake kwa juhudi ilizozifanya mpaka kutoa mwanafunzi bora. Waziri alipomaliza hotuba yake, alipanda gari lake lililokuwa linaongozwa na msafara wa polisi.

## Maswali

1. Bainisha sentensi zenye o-rejeshi katika kifungu cha habari ulichokisoma.
2. Tunga sentensi kumi zenye vitenzi vyenye o-rejeshi.
3. Fasili istilahi ya o-rejeshi.

## Zoezi la 1.2

1. Fafanua dhana ya o-rejeshi katika upatanisho wa kisarufi.
2. Tunga sentensi tatu, kila moja iwe na kiambishi rejeshi {-mo-}.
3. Tunga sentensi katika umoja na wingi zenye viambishi vya o-rejeshi kwa kutumia maneno yafuatayo: embe, nyumba, kitanda, mtu, kitabu, jembe na kabati.
4. Orodhesha maneno sita yaliyobeba viambishi rejeshi vya ngeli ya KI-VI.

FOR ONLINE USE ONLY

### Zingatia

O-rejeshi hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi. O-rejeshi hufuata mfumo wa upatanisho wa kisarufi katika ngeli. Angalia mifano ya o-rejeshi katika sentensi zifuatazo:

(a) Wagonjwa wali**o**pimwa walitibiwa.
(b) Jambo lili**lo**kusudiwa silo lili**lo**tendeka.
(c) Mwanafunzi ataka**ye**chelewa ataadhibiwa.
(d) Kitambaa kili**cho**pelekwa kitarudishwa.
(e) Tuliingia mahali tuli**mo**pangiwa.
(f) Mitungi ili**yo**tolewa shuleni inavuja.

Katika urejeshi, vitenzi hubeba viambishi ngeli vyenye kiambishi -o-, isipokuwa kama nomino iliyotajwa, ni ya ngeli ya kwanza umoja. Urejeshi wa ngeli hiyo hutumia {-ye-} badala ya {-o-}.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 12 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Jedwali la 1.2:** Matumizi ya o - rejeshi katika ngeli za upatanisho wa kisarufi

| | Aina ya ngeli | Viambishi vya ngeli | Viambishi vya -o- rejeshi | Mifano |
|---|---|---|---|---|
| 1. | YU/A-WA | YU-<br>A-<br>WA- | -YE-<br>-YE-<br>-O- | Mbuzi ana**ye**tafutwa yumo zizini<br>Mbuzi wana**o**tafutwa wamo zizini<br>Mzazi ali**ye**kuja ametoa zawadi<br>Wazazi wali**o**kuja wametoa zawadi |
| 2. | U - I | U-<br>1- | -O-<br>-YO- | Mti uli**o**nipa umestawi<br>Miti uli**yo**nipa imestawi |
| 3. | LI-YA | LI-<br>YA- | -LO-<br>-YO- | Koti lili**lo**fuliwa limekauka<br>Makoti yali**yo**fuliwa yamekauka |
| 4. | Kl-VI | KI-<br>VI- | -CHO-<br>-VYO- | Kiazi uli**cho**panda kimeota<br>Viazi uli**vyo**panda vimeota |
| 5. | I-ZI | I-<br>ZI- | -YO-<br>-ZO- | Kalamu ili**yo**nunuliwa imepotea<br>Kalamu zili**zo**nunuliwa zimepotea |
| 6. | U-ZI | U-<br>ZI- | - O-<br>-ZO | Uzi uli**o**shonea umekwisha<br>Nyuzi uli**zo**shonea zimekwisha |
| 7. | U-YA | U-<br>YA- | -O-<br>-YO- | Ugonjwa uli**o**ingia hauna dawa<br>Magonjwa yali**yo**ingia hayana dawa |
| 8. | I-I | I- | -YO- | Chai ili**yo**pikwa imeuzwa<br>Sukari ili**yo**nunuliwa imetumika |
| 9. | U-U | U- | -O- | Uongo ana**o**zungumza utamgharimu<br>Unga uli**o**anikwa umenyeshewa |
| 10. | YA-YA | YA- | -YO- | Maziwa yali**yo**uzwa yameganda<br>Maji yali**yo**letwa yanavuja |
| 11. | KU- | KU- | -KO- | Kucheza kuli**ko**nifurahisha ni kwa Kiba<br>Kuchora kuli**ko**pendekezwa kutazingatiwa |
| 12. | PA-MU-KU | PA-<br>MU-<br>KU- | -PO-<br>-MO-<br>-KO- | Hapo uli**po**kaa pamelowa<br>Humo uli**mo**ingia mmejaa<br>Huko una**ko**kwenda hakuna kitu |

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 13 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la marudio la 1

1. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

   (i) Mende anapenda kula uchafu. Neno lililopigiwa mstari lipo katika ngeli ipi?

   (a) KI-VI
   (b) U-I
   (c) A-WA
   (d) KU
   (e) LI-YA

   (ii) __________ mna watu wengi.

   (a) Aliingia
   (b) Alipoingia
   (c) Alikoingia
   (d) Alivyoingia
   (e) Alimoingia

   (iii) Neno "papai" linaingia katika ngeli ya __________

   (a) PA-MU-KU
   (b) U-ZI
   (c) U-YA
   (d) KI-VI
   (e) LI-YA

   (iv) "Shangazi yupo shambani kwake." Kifungu hiki cha maneno kipo katika ngeli gani?

   (a) I-ZI
   (b) YU-A-WA
   (c) PA-MU-KU
   (d) KI-VI
   (e) U-I

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Jaza nafasi zilizoachwa wazi.
   (i) Ng'ombe amekula mahindi shambani. Neno "ng'ombe" lipo katika ngeli ya ________
   (ii) Kigezo cha uainishaji wa ngeli za nomino kwa kuangalia ushikamani wa maneno katika sentensi huitwa ________
   (iii) ________ ni neno lenye asili ya lugha ya Kibantu inayozungumzwa na jamiii ya Wahaya.
   (iv) Maumbo "-ye-, -cho-, -o-, -mo-" yanajulikana kama maumbo ya ________
   (v) Upepo ulivuma kwa kasi. Neno "upepo" lipo katika ngeli ya ________
3. Eleza maana ya upatanisho wa kisarufi.
4. Tunga sentensi kumi zenye o-rejeshi ukitumia ngeli mbalimbali, kisha onesha kiambishi cha urejeshi kwa kila sentensi.
5. Kwa kutumia viambishi ngeli vya o-rejeshi, tunga sentensi kumi, kisha onesha matumizi ya viambishi ngeli vya [yu-a-/wa-] katika sentensi hizo.
6. Ngeli za nomino zinakusaidiaje katika maisha ya kila siku?
7. Tunga sentensi kumi, kisha zipange katika ngeli za kisintaksia zinazohusika.
8. Kwa kuzingatia kigezo cha kisintaksia, tunga dayalojia isiyozidi ukurasa mmoja, kisha pigia mstari kila ngeli iliyojitokeza.
9. Fafanua dhana ya ngeli za nomino.
10. Upatanisho wa kisarufi ni kigezo kimojawapo kinachounda ngeli za nomino. Kwa kutumia ngeli zifuatazo, tunga sentensi mbili kuthibitisha usemi huu:
    (a) U-I
    (b) LI-YA
    (c) I-ZI
    (d) A-WA
    (e) U-ZI

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Pili

## Tungo

### Utangulizi

*Tungo hujengwa na kanuni, taratibu na vipashio vinavyohusika. Katika sura hii, utajifunza maana, aina na miundo ya tungo za Kiswahili. Vilevile, utajifunza uchanganuzi wa sentensi kwa njia ya matawi na majedwali. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano kwa ufasaha.*

FOR ONLINE USE ONLY

### Kazi ya 2.1

**Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Pisha! Pisha! Pisha! Nipite,
Neno, kirai, kishazi!
Sisi sote ni tungo, twapaswa kushikamana,
Mimi sentensi ni mama, naitwa tungo mkubwa,
Naweza kaa peke yangu, maana nikaileta,
Twaweza kaa wawili, ujumbe kuufikisha.

Tungo neno menisusa, tungo kirai najua,
Mimi nawe marafiki, ukaribu wetu wa kale,
Naweza simama pekee, au kumshirikisha yule rafiki,
Tungo kirai watano, hiyo ni idadi yetu,
Tungo neno kwa hesabu, idadi yenu nane.

Mimi tungo kirai, wadogo zangu watano,
Yupo kirai nomino, na kirai kitenzi,
Hata kirai kivumishi, yeye pia ni wangu,
Naye kirai kielezi na kirai kihusishi wote wangu daima.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 16 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Nami kishazi najidai, kwetu tupo wawili,
Naweza kuwa huru, au nikawa tegemezi,
Tegemezi kishazi mtundu, kazaa watoto wawili,
Tegemezi kivumishi, na tegemezi kielezi,
Zama hizi tabu tupu, watoto kimbilia uhenga.

Kikongwe nimetulia, watoto wapiga domo,
Sentensi sina mbwembwe, kama maji ya mtungi,
Wanangu wapo watatu, unyenyekevu wanao,
Wa kwanza aitwa Sahili, wa pili ni Ambatani,
Naye mtoto mkubwa, jinale ni Changamani.

Popote utakapoenda, mimi utanikuta,
Kwa neno nipo, kwa kirai nipo, pia kwa kishazi,
Kwa vikongwe nimo, mtulivu wa zamani,
Tungo neno nakupenda, wewe tungo kirai,
Tungo kishazi mwenzangu, rafikiye na sentensi.
Sentensi kikongwe wetu, anahimiza umoja,
Sote tushikamane, lugha kuinogesha.

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

1. Je, shairi hilo linahusu nini?
2. Kutokana na shairi ulilolisoma, kuna aina ngapi za virai? Zitaje.
3. Kwa mujibu wa shairi ulilolisoma, kishazi ni nini?
4. Kutokana na shairi ulilolisoma, kuna aina ngapi za sentensi? Zitaje.

## Zingatia


Kisarufi, neno tungo lina maana ya kupanga pamoja vipashio vidogo vya lugha ili kupata vipashio vikubwa zaidi. Hivyo, tungo ni neno au mpangilio wa maneno ambao hutoa taarifa fulani inayoweza kuwa kamili au isiwe kamili. Tungo hufanya kazi ya kufanikisha mawasiliano katika maandishi au mazungumzo. Hata hivyo, tungo inaweza kuunganisha vipashio vidogo ili kuunda vipashio vikubwa, kudokeza taarifa fulani, kuonesha miundo mbalimbali ya sentensi, na kuhusianisha maneno



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 17 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

katika tungo, mfano: neno kuu na maneno mengine. Tungo zimegawanyika katika aina nne, nazo ni: tungo neno, kirai, kishazi na sentensi. Tazama kielelezo kifuatacho:




**Kielelezo Namba 2.1:** *Mjengo wa tungo*

FOR ONLINE USE ONLY

**Kazi ya 2.2**

Kusanya visoda au vibao vya kutosha kulingana na idadi ya vipashio vya sentensi, kisha andika herufi tofautitofauti kwa kila kibao au kisoda. Vipange visoda vyako ili kuunda neno, kirai, kishazi na sentensi kwa kuzingatia kielelezo cha mjengo wa tungo.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 18 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Tungo neno

**Kazi ya 2.3**

**Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Katika kijiji kimoja, alikuwako kuku wa aina yake aliyeitwa Koko. Kuku huyo aliishi ndani ya Pango la Komia lililopo pembezoni mwa kijiji hicho. Maadui wake walimwogopa kutokana na uwezo wake wa kupigana uliotokana na nguvu za wahenga wa jamii yake. Koko alifanikiwa kutaga yai moja. Yai hilo liliitwa Kitamkwa. Siku zilivyosonga, Kitamkwa alitotolewa na kuwa kifaranga. Kifaranga alipokuwa mkubwa alitaga mayai mawili na wakati mwingine alitaga mayai matatu au zaidi. Mayai hayo kwa pamoja yaliangua vifaranga vilivyoitwa Silabi. Silabi aliangua neno. Neno alitokana na Silabi mmoja na wakati mwingine Silabi wawili au zaidi. Kadiri Silabi walivyoshirikiana na Silabi wengine waliweza kuunda maneno mengi zaidi.

### Maswali

1. Kisa hiki kinahusu nini?
2. Kipashio cha Silabi kinaitwaje?
3. Kipashio kidogo cha tungo neno ni kipi?
4. Kipashio kikubwa kinachounda neno kinaitwaje?

**Kazi ya 2.4**

Chunguza vipashio vifuatavyo, kisha vitumie kuunda maneno ishirini.
/a/, /l/, /n/, /k/, /v/, /w/, /o/, /g/, /y/, /m/, /i/, /z/, /r/, /e/

**Zoezi la 2.1**

Tunga sentensi kumi, kisha bainisha aina za maneno zilizojitokeza katika kila sentensi.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zingatia

Katika lugha ya Kiswahili, tungo neno hujumuisha aina zote za maneno ambazo ni: nomino, kiwakilishi, kitenzi, kivumishi, kielezi, kihusishi, kihisishi na kiunganishi. Kila aina ya neno, husimama kama tungo neno. Tungo neno huweza kuundwa kwa

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kuunganisha vitamkwa, mfano: /l/, /a/, /k/, /i/, /m/, /y/, na /v/ ambavyo huungana kuunda silabi, mfano: $la$, $ka$, $ma$, $ki$, $ya$ na $va$. Silabi nazo huungana kuunda neno, mfano, silabi $ma$ na $ma$ zikiungana tunapata neno "mama". Hata hivyo, yapo maneno yanayoundwa na vitamkwa viwili tu, yaani silabi moja, mfano: kitamkwa /y/ na /a/ tunapata neno "ya", mfano: mawe **ya** kujengea yameletwa. Pia, kitamkwa /w/ na /a/ vikiunganishwa tunapata neno "wa", mfano: mpira **wa** mtoto umepotea. Vilevile, yapo maneno yanayoundwa na kitamkwa kimoja tu. Hii inajipambanua katika sentensi hizi: (a) Wewe **u** mwembamba. (b) Miti **i** mizuri. Kwa kuwa aina zote za maneno zipo katika kategoria ya tungo neno, ifuatayo ni mifano ya tungo neno. Nomino: mfano, *mwalimu, mtoto, mkulima*; Kiwakilishi: mfano, *sisi, yule, wao*; Kitenzi: mfano, *cheza, imbisha, palilia*; Kivumishi: mfano, *hodari, mzuri, mwembamba*; Kielezi: mfano, *shambani, polepole, haraka sana*; Kihusishi: mfano, *wa, kwa, la, ya, mwa*; Kihisishi: mfano, *lo! Lahaula! Aisee!;* na Kiunganishi: mfano, *lakini, na, ingawa, ili.*

## Tungo kirai

**Kazi ya 2.5**

**Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Vijana wengi wa Kitanzania ni shupavu sana na wazalendo. Hutumia nguvu zao kuijenga nchi kwa hiari yao wenyewe bila kulazimishwa wala kushurutishwa. Hali hii inatokana na elimu ya uraia na matumizi ya lugha ya Kiswahili inayokuwa kama daraja la kuwaunganisha. Hutambua umuhimu wa kuitumia lugha yao maridhawa sambamba na faida za kulipa kodi. Hununua bidhaa nchini mwao hali ambayo inafanya uchumi wao ukue kwa kasi. Yeyote anayejaribu kukiuka huelimishwa kuhusu faida za kujenga uchumi wa ndani ya nchi yao. Faida hizo ni uboreshaji wa huduma mbalimbali, mfano: elimu, afya, uvuvi na kilimo.

## Maswali

1. Orodhesha tungo virai zinazopatikana katika kifungu cha habari ulichokisoma.
2. Kwa kutumia tungo virai ulizoorodhesha, eleza maana ya tungo kirai kwa maneno yako mwenyewe.
3. Kuna uhusiano gani kati ya tungo neno na tungo kirai?
4. Eleza tofauti iliyopo kati ya tungo neno na tungo kirai.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 20 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Zingatia

Tungo yenye neno moja au zaidi inayotoa taarifa fulani kwa kujikita katika neno kuu huitwa kirai. Kirai huundwa na neno kuu na wakati mwingine huwa na kijalizo. Neno kuu ndilo hutambulisha aina ya kirai.

Kirai huweza kubainishwa kwa kuzingatia sifa bainifu zifuatazo: kirai huwa na neno kuu moja, vipashio vya kirai hupangwa kimantiki kutegemeana na sarufi ya lugha inayohusika, huwa na neno moja au kikundi cha maneno, huwa na taarifa kamili au isiyo kamili, na huwa hakina muundo wa kiima na kiarifu.

## Kirai nomino (KN)

### Kazi ya 2.6

**Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Mzee Kijembe amekula chumvi nyingi sana. Mzee huyu ana watoto nane na wajukuu kumi na wawili. Mzee Kijembe bado ana nguvu, yeye ni mkulima stadi wa zao la ngano. Yeye na mkewe hushirikiana katika kilimo cha ngano. Ngano ni zao la chakula linalohitajika sana duniani. Wakati wa jioni, yeye na mkewe hupumzika wakiangalia taarifa ya habari na michezo mingine. Pia, huwa na muda wa kuzungumza na wajukuu wao wakiwasimulia hadithi na visa vya kuchekesha. Wazee hawa ni mfano wa kuigwa kwani ni wakarimu na wana upendo kwa watu.

FOR ONLINE USE ONLY

### Maswali

1. Bainisha virai nomino katika kifungu cha habari ulichokisoma.
2. Kwa kutumia kifungu cha habari ulichokisoma, bainisha miundo ya kirai nomino.
3. Andika virai nomino vitano, ambavyo havipo katika habari uliyoisoma.
4. Eleza maana ya kirai nomino kwa maneno yako mwenyewe.

### Zoezi la 2.2

Kwa kutumia miundo mbalimbali ya kirai nomino, tunga sentensi tano zinazozungumzia mazingira ya darasa au shule yako. (Wasilisha darasani kwa kufafanua muundo wa kila sentensi).



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 21 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Zingatia

Neno kuu katika kirai nomino ni nomino au kiwakilishi. Kirai nomino hubainika au kutambulika katika sentensi kwa kuangalia uhusiano wa nomino moja au zaidi na maneno mengine katika tungo. Kirai nomino kinaweza kuundwa na:

(a) Nomino moja tu, mfano: baba;

(b) Kiwakilishi pekee, mfano: huyu;

(c) Nomino na kivumishi, mfano: mtoto mrefu;

(d) Kiwakilishi na kivumishi, mfano: ninyi warembo;

(e) Nomino, kiunganishi na nomino, mfano: mama na mtoto;

(f) Nomino na kirai kihusishi, mfano: mtoto wa mjomba;

(g) Nomino na kishazi tegemezi, mfano: jogoo aliyewika usiku.

## Kirai kivumishi (KV)

### Kazi ya 2.7

**Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Itala ni kijana mwenye umbo la miraba minne. Kutokana na uwezo wake wa kushawishi, amewahamasisha vijana wenzake, kuanzisha umoja wa kusaidiana katika shughuli za kijamii, kama vile, sherehe. Kwa upande mwingine, kijana huyo ameonekana mwenye bidii na upendo wa hali ya juu kwa majirani. Hivi karibuni, imebainika kuwa, kijana huyo licha ya kuwa mtanashati, ana mkono wa birika. Pale inapofika zamu yake ya kuchangia fedha wenzake, huwa mdanganyifu. Pia, Itala ni kijana mwenye kiburi. Alidhaniwa kuwa ni kijana hodari kutokana na uchapakazi wake. Vilevile, uvaaji wake ulitufanya tuamini kuwa ana hekima, kumbe sivyo.

FOR ONLINE USE ONLY

### Maswali

1. Orodhesha virai vivumishi vilivyojitokeza kwenye kifungu cha habari.
2. Eleza namna ulivyoweza kutofautisha virai vivumishi na virai nomino katika habari uliyoisoma.
3. Taja sifa za virai vivumishi unazozifahamu.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 22 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Zoezi la 2.3

Bainisha virai vivumishi vinavyojitokeza katika sentensi zifuatazo:

(a) Mtoto mdogo anasoma kitabu polepole.
(b) Mwanafunzi hodari amefaulu mtihani.
(c) Agapita ni mweusi wa kuvutia.
(d) Gauni jeupe lililochanika limeshonwa.
(e) Kaka mwenye duka kubwa kijijini amewasili.
(f) Nyumba yenye wapangaji wengi imeungua moto.

### Zingatia

Neno kuu katika kirai kivumishi ni kivumishi. Kirai hiki hukamilishwa na vivumishi, aina nyingine za maneno au kirai kingine. Kirai kivumishi hufanya kazi ya kufafanua nomino au kiwakilishi katika sentensi. Kirai Kivumishi huweza kubainika au kutambulika katika sentensi kutokana na muundo wake. Muundo huo hutawaliwa na neno kuu ambalo ni kivumishi. Ifuatayo ni miundo ya kirai kivumishi:

(a) Kivumishi pekee, mfano: mzuri;
(b) Kivumishi na kivumishi, mfano: mkorofi mwenye makengeza;
(c) Kivumishi na kishazi tegemezi, mfano: mtundu aliyeumia, pale palipojazwa kifusi;
(d) Kivumishi na kirai kihusishi, mfano: nzuri ya mwalimu, kubwa ya ukutani;
(e) Kivumishi na kirai nomino, mfano: mwenye kuku wakubwa.
(f) Kivumishi na kirai kielezi, mfano: ndefu sana.

## Kirai kitenzi (KT)

### Kazi ya 2.8

**Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Mzee Chikala baada ya kustaafu alilipwa milioni 120 kama kiinuamgongo. Alitumia nusu ya fedha hizo kujenga nyumba ili aondokane na adha ya kupanga. Baada ya kumaliza, alizungushia wigo. Vilevile, alipanda maua na miti mbalimbali ya matunda eneo lililobaki. Sasa, Mzee Chikala anaishi kwa raha mustarehe, akipata kivuli na matunda.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 23 9/6/21 5:52 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Katika kifungu cha habari ulichokisoma, bainisha virai vitenzi, kisha viorodheshe.
2. Andika virai vitenzi vitano, ambavyo havipo katika kifungu cha habari ulichokisoma.

### Kazi ya 2.9

1. Soma matini au gazeti lolote, kisha bainisha virai nomino, virai vivumishi na virai vitenzi vilivyojitokeza katika matini hiyo.
2. Chunguza picha ifuatayo, kisha tunga sentensi tano kutokana na picha hiyo na bainisha virai vitenzi vitakavyojitokeza katika sentensi hizo.



### Zingatia

Neno kuu katika kirai kitenzi ni kitenzi. Kirai kitenzi huonesha uhusiano uliopo baina ya kitenzi na maneno mengine katika sentensi. Kirai kitenzi huweza kujitokeza kwa namna tofautitofauti kama ifuatavyo:

(a) Kitenzi kikuu pekee, mfano: lala, komaa;

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Kitenzi kisaidizi kimoja au zaidi na kitenzi kikuu, mfano: kwenda kulima, alikuwa anataka kula;

(c) Kitenzi kikuu na kielezi, mfano: palilia vizuri, soma barabara;

(d) Kitenzi kikuu na kirai kihusishi, mfano: kula kwa maringo, tembea kwa miguu;

(e) Kitenzi kikuu na nomino moja au zaidi, mfano: andika barua, panda mahindi;

(f) Kitenzi kishirikishi na kivumishi, mfano: ni mvivu, ndiye mchafu;

(g) Kitenzi kishirikishi na nomino, mfano: yu mwalimu, si mtoto;

(h) Kitenzi na kishazi tegemezi, mfano: cheza walipokuandalia, nenda alikokimbilia.

## Kirai kielezi (KE)

### Kazi ya 2.10

**Soma kisa kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Ilikuwa saa sita mchana, wakati nikitoka shambani, jua lilikuwa kali sana. Niliamua kukaa kivulini kupata upepo kidogo. Siku hiyo, nilikuwa na uchovu mwingi kutokana na shughuli za shamba. Karibu na mti niliokuwa nimekaa, kulikuwa na shimo lililoonekana dogo, lakini ndani yake kulikuwa na maajabu. Ghafla, nilimwona mnyama mrefu aliyeonekana kama paka kichwani na kama nyoka mwenye manyoya meusi kuanzia sehemu za shingoni hadi mkiani. Kwa kuhofia usalama wangu, nilisogea mbali kidogo na ule mti, ili kumtazama mnyama huyo. Mnyama alitoka ndani ya shimo polepole huku mwili wake ukimeremeta. Alipanda juu ya mti huo mkubwa kwa maringo huku nikimwangalia. Baada ya muda, nilijikuta nipo kitandani nimelala. Nimefikaje kitandani, nilijiuliza. Kwa hofu nilijigeuza kimyakimya, huku mapigo ya moyo yakienda mbio.

FOR ONLINE USE ONLY

### Maswali

1. Katika kisa ulichokisoma, bainisha virai vielezi, kisha viorodheshe.
2. Onesha virai vielezi vitano, ambavyo havipo katika kisa ulichokisoma.
3. Kwa maneno yako mwenyewe, eleza maana ya kirai kielezi.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya 2.11**

Chunguza picha hii, kisha tunga sentensi tano zenye virai vielezi kuhusiana na picha hiyo.



## Zingatia

Kirai kielezi ni kirai ambacho neno kuu ni kielezi. Kirai kielezi huweza kuwa na kielezi kimoja au zaidi. Kirai kielezi huundwa na:

(a) Kielezi pekee, mfano: polepole, mara kwa mara;

(b) Kielezi na kirai kihusishi, mfano: nyumbani kwa mjomba, juu ya mti;

(c) Kielezi na kielezi, mfano: usiku kucha, asubuhi mno, vizuri sana.

## Kirai kihusishi (KH)

**Kazi ya 2.12**

**Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Mwanahawa na Roza ni wanafunzi wa kidato cha tatu katika shule ya sekondari Ipitimbi. Wanafunzi hao wanapenda kusoma kwa bidii. Katika matokeo ya muhula wa kwanza, wote wawili walifaulu vizuri masomo yao. Mwalimu wao wa darasa aliwapatia zawadi nzuri sana. Wanafunzi wenzao waliwafurahia sana. Kila mwanafunzi alitamani apewe yeye zawadi hizo. Hata hivyo, mwalimu wa darasa aliwasisitiza wanafunzi wote wasome kwa bidii. Vilevile, aliwaahidi kuandaa zawadi nyingi zaidi katika muhula wa pili.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Bainisha virai vihusishi kutoka katika kifungu cha habari ulichokisoma.
2. Unafikiri virai vihusishi vimeundwa kwa namna gani?

## Zingatia

Neno kuu la kirai kihusishi ni kihusishi. Mara nyingi kirai kihusishi hakiwezi kuwa na muundo wa kihusishi pekee, bali hufuatana na aina nyingine za maneno ili kukamilisha muundo wake. Kirai kihusishi kinaweza kutokea mahali popote katika sentensi. Kirai kihusishi huundwa na:

(a) Kihusishi na nomino, mfano: katika jumba bovu, cha mtoto, kwa kijiko;

(b) Kihusishi na kielezi, mfano: ya mkononi, hadi bondeni, la barabarani.

### Zoezi la 2.4

1. Panga vizuri virai vifuatavyo ili viweze kuunda sentensi zenye maana.
   (a) na kuimba wote wanafunzi madaha kwa walimshangilia
   (b) matunda wa uuzaji na kutokana nyingi pesa hupata hawa wakulima
   (c) letu analima baba dogo bidii  shamba kwa
   (d) sana mbuzi leo amekonda tuliyemchinja alikuwa huyo
   (e) ni  wa zawadi nyingi aliyepata kijana kuogelea nzuri hodari
2. Andika hadithi fupi yenye maneno yasiyozidi 150 na yasiyopungua 100, kisha bainisha virai vyote vilivyojitokeza.
3. Tofautisha muundo wa virai vitenzi na virai vielezi.
4. Ujifunzaji wa aina za virai unakusaidiaje katika maisha yako ya kila siku?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya 2.13**

Tunga hadithi kuhusu mazingira ya shule, kisha bainisha virai vitenzi, virai vihusishi na virai vielezi kama vilivyojitokeza katika hadithi hiyo.

## Tungo kishazi

**Kazi ya 2.14**

**Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Mwalimu Hango anapenda maendeleo ya wanafunzi wake wa Kidato cha Tatu. Jana aliwaketisha chini ya kivuli akiwahimiza wasome kwa bidii. Aliwapa mifano ya faida zitokanazo na elimu. Hakwenda mbali kutafuta mifano, bali alianzia hapohapo kijijini. Alizungumzia habari za kijana wa Mzee Masisi aliyekuwa mwanafunzi mwenye bidii sana darasani. Kwa sasa, kijana huyo ni Balozi huko Marekani. Alitoa mifano dhahiri ya watu ambao wamefanikiwa kiuchumi, kisiasa na kijamii kutokana na elimu. Alisema "Elimu humwinua mtu na humpaisha mithili ya ndege angani." Mwalimu alipomaliza mazungumzo, alimtaka kila mmoja aeleze malengo yake kuhusu safari yake ya masomo. Wapo waliosema wanataka kuwa wataalamu wa lugha, walimu na wengine walitaka kuwa wahadhiri. Wapo waliotaka kuwa marubani na wengine wachumi wa kimataifa. Kila mmoja aliondoka akiwa na ari ya kuanza ukurasa mpya wa masomo.

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

1. Bainisha vishazi vilivyotumika kwenye kifungu cha habari, kisha uviorodheshe.
2. Umetumia mbinu gani kubainisha vishazi hivyo katika kifungu cha habari?
3. Andika vishazi sita ambavyo havipo katika kifungu cha habari.
4. Eleza maana ya vishazi kwa maneno yako mwenyewe.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 28 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 2.5**

**Chunguza tungo zifuatazo katika kundi A na kundi B, kisha jibu maswali yanayofuata.**

| **Kundi A** | **Kundi B** |
|---|---|
| wawili | sisi tutamuaga leo |
| kile kinene | yaliondolewa kitambo |
| wakubwa na wadogo | tuliyopewa na kiranja |
| rafiki yangu | limepata ajali |
| wale wengine | hatujachukua vitambulisho |
| nyumbani | kisu kilichopotea |

**Maswali**

1. Bainisha tungo zinazotoa taarifa kamili na zile zisizotoa taarifa kamili katika kundi B. Eleza kwa nini?
2. Orodhesha aina ya vishazi kutokana na tungo ulizozichunguza.
3. Kwa kutumia tungo ulizochunguza, kwa maneno yako, fasili maana ya kishazi.
4. Tungo za kundi A zinaitwaje?

## Zingatia

Kishazi ni neno au mpangilio wa maneno wenye kitenzi kimoja ndani yake. Kitenzi hicho kinaweza kuwa kikuu au kilichoshushwa hadhi kwa kuwekewa viambishi vya urejeshi, masharti na kuambatana na umbo la "amba" au viunganishi tegemezi. Tungo zifuatazo ni mfano wa tungo kishazi. (a) *Amepita hapa.* (b) *Jembe lililonunuliwa juzi limeharibika.* (c) *Amekunywa uji wote*. Vishazi hubainishwa kwa kuzingatia muundo wake. Hivyo, kishazi kinaweza kugawanyika katika aina mbili, nazo ni: kishazi huru (K/Hr) na kishazi tegemezi (K/Tg au β).

Katika lugha ya Kiswahili, vishazi huwa na sifa zinazovitambulisha na kuvitofautisha na aina nyingine za tungo. Zifuatazo ni sifa za vishazi: kishazi huwa ndani ya sentensi, mfano: *Migomba iliyokatwa* / imechipua tena; kishazi kimojawapo katika sentensi huwa na o-rejeshi, au kiambishi cha masharti, mfano: *Somo lili**lo**fundishwa* / lilieleweka vizuri au *Mwalimu a**ki**fika* nitamuuliza swali. Baadhi ya vishazi haviwezi kutoa maana inayojitosheleza, mfano:
(a) *Mbuzi anayetafutwa* / yupo zizini. (b) *Kibuyu alichonipatia bibi* / kina asali; Kishazi kimojawapo katika sentensi huwa na hadhi ya sentensi sahili, mfano:



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 29 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kijana aliyefika jana / *analima bustani;* kishazi huweza kuundwa na viunganishi tegemezi, mfano: (a) *Kama* atakuja, nitampeleka shuleni. (b) Nitaenda sokoni, *endapo* nitapata usafiri; kishazi ni ngazi ya juu kuliko kirai na ya chini kuliko sentensi, mfano: Neno ⟶ Kirai ⟶ Kishazi ⟶ Sentensi

## Zoezi la 2.6

1. Chunguza sentensi zifuatazo, kisha bainisha vishazi.
   (a) Mwanafunzi aliyetoroka amepita hapa.
   (b) Gari lililonunuliwa juzi linapendwa na watoto.
   (c) Wagonjwa walioruhusiwa wamekunywa uji wote.
   (d) Timu yetu ikirejea tutaipokea kwa shangwe.
   (e) Kiti kilichovunjika jana kimetengenezwa vizuri.
2. Je, vishazi ulivyobainisha katika swali la kwanza, vinatofautianaje kimuundo na kimaana?

## Kazi ya 2.15

**Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Tunga sentensi tano kutokana na picha hii, kisha uoneshe vishazi vilivyomo.
2. Bainisha vishazi huru na vishazi tegemezi kutokana na sentensi zifuatazo:
   (a) Wanafunzi waliotumbuiza katika tukio hilo walitia fora.
   (b) Mgeni aliyealikwa alifika kwa wakati.
   (c) Vitabu walivyobeba vilikuwa vya Kiswahili.
   (d) Upepo unavuma kwa kasi.

## Zoezi la 2.7

1. Andika tungo tano zenye vishazi huru.
2. Andika tungo sita zenye vishazi tegemezi.
3. Tunga sentensi sita, zenye vishazi huru na vishazi tegemezi, kisha bainisha tofauti kati ya kishazi huru na kishazi tegemezi.
4. Kamilisha taarifa za vishazi tegemezi vya swali la 2 hapo juu kwa kuongezea vishazi huru.
5. Ainisha vishazi katika tungo zifuatazo kwa kupigia mstari. Weka alama K/Tg katika kishazi tegemezi na alama K/Hr katika kishazi huru.
   (a) Mtoto uliyemwona amepata tuzo.
   (b) Amesimama nyuma ya lango lililobomoka.
   (c) Kaka anacheza mpira wa miguu.
   (d) Binti aliyekalia kiti kirefu ni mwanafunzi wa shule ya Sekondari Songambele.
   (e) Mahali palipobomoka hapajarekebishwa hadi leo.
   (f) Chumbani walimokaa mna maji mengi.
   (g) Yale machungwa matamu yaliyonunuliwa na mwalimu wa zamu yameibiwa asubuhi.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 31 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zingatia**

Kishazi tegemezi hutoa taarifa isiyojitosheleza. Kishazi hiki hutegemea kishazi huru ili kukamilisha taarifa yake. Kishazi hiki huundwa na:

(a) Vitenzi vyenye viambishi vya o-rejeshi ambavyo husababisha utegemezi, mfano: -o-, -ye-, -cho-, -po-, na -zo-. Mifano ya vishazi tegemezi:

- (i) Wanafunzi wote *walioandikishwa* / watakuja kesho,
- (ii) Embe limedondoka karibu na *walipochimba* shimo.

(b) Vitenzi vyenye viambishi vya masharti ambavyo husababisha utegemezi, mfano: -ki-, -ngali-, -ngeli-, na -nge-. Mifano ya vishazi tegemezi:

- (i) Kijana *angalisoma* kwa bidii angalifaulu,
- (ii) Mwalimu *akija* wanafunzi watanyamaza kimya.

(c) Umbo la "amba" lenye viambishi vya o-rejeshi ambavyo husababisha utegemezi. Mfano wa viambishi hivyo katika umbo hili ni: ambaye, ambao, ambapo, ambacho.

- (i) *Ambaye* ameshinda mtihani,
- (ii) *Ambapo* pamezuiliwa.

(d) Viunganishi tegemezi mfano: ijapokuwa, wakati, endapo, katika, kama, iwapo, mfano:

- (i) *Ijapokuwa* mwalimu anafundisha,
- (ii) *Katika* jitihada ya kujinasua,
- (iii) *Endapo* atakuja leo.

Sifa za vishazi tegemezi ni pamoja na; kutoa taarifa isiyojitosheleza, mfano: (i) Kilichokuwa mtoni. (ii) Aliyenunuliwa jana.

Kitenzi chake huwa na o-rejeshi, mfano: Ulipopigwa watu walishangilia; Kishazi tegemezi kinaweza kuondolewa katika sentensi bila kuathiri maana ya msingi, mfano: Kiti *ulichokalia* kimeliwa na mchwa.

Kuna vishazi tegemezi vya aina mbili, yaani kishazi tegemezi kivumishi (βV) na kishazi tegemezi kielezi (βE). Kishazi tegemezi kinapokuwa katika nafasi ya kivumishi hutoa taarifa au kufafanua nomino au kiwakilishi katika tungo. Kishazi tegemezi hufanya kazi ya kivumishi katika tungo.

Mfano: (i) Mnyama *aliyetoroka hifadhini* / amerejeshwa na askari wa hifadhi,
(ii) Wali *uliopikwa juzi* / haukuwatosha wageni wote.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kishazi tegemezi kinapofanya kazi ya kielezi hutoa maelezo ya kufafanua kitenzi, kivumishi na kielezi chenyewe katika sentensi. Kishazi hiki hujitokeza mara tu baada ya kitenzi katika sentensi. Hutumia viambishi vya o-rejeshi kama vile *-po-*, *-mo-* na *-ko-* kuelezea mahali pa kufikirika au mahali pasipo dhahiri.
Mfano: (i) Alifurahi *aliposifiwa*, (ii) Nyoka amekimbilia *wanakofyeka* majani.

Kishazi huru hutoa ujumbe au taarifa iliyokamili. Kishazi hiki huundwa na kitenzi kikuu, kifungu tenzi au kitenzi kishirikishi kimoja,
Mfano: (i) Mwalimu mgeni aliyefika jana / *atatunga wimbo*,
(ii) Kiatu kilichonunuliwa / *ni kizuri sana*.

Kishazi huru huwa na sifa zifuatazo:

(a) Kitenzi kikuu kimoja au kifungu tenzi.
Mfano: Miche iliyonunuliwa *imestawi vizuri* sana;

(b) Huundwa na kitenzi kishirikishi.
Mfano: Kijana aliyeondoka *si* mwalimu wetu;

(c) Kishazi huru hutoa taarifa inayojitosheleza.
Mfano: Mbuzi walionona *wanakula mahindi shambani kwa Mzee Mtundi*;

(d) Kishazi huru kina hadhi ya sentensi sahili.
Mfano: Mashine ya kusaga nafaka iliyohitajika *imenunuliwa leo mchana*.

Katika mfano wa sentensi (d) hapo juu, kishazi huru "imenunuliwa leo mchana" kinaweza kusimama peke yake kama sentensi.

Katika tungo, vishazi huwa na dhima mbalimbali kama ifuatavyo: kishazi hukamilisha taarifa katika tungo, mfano: Mtoto mtundu aliyepanda mtini *ameumia*; hufanya kazi ya kivumishi, mfano: Mtoto *aliyevaa gauni jeupe*; hufanya kazi ya kielezi, mfano: Watoto walisimama *walipochomea takataka*; kishazi tegemezi hufanya kazi ya kiima katika tungo, mfano: *Kilichovunjwa* kimetengenezwa.

FOR ONLINE USE ONLY

## Tungo sentensi

### Kazi ya 2.16

**Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

1. Sentensi ndiye mama, mwenye watoto watatu,
   Kazaa kwa mpango, hakika hakukosea,
   Akawapa majina, majukumu kutekeleza,
   Sahili, Changamani na Ambatani wa viungo.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 33 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Sahili ni dada yao, yeye hana utata,
Katulia kwa hakika, kwa miundo ilopangika,
Vitenzi vikuu kabeba, ukitunga hutetereki,
Kisaidizi kadhalika, kuipamba sentensi,
Mdogo wake shirikishi, kaongeza uhusiano.

3. Wa pili ni Changamani, sentensi kuitunza,
Kuijaliza maana, kwa pambo lilo azizi,
Changamani kwa miundo, yeye ni mahiri,
Kaweka chake kikao, kwa sahili kumuomba,
Kusaidia tegemezi, kukamilisha maana.

4. Hakutaka omboleza, kajiongeza kwa hakika,
Kaweka mbili tegemezi, na sahili karibisha,
Ngali na ngeli aliwaza, kuchukua tegemezi,
Zilizojikamilisha, kwa maana iloshiba.

5. Ambatani mwanana, yeye katia fora,
Kwa muundo stahiki, mamaye kampamba,
Kaunganisha sahili, kwa viungo maridhawa,
Yeye hakuwa bahili, kuijenga yake tungo.

6. Kaiweka Changamani, katika wake muundo,
Na Sahili ikatungwa, kutumia viunganishi,
Sahili mbili zaidi, kaijenga yake tungo,
Kuimiliki Sahili, sambamba na Changamani.

7. Sentensi kazeeka, anao na wajukuu,
Kiima na kiarifu, mkwaju wamshikia,
Kiima kashika jina, la nafasi ya mtenda,
Arifu mtekelezaji, kumfikisha nyumbani.

8. Pia, vikundi virai, hakika vimesimama,
Katika kuchanganua, kwa njia zilo bayana,
Matawi na visanduku, weledi kuutumia.

9. Ili kuijenga nyumba, isokuwa matata,
Furahisha wapangaji, na wale walo wenyeji,
Sentensi kuzing'amua, na lugha kuitanua.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Kutokana na shairi ulilolisoma, unafikiri kuna aina ngapi za sentensi?
2. Ainisha miundo ya kila aina ya sentensi kutokana na shairi.
3. Mshairi anaposema, wajukuu wa sentensi anamaanisha nini?
4. Kwa mujibu wa shairi ulilolisoma, ni njia zipi za uchanganuzi wa sentensi zimebainishwa?
5. Tunga sentensi sahili, kisha tenga sehemu kuu za sentensi hiyo.

### Kazi ya 2.17

**Chunguza sentensi zifuatazo, kisha jibu maswali.**

1. Magari yamekwama pale bondeni.
2. Tutafyeka viwanja, kisha tutafagia barabara.
3. Madhumuni ya safari yangu ni kukuona tu.
4. Ameipata barua aliyokuwa anaisubiri.
5. Ningelikuwa na fedha ningelinunua baiskeli.

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

1. Je, umebaini nini baada ya kuchunguza sentensi hizi?
2. Tenga sentensi zenye vishazi tofauti katika makundi anuai.
3. Ainisha sentensi ulizotenga kimuundo.

### Kazi ya 2.18

Soma matini mbalimbali kubaini kiima na kiarifu kwenye aya kadhaa za matini hizo. Andika majibu yako na kufanya uwasilishaji darasani.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 35 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zingatia

Tungo yenye kirai kitenzi kimoja au zaidi inayotoa taarifa kamili kuhusu jambo fulani huitwa sentensi. Sentensi ni ngazi ya juu kabisa ya tungo yenye muundo wa kirai nomino na kirai kitenzi.

Katika mkabala wa kimapokeo (kidhima) sentensi yoyote ya Kiswahili huwa na sehemu kuu mbili. Sehemu inayokaliwa na mtenda au mtendwa wa jambo na sehemu inayokaliwa na tendo na vijalizo vyake. Kwa mujibu wa wanamapokeo, sehemu inayokaliwa na mtenda au mtendwa huitwa kiima (K) na sehemu inayokaliwa na tendo na vijalizo vyake huitwa kiarifu (A).

Mtenda au mtendwa wa jambo anaweza kuoneshwa bayana katika kiima au asiwe bayana au kapa (Ø). Kiima huwa na miundo ifuatayo:

(a) Nomino/kiwakilishi pekee, mfano: *Mtoto* anakula chakula;

(b) Nomino na nomino, mfano: *Baba na mama* wanalima;

(c) Nomino na kivumishi, mfano: *Kijana mvivu* amelala njaa;

(d) Nomino, kivumishi na kielezi, mfano: *Mbwa mkali sana* amepigwa risasi;

(e) Nomino na kishazi tegemezi, mfano: *Ng'ombe aliyevunjika mguu* ameuzwa;

(f) Kishazi tegemezi peke yake, mfano: *Kinachotafutwa* kimeonekana.

Kiarifu huwa na miundo ifuatayo:

(a) Kitenzi kikuu peke yake, mfano: Mtoto *anacheza*;

(b) Kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu, mfano: Diamond *alikuwa anaimba*;

(c) Kitenzi kishirikishi, mfano: Maua ni *mkulima hodari*;

(d) Kitenzi au kirai kitenzi na nomino, mfano: Selestino *amekalia kiti*;

(e) Kitenzi au kirai kitenzi na kielezi, mfano: Fundi wangu *anashona vizuri*.

Upande wa kiarifu huweza kuwa na vipashio kama vile prediketa, shamirisho na chagizo.

Nafasi inayokaliwa na vitenzi katika sentensi huitwa prediketa (P).

Mfano: (a) Mti mkubwa *umeangukia* nyumba.

(b) Chupa zote *zimetunzwa* kabatini.

Shamirisho (SH) ni nomino au kikundi nomino ambacho hukamilisha taarifa ya kitenzi. Mfano: (a) Baba yangu amenunua *machungwa mawili*.

(b) Kaka yake alilima *shamba kubwa*.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 36 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Chagizo ni neno linalotoa taarifa ya ziada ambayo siyo ya lazima katika kukamilisha sentensi. Nafasi inayokaliwa na vielezi katika sentensi huitwa chagizo (CH).

Mfano: (a) Mtoto analia *sana*.

(b) Kalamu yangu imevunjika *vibaya*.

Katika mkabala wa kimuundo, sentensi hupambanuliwa kwa kuangalia viambajengo vinavyoiunda. Istilahi zinazotumika kuigawa sentensi ni zile za kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT). Viambajengo hivyo (KN na KT) huendelea kugawanywa katika viambajengo vingine yaani kirai kivumishi (KV), kirai kielezi (KE) na kirai kihusishi (KH). Mgawanyo huu huendelea hadi kufikia ngazi ya neno na wakati mwingine viambajengo vya neno hugawanywa zaidi.

Sentensi huwa na sifa zifuatazo: sharti ibebe ujumbe unaojitosheleza; ni ngazi ya juu katika tungo; huweza kuwa na kitenzi kikuu kimoja na kitenzi kisaidizi kimoja au zaidi; inaweza kuwa na vishazi viwili yaani kishazi huru na kishazi tegemezi; huonesha hali mbalimbali, mfano: amri, maelezo, swali au ombi; inaweza kujengwa na kishazi huru kimoja au zaidi.

## Sentensi sahili

### Zoezi la 2.8

1. Tunga sentensi sahili mbili zenye miundo mbalimbali, kisha ainisha miundo hiyo kwa kutumia t, Ts, T.
2. Tunga sentensi sahili mbili zenye kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu.
3. Tunga sentensi sahili tatu zenye kitenzi kikuu tu.
4. Andika sentensi sahili mbili kwa kila kitenzi kishirikishi (ndiye, ndimi, ndimo, ni, si).
5. Kila sentensi ina muundo wake. Thibitisha dai hili kwa kutumia sentensi sahili.

FOR ONLINE USE ONLY

### Zingatia

Sentensi sahili huwa na kitenzi kikuu kimoja au kirai kitenzi na hubeba wazo kuu moja. Sentensi sahili ina muundo wake bayana ambao huitofautisha na aina nyingine za sentensi.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 37 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Sentensi sahili huweza kuundwa kwa namna anuwai kama ifuatavyo:

(a) Kitenzi kikuu kimoja (T),
mfano: Twiga *wanaishi* porini katika eneo lenye miti mirefu.
Wanakijiji *walikata* mti;

(b) Kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu (Ts + T),
mfano: Karatasi *zilikuwa zimezagaa* kila mahali;

(c) Vitenzi visaidizi viwili na kitenzi kikuu (Ts +Ts+T),
mfano: *Tulidhani tutamkuta* akicheza mpira na Bakari hapa kwako;

(d) Vitenzi visaidizi vitatu na kitenzi kikuu (Ts+Ts+Ts+T),
mfano: Vijana *walikuwa wanataka kwenda kuomba* msaada wa chakula;

(e) Kitenzi kishirikishi (t),
mfano: (i) Yule *ni* mwalimu wa somo la Kiswahili Kidato cha Tatu.
(ii) Huu *si* mmea wa dawa ya watoto hata kidogo.
(iii) Mwalimu *alikuwa* shuleni mnamo saa saba.

## Sentensi changamani

**Kazi ya 2.19**

1. Tunga sentensi changamani tano zenye miundo mbalimbali.
2. Chunguza sentensi zifutazo, kisha jibu maswali.
   (a) Ng'ombe aliyepotea kundini amepatikana.
   (b) Ijapokuwa Diana alikuwa mgonjwa, alifanya mtihani wake vizuri.
   (c) Nguo zilizoanikwa zimeangushwa na upepo.
   (d) Ndama ambaye alivunjika mguu alipokuwa anaruka mtaro amechinjwa.
   (e) Bibi alivunja chungu kilichokuwa na maji mengi alipotoka mtoni.
   (f) Huyu ni mwanafunzi aliyepoteza viatu alivyoazima alipokuwa anacheza mpira.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 38 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Bainisha sentensi zenye muundo wa kishazi huru kimoja na tegemezi kimoja.
2. Bainisha sentensi yenye kishazi huru kimoja na vishazi tegemezi viwili.
3. Bainisha sentensi yenye kishazi huru kimoja na vishazi tegemezi zaidi ya viwili.

## Zingatia

Sentensi changamani aghalabu huwa na kishazi huru kimoja na kishazi tegemezi kimoja au zaidi. Sifa kuu ya sentensi hii ni kuwa na kishazi tegemezi kinachotegemea kishazi huru ili kukamilisha taarifa. Uhusiano wa vishazi hivyo ni ule wa kishazi kimoja kutegemea kingine. Aidha, kishazi hiki huhitaji kishazi huru kukamilisha taarifa ya sentensi. Katika sentensi zifuatazo, kishazi tegemezi kimeandikwa kwa italiki, mfano: (i) Madarasa *yaliyosafishwa* yamefungwa.
(ii) Mtoto *aliyepotea* ameonekana.

Sentensi changamani huweza kuundwa na:

(a) Kishazi tegemezi kimoja na kishazi huru kimoja, mfano:
(i) Madarasa yaliyosafishwa yamefungwa.
(ii) Mwanafunzi aliyeleta vitabu hivi ametoroka;

(b) Vishazi tegemezi viwili, na kishazi huru kimoja, mfano:
Mama alipotoka mjini alivunja televisheni iliyokuwa imenunuliwa na baba;

(c) Vishazi tegemezi viwili, mfano:
Angelisoma kwa bidii, angelifaulu mtihani.

## Sentensi ambatani

**Kazi ya 2.20**

Soma matini au gazeti, kisha bainisha sentensi ambatani kumi zilizojitokeza na uziwasilishe darasani.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya 2.21**

1. Tunga sentensi ambatani sita zenye miundo tofauti, kisha bainisha muundo wa kila sentensi.
2. Chunguza sentensi zifuatazo, kisha jibu maswali.
   (a) Nimekula lakini sijashiba.
   (b) Utanipa kiatu changu au niondoke na begi lako.
   (c) Alikula, akaoga, akalala.
   (d) Mwambie aninunulie mbili.
   (e) Mtoto aliyefaulu mtihani ni mwanangu lakini aliyemsindikiza kupokea zawadi ni mpwa wangu.

## Maswali

1. Bainisha sentensi ambatani zenye muundo wa sentensi sahili mbili.
2. Bainisha sentensi ambatani yenye sentensi changamani na sentensi sahili.

### Zingatia

Sentensi ambatani huundwa na sentensi mbili au zaidi. Sentensi ambatani huweza kuwa na kiunganishi kimoja au zaidi. Vilevile, huweza kutenganishwa kwa alama ya mkato (**,**). Sentensi ambatani huweza kuundwa na:

(a) Sentensi sahili mbili au zaidi, mfano:
   (i) Nyumba imeezekwa lakini inavuja.
   (ii) Walimsukuma Juma akaanguka, akavunjika mkono.

(b) Sentensi changamani moja na sentensi sahili moja au zaidi, mfano:
   (i) Mayai yaliyonunuliwa yalidondoka chini japokuwa alibeba kwa uangalifu.
   (ii) Walipotoka pale nyumbani tuliwaona lakini wao hawakutuona wala hawakupata habari zetu.

(c) Sentensi changamani mbili na sentensi sahili mbili, mfano:
   (i) Alinunua mashuka yaliyofumwa na foronya zilizotariziwa.
   (ii) Ng'ombe aliyevunjika mguu amepona na mchungaji aliyekuwa anamhudumia ameondoka.

FOR ONLINE USE ONLY


## Uchanganuzi wa sentensi

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Mkabala wa kimapokeo

**Kazi ya 2.22**

**Chunguza mchoro ufuatao, kisha jibu maswali yanayofuata.**




### Maswali

1. Mchoro huo umechorwa kwa kuzingatia umbo gani?
2. Mchoro huo una msaada wowote katika taaluma ya uchanganuzi wa sentensi? Fafanua.
3. Onesha uhusiano uliopo kati ya sentensi na mchoro huo.




Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 41 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya 2.23**

**Chunguza mifano ya uchanganuzi wa sentensi, kisha jibu maswali yanayofuata.**

(a) Nasibu anacheza mpira vizuri sana.




(b) Shehiza ni mwalimu.

| S. Sahili | | |
|---|---|---|
| K | A | |
| N | P | SH |
| | t | N |
| Shehiza | ni | mwalimu. |



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 42 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Njia zipi za uchanganuzi wa sentensi zimetumika katika michoro hiyo?
2. Ni hatua ipi ya mwanzo kabisa katika uchanganuzi wa sentensi?
3. Hatua ya tatu katika uchanganuzi wa sentensi ni ipi?

### Njia ya majedwali (visanduku)

Ifuatayo ni mifano ya uchanganuzi wa sentensi kwa njia ya majedwali.

(i) Yule alikataa mawazo yetu kabisa.

<table>
<tr><th colspan="5">S. Sahili</th></tr>
<tr><td>K</td><td colspan="4">A</td></tr>
<tr><td rowspan="2">W</td><td>P</td><td colspan="2">SH</td><td>CH</td></tr>
<tr><td>T</td><td>N</td><td>V</td><td>E</td></tr>
<tr><td>Yule</td><td>alikataa</td><td>mawazo</td><td>yetu</td><td>kabisa</td></tr>
</table>

FOR ONLINE USE ONLY

(ii) Nguo zilizofuliwa zimekauka vizuri.


<table>
<tr><th colspan="4">S. Changamani</th></tr>
<tr><td colspan="2">K</td><td colspan="2">A</td></tr>
<tr><td rowspan="2">N</td><td>βV</td><td>P</td><td>CH</td></tr>
<tr><td>V</td><td>T</td><td>E</td></tr>
<tr><td>Nguo</td><td>zilizofuliwa</td><td>zimekauka</td><td>vizuri</td></tr>
</table>

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


### Njia ya matawi (ngoe)

Ifuatayo ni mifano ya uchanganuzi wa sentensi kwa njia ya matawi.

(i) Dada atachimba viazi kesho na wewe utachanja kuni.




(ii) Nitahudhuria lakini sitakaa sana.





Katika sentensi hii, kiima hakikutajwa, lakini nafasi ya kiima inaeleweka. Kiima hicho huitwa kiima kapa (Ø). Kiwakilishi nafsi huru huwekwa kwenye mabano kusimama sehemu ya mtenda ambaye hakutajwa.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 44 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) Mbuzi aliyenunuliwa juzi amechinjwa leo asubuhi.




## Zingatia

Uchanganuzi wa sentensi ni uainishaji wa vipashio mbalimbali vinavyoijenga sentensi hiyo. Sentensi huchanganuliwa kwa kuanza na vipashio vikubwa kwenda vipashio vidogo.

Uchanganuzi wa sentensi kwa kutumia mkabala wa kimapokeo (kidhima) huzingatia dhima ya kila kipashio katika tungo. Uchanganuzi huu hufuata hatua zifuatazo:

(a) Kubaini aina ya sentensi inayochanganuliwa;

(b) Kubaini sehemu kuu za sentensi ambazo ni kiima na kiarifu;

(c) Kubaini vipashio vya kiima na kiarifu;

(d) Kubaini aina za maneno yanayoijenga sentensi hiyo, mfano: nomino (N), kiwakilishi (W), kivumishi (V), kielezi (E), kihusishi (H), kihisishi (Hs), kitenzi (T) na Kiunganishi (U);

(e) Kuiandika sentensi.

Uchanganuzi wa sentensi kwa njia ya visanduku (majedwali) hufafanua vijenzi vya sentensi katika ngazi mbalimbali.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 45 9/6/21 5:53 PM


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Njia ya uchanganuzi wa sentensi kwa kutumia mchoro uliokaa kama mti na matawi yake huitwa *njia ya matawi au ngoe.*

## Mkabala wa kimuundo

### Kazi ya 2.24

**Chunguza mchoro ufuatao, kisha jibu maswali yanayofuata.**




### Maswali

1. Mchoro huo unahusu nini?
2. Kuna uhusiano gani kati ya uchanganuzi wa sentensi na mchoro huo?
3. Mchoro huo unasaidiaje mchakato wa uchanganuzi wa sentensi?




Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 46 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


## Njia ya matawi

Ifuatayo ni mifano ya sentensi zilizochanganuliwa kwa njia ya matawi.

(i) Baba anafuga nyuki wadogo.




(ii) Walimu na wanafunzi walikuwa wanacheza mpira wa miguu.








Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 47 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) Sisi tunataka kuendesha gari la mjomba lakini Maswi anapalilia viazi vya babu yake.





(iv) Nyoka aliyekatwa mkia ameingia shimoni.



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(v) Mtoto alifurahi alipopewa zawadi.




## Zoezi la 2.9

Kwa kutumia njia ya matawi, changanua sentensi zifuatazo:

(a) Haya ni maelezo ya mtu mwingine.
(b) Sikukusudia hayo bali ilikuwa bahati mbaya.
(c) Mtoto aliyegongwa na gari amelazwa hospitalini.
(d) Mwanafunzi mwema hakufurahi wenzake walipogombana darasani.
(e) Walimu na wanafunzi wanaimba wimbo wa Taifa.

FOR ONLINE USE ONLY

### Njia ya majedwali

Ifuatayo ni mifano ya uchanganuzi wa sentensi kwa njia ya majedwali.

(i) Jambazi aliyetoroka jana amekamatwa leo mchana.

<table>
<tr><th colspan="7">S. Changamani</th></tr>
<tr><td colspan="4">KN</td><td colspan="3">KT</td></tr>
<tr><td rowspan="4">N</td><td colspan="3">S</td><td rowspan="4">T</td><td colspan="2">KE</td></tr>
<tr><td>KN</td><td colspan="2">KT</td><td rowspan="3">E</td><td rowspan="3">E</td></tr>
<tr><td rowspan="2">N</td><td rowspan="2">T</td><td>KE</td></tr>
<tr><td>E</td></tr>
<tr><td>Jambazi</td><td>Ø</td><td>aliyetoroka</td><td>jana</td><td>amekamatwa</td><td>leo</td><td>mchana</td></tr>
</table>



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 49 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ii) Wanafunzi wa kidato cha kwanza wanacheza mpira wakati wanafunzi wengine wanaimba nyimbo.

<table>
<tr><td colspan="12">S. Ambatani</td></tr>
<tr><td colspan="7">S1</td><td rowspan="6">U</td><td colspan="4">S2</td></tr>
<tr><td colspan="5">KN</td><td colspan="2">KT</td><td colspan="2">KN</td><td colspan="2">KT</td></tr>
<tr><td rowspan="4">N</td><td colspan="4">KH</td><td rowspan="4">T</td><td>KN</td><td rowspan="4">N</td><td>KV</td><td rowspan="4">T</td><td>KN</td></tr>
<tr><td rowspan="3">H</td><td colspan="3">KN</td><td rowspan="3">N</td><td rowspan="3">V</td><td rowspan="3">N</td></tr>
<tr><td rowspan="2">N</td><td colspan="2">KH</td></tr>
<tr><td>H</td><td>N</td></tr>
<tr><td>Wanafunzi</td><td>wa</td><td>kidato</td><td>cha</td><td>kwanza</td><td>wanacheza</td><td>mpira</td><td>wakati</td><td>wanafunzi</td><td>wengine</td><td>wanaimba</td><td>nyimbo</td></tr>
</table>

**Zoezi la 2.10**

Kwa kutumia njia ya jedwali (visanduku), changanua sentensi zifuatazo:

(a) Kuku mweupe amechinjwa asubuhi.

(b) Tunu ni mwanafunzi hodari katika mpira wa pete.

(c) Tutakwenda baharini kesho jioni.

(d) Kisu kilichopotea kimeonekana jikoni.

(e) Gari lilianguka lilipoingia bondeni.

(f) Mimi nitaenda shambani ingawa mvua imenyesha.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zingatia

Uchanganuzi wa sentensi kwa mkabala wa kimuundo hufuata hatua zifuatazo:

(a) Kubaini au kutambua aina ya sentensi inayochanganuliwa, yaani sentensi sahili, sentensi ambatani na changamani;

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Kubaini sehemu kuu za sentensi, mfano: kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT);

(c) Kutenga sentensi katika virai, mfano: kirai nomino (KN), kirai kitenzi (KT), kirai kielezi (KE), kirai kihusishi (KH) na kirai kivumishi (KV);

(d) Kubaini na kuandika aina za maneno yanayoijenga sentensi hiyo, mfano: nomino (N), kiwakilishi (W), kivumishi (V), kielezi (E), kihusishi (H), kihisishi (I), kitenzi (T) na kiunganishi (U);

(e) Kuiandika sentensi yote.

**Kazi ya 2.25**

Katika vikundi vya wanafunzi wanne au watano, jadili taaluma ya uchanganuzi wa sentensi inavyoweza kutumika katika maisha ya kila siku.

**Zoezi la marudio la 2**

1. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

(i) Chagizo katika uchanganuzi wa sentensi hutumika katika mkabala wa_____
- (a) kimuundo
- (b) kimapokeo
- (c) kisiasa
- (d) kiupatanishi
- (e) kisintaksia

(ii) Uchanganuzi wa sentensi kwa mkabala wa kimuundo hujikita katika_____
- (a) kiima na kiarifu
- (b) kirai nomino na kivumishi
- (c) kirai kitenzi na kishazi tegemezi kielezi
- (d) kirai nomino na kirai kitenzi
- (e) kiima na prediketa

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 51 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) Zifuatazo ni sifa za tungo isipokuwa ______
  (a) huweza kuwa na kitenzi
  (b) hufanikisha mawasiliano
  (c) huweza kuwa na kirai nomino na kirai kitenzi
  (d) huweza kuwa na neno moja au zaidi
  (e) huonesha ukanushi kila inapotumika

(iv) Obogo alifurahi alipopata maswali yote ya Kiswahili. Neno lililopigiwa mstari ni ______
  (a) nomino
  (b) kielezi
  (c) kitenzi
  (d) kishazi tegemezi kielezi
  (e) kishazi tegemezi kivumishi

(v) Kimapokeo, nomino inayojitokeza upande wa kiarifu inaitwa ______
  (a) kiima
  (b) chagizo
  (c) shamirisho
  (d) kiarifu
  (e) prediketa

2. Bainisha vishazi tegemezi katika tungo zifuatazo:
  (i) Mwanafunzi wetu aliyepewa zawadi ameondoka.
  (ii) Mbuzi aliyenunuliwa jana asubuhi amechinjwa.
  (iii) Mzee aliyefukuza kondoo wake amerudi leo.
  (iv) Uwanja uliojengwa Lindi umekamilika.
  (v) Katapila lililobomoa nyumba yetu limeharibika.
  (vi) Mkulima ambaye alifika hapa jana ni mchapakazi.
  (vii) Pesa zilizopotea zimepatikana.
  (viii) Msichana ambaye alituimbia jana jioni atakuja kesho.
  (ix) Kiti kilichovunjika kimetengenezwa.
  (x) Inashangaza sana jinsi alivyotoroka jela.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Eleza dhana ya tungo.
4. Tofautisha kirai na kishazi.
5. Tunga sentensi 5 zenye virai na 5 zenye vishazi.
6. Fafanua muundo wa kirai nomino.
7. Bainisha tofauti iliyopo kati ya KN na KT.
8. Eleza maana ya sentensi.
9. Orodhesha aina za sentensi.
10. Changanua sentensi zifuatazo kwa njia ya jedwali
    (a) Mkulima hodari amevuna mazao mengi.
    (b) Bibi anapika na babu anasikiliza redio.
11. Changanua sentensi zifuatazo kwa njia ya matawi
    (a) Mwalimu wa Kiswahili alimwadhibu mwanafunzi mtoro darasani.
    (b) Mbuzi aliyevunjika mguu amepona.
12. Oanisha maelezo ya kifungu A na maneno katika kifungu B.

| Kifungu A | Kifungu B |
|---|---|
| i. Sehemu ya kiarifu inayokaliwa na nomino ______ | A. kirai |
| | B. kishazi tegemezi |
| ii. Neno au mpangilio wa maneno wenye neno kuu moja ______ | C. kirai kivumishi |
| | D. shamirisho |
| iii. Sehemu ya kiarifu inayokaliwa na kielezi ______ | E. kirai kitenzi |
| | F. kishazi tegemezi kielezi |
| iv. Huundwa na vitenzi vyenye viambishi vya o-rejeshi ______ | G. chagizo |
| | H. kirai kielezi |
| v. "Mwenye duka" ni muundo wa ______ | I. kirai nomino |
| | J. ambatani |
| vi. "Atarudi kesho" ni muundo wa _____ | K. prediketa |
| vii. "Mwanafunzi ambaye hakufika jana, asimame" ni mfano wa sentensi ______ | L. kiarifu |
| | M. changamani |

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 53 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tatu

## Maendeleo ya Kiswahili

### Utangulizi

*Lugha yoyote ile ina historia na asili yake. Uhai wa lugha fulani hutokana na kuwapo kwa watu wanaoitumia lugha hiyo. Katika sura hii, utajifunza asili ya Kiswahili kwa kuzingatia ushahidi wa kimuundo na kimsamiati wa Kiswahili na lugha zingine za Kibantu. Vilevile, utajifunza chimbuko la Kiswahili. Umahiri utakaoujenga, utakuwezesha kubaini namna lugha zinavyoathiriana. Pia, utakuwezesha kufanya utafiti kuhusu asili za lugha zingine za Kibantu na kujiongezea maarifa.*

FOR ONLINE USE ONLY

### Kazi ya 3.1

**Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Katika karne ya 10 na 12 BK, watu wawili wasiofahamiana walikutana. Watu hawa walikuwa Juma na Ashura. Juma alikuwa anazungumza lugha yake ambayo haikufahamika kwa Ashura. Hali kadhalika, Ashura naye alikuwa na lugha yake isiyofahamika kwa Juma. Juma alitoka mbali na kufika nyumbani kwa Ashura. Lengo la Juma lilikuwa kufanya biashara, kueneza utamaduni wake na kutawala. Pepo za Kaskazi na Kusi zilimsaidia Juma kufika kwa Ashura. Watu hawa walikutana maeneo ya pwani na sehemu zingine za visiwani zilizo katika Pwani ya Afrika Mashariki. Kabla ya makutano hayo, Ashura na wenyeji wengine walikuwa wakizungumza lugha zao ambazo hazikufahamika miongoni mwao. Vipo visasili tu ambavyo vinajaribu kueleza hali ilivyokuwa.

Kuna visasili kadhaa vinavyotaja baadhi ya maeneo ambayo lugha ya Ashura ilitamalaki wakati wa makutano na Juma. Maeneo hayo ni: Lamu, Visiwa vya Ngozi na Kaskazini mwa Kenya. Aidha, kuna visasili vingine vinataja maeneo ya kushangaza kidogo ambayo kwa wakati huu ukifuatilia, unashindwa



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 54 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kugundua ni wapi hasa, kwa mfano Shungwaya. Kisasili chenye kuvutia zaidi ni kile kinachotaja lugha ya Ashura kwamba, ilielekea kutamalaki katika jamii pana zaidi hadi nje ya jamii ya Ashura. Visasili hivi vina maana kuwa Juma na kundi lake wakati wanakuja waliikuta lugha ya Ashura ikiwa tayari inatumika. Asikwambie mtu! Binadamu bwana! hawana ugeni wala wenyeji; wakikaa pamoja kwa muda, huanza kujenga uhusiano na hatimaye ndoa. Juma na Ashura walioana, hatimaye walizaa watoto kisha wakapata wajukuu. Watoto wao walianza kuzungumza lugha iliyowaunganisha wazazi wao, ambayo ilikuwa mchanganyiko wa lugha ya Ashura na ya Juma. Aidha, shughuli za ndoa, biashara na mahubiri ya dini ya Kiislamu vilivyofanywa na Juma vilisababisha athari kwenye lugha. Yaani, kulitokea mabadilishano ya vitu kutoka upande wa Ashura kwenda wa Juma na kutoka upande wa Juma kwenda wa Ashura. Lugha ya Ashura ambayo awali ilikuwa haina mchanganyiko wowote, ilianza kupokea baadhi ya maneno na miundo kutoka kwenye lugha ya Juma. Vilevile, lugha ya akina Ashura ambayo ilikuwa inazungumzwa katika kijiji chao tu, ilitamalaki maeneo mbalimbali kutokana na shughuli za kibiashara na kidini zilizofanywa na Juma.

## Maswali

1. Eleza mahali walipotokea Juma na Ashura katika kifungu cha habari ulichokisoma.
2. Bainisha maeneo yaliyokuwa kitovu cha makutano kati ya Juma na Ashura.
3. Kutokana na kifungu cha habari ulichokisoma, eleza athari za kijamii zilizotokea kutokana na makutano hayo.
4. Bainisha mazingira ambayo lugha ya wenyeji ilikuwa inazungumzwa kabla ya Ashura kukutana na Juma.
5. Fafanua mambo yaliyochangia kuenea kwa lugha ya akina Ashura kwenda katika vijiji vingine.
6. Eleza sifa za lugha ya Ashura baada ya kukutana na Juma.

### Asili ya Kiswahili

Kiswahili kama lugha nyingine yoyote kina asili yake. Neno asili lina maana ya chanzo au mwanzo wa kitu au namna kitu kilivyoanza. Kuna mitazamo mikuu minne kuhusu asili ya Kiswahili: Kiswahili ni Kiarabu, Pijini au Krioli, lugha chotara na Kibantu. Mitazamo hiyo imefafanuliwa kama ifuatavyo:



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 55 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kiswahili ni Kiarabu

Mtazamo huu unadai kuwa, neno lenyewe "Kiswahili" limetokana na neno la Kiarabu "sahil" umoja na "sawahil" wingi, lenye maana ya pwani. Pia, Kiswahili kina msamiati mwingi wa Kiarabu, mfano: *salamu, shukrani*, *ishirini* na mengineyo. Baadhi ya maneno yaliyotumiwa katika shughuli za kibiashara ni: *bei, ushuru, shukrani na laki*. Vilevile, kuna maneno yanayohusu sehemu ya kitu au vitu kutoka lugha ya Kiarabu. Mfano: *theluthi, thumni* na *sudusi*. Kuna msamiati mwingine wa hesabu kama vile: *ishirini, thelathini, arobaini, hamsini* ambao ulitokana na lugha ya Kiarabu.

Aidha, dini ya Kiislamu ambayo ilianzia Pwani ya Afrika Mashariki ni ushahidi kwani ilitumia Kiswahili. Hivyo, kwa kuwa wenyeji wa Pwani ni Waislamu na uislamu ulileta na Waarabu, basi hata Kiswahili kililetwa na Waarabu.

Hata hivyo, wanaisimu wanadai kuwa sababu za kukihusisha Kiswahili na Kiarabu hazijitoshelezi, kwani lugha yoyote inaweza kukopa maneno kutoka lugha zingine. Hivyo, Kiswahili nacho kama ilivyo lugha nyingine kimekopa baadhi ya maneno kutoka lugha zingine, mfano: *Kihindi, Kiajemi, Kireno, Kijerumani, Kifaransa,* na *Kiingereza*. Aidha, lugha yoyote inaweza kuathiri na kuathiriwa na lugha nyingine. Hivyo, Kiswahili nacho kimeathiriwa na lugha ya Kiarabu pamoja na lugha zingine kwa sababu ya mwingiliano wa shughuli za kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa.

Udhaifu uliopo katika mtazamo huu ni kuwa, maneno mengi ya mkopo kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine si sababu ya asili ya lugha hiyo. Pia, asili ya lugha haitokani na sababu ya imani ya dini. Dini ya Kiislamu, haiwezi kuwa asili ya Kiswahili, kwani Kiarabu si uislamu.

## Kiswahili ni Pijini au Krioli


Mtazamo huu unadai kuwa Kiswahili ni Pijini. Pijini ilitokana na makundi mawili ya watu waliotumia lugha tofauti, kukutana na kushirikiana katika shughuli za kijamii na kiuchumi. Kwa kuwa watu hao hawakuwa na lugha moja ya mawasiliano katika shughuli zao, waliamua kuunda lugha moja iliyokidhi mawasiliano katika kipindi hicho. Aidha, mtazamo huu unadai kuwa Kiswahili ni lugha iliyozaliwa kutokana na mwingiliano wa Waarabu na Waafrika katika shughuli zao mbalimbali. Mwingiliano huu ulisababisha mchanganyiko wa msamiati wa pande zote mbili za watumiaji wa lugha. Hatimaye, kuzaliwa kwa lugha ya kati iliyoitwa Pijini. Tazama kielelezo kifuatacho:



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 56 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Msamiati wa Kibantu




Msamiati wa Kiarabu

Pijini

**Kielelezo Namba 3.1:** *Hali ya kutokea kwa Pijini*

Krioli huzaliwa kutokana na Pijini. Watu wanaozungumza Pijini, wanapooana na kuzaa watoto, watoto hao huzungumza lugha ambayo si ya mama wala ya baba, bali huzungumza lugha ya kati inayotokana na lugha mbili tofauti za wazazi wao ambayo ni Krioli. Hivyo, watoto waliozaliwa hawakuzungumza lugha ya Kiarabu wala lugha za Kibantu, bali walizungumza mchanganyiko wa lugha hizo mbili yaani Krioli. Wataalamu wa mtazamo huu, wanadai kuwa Kiswahili ni Pijini au Krioli iliyotokana na mwingiliano wa jamii mbili yaani jamii ya Waarabu na Waafrika.

Udhaifu wa mtazamo huu, haujaonesha wazi kuwa Pijini iliyozuka katika mwingiliano huo kama ilikuwa na muundo rasmi kabla ya kuwa Krioli. Pia, hakuna msamiati wowote wa Pijini uliothibitisha kuwapo kwa lugha hiyo. Hivyo, ushahidi huu hauna mashiko kuthibitisha asili ya Kiswahili, kwani hadi sasa watoto hao siyo wengi hadi kuunda lugha ikaweza kutamalaki.

FOR ONLINE USE ONLY

### Zoezi la 3.1

1. Fafanua dhana ya Pijini.
2. Unaelewa nini kuhusu Krioli?
3. Kuna uhusiano gani kati ya Krioli na Pijini?

### Kazi ya 3.2

Tunga igizo lenye kuhusisha wahusika wenye lugha tofauti katika shughuli za kibiashara, kisha liigizwe darasani.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kiswahili ni lugha chotara

Lugha chotara huzaliwa kutokana na mwingiliano wa watu wenye asili tofauti katika biashara au shughuli za kijamii. Mtazamo huu unadai kuwa Waarabu walipofika Pwani ya Afrika Mashariki kwa shughuli za kibiashara walioa wanawake wa Kiafrika na kuzaa nao. Watoto hao walikuwa chotara wa Kiarabu na Kiafrika. Hawakuwa na lugha moja waliyoitumia kuwasiliana bali walikuwa na lugha mchanganyiko. Lugha hiyo haikuwa Kiarabu kutoka upande wa baba wala Kiafrika kutoka upande wa mama. Hivyo, mwingiliano huo ulizaa lugha ya Kiswahili.

Hata hivyo, mtazamo huu haujaeleza wazi kuwa ni lugha zipi za Kiafrika zilizochanganyika na Kiarabu na kuzaa Kiswahili. Pia, haujasema kuhusu wenyeji walioolewa na Waarabu, walikuwa Wabantu, Wanailoti au Wakushi.

**Zoezi la 3.2**

1. Fasili dhana ya uchotara.
2. Makutano ya Waarabu na Waafrika yalikuwa wapi na yalitokana na nini?
3. Je, mtazamo unaodai Kiswahili ni lugha chotara una mashiko? Kwa nini?

FOR ONLINE USE ONLY

### Kiswahili ni Kibantu

Watafiti wa lugha za Kiafrika wamekitambulisha Kiswahili kuwa mojawapo ya lugha za Kibantu. Kwa msingi huo, ufafanuzi kuhusu asili na maendeleo ya Kiswahili hauna budi kujadiliwa kwa kuzingatia muundo wa Kiswahili na Kibantu. Neno "Bantu" lina maana ya watu wanaoishi Kusini mwa jangwa la Sahara. Lugha za watu hao katika eneo hilo huitwa lugha za Kibantu. Nchi zenye wazungumzaji wa lugha za Kibantu kusini mwa jangwa la Sahara ni: Kongo, Kameruni, Tanzania, Uganda, Kenya, Burundi, Rwanda, Malawi, Zambia na Afrika Kusini. Kiswahili ni lugha mojawapo ya lugha za Kibantu kwani ina ufanano na lugha nyingi zinazozungumzwa kusini mwa jangwa la Sahara.

Upo ushahidi wa kimuundo na kimsamiati (kiisimu) unaojikita katika misingi ya kisayansi ya lugha inayohusu orodha ya msamiati, vipengele vya kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia. Kwa kuzingatia misingi ya sayansi ya lugha, mtazamo wa kiisimu unathibitisha kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 58 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Msamiati wa msingi wa Kiswahili una mfanano na ule wa lugha zingine za Kibantu. Ufanano huo upo katika mzizi wa maneno ingawa kuna tofauti ndogondogo katika matamshi na viambishi. Maneno mengi ya Kiswahili yanafanana kimuundo na maneno kutoka lugha zingine za Kibantu.

**Kazi ya 3.3**

Kusanya maneno kumi kutoka katika lugha nne za Kibantu, kisha yapange maneno hayo katika umoja na wingi huku ukihusianisha na Kiswahili.

**Kazi ya 3.4**

Kusanya maneno kumi ya lugha nne za Kibantu, kisha onesha muundo wa silabi kwa kuzingatia KI, KKI na I huku ukilinganisha na yale ya Kiswahili.

## Zingatia

Muundo wa maneno ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu una mfanano katika msamiati, maumbo ya maneno, muundo wa silabi na miundo ya sentensi.

Mfanano wa msamiati

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kiswahili** | watoto (wana) | mtu | maji | jicho |
| **Kingoni** | *vana* | *mundu* | *manji* | *lihu* |
| **Kizigua** | *wana* | *mntu* | *mazi* | *ziso* |
| **Kihaya** | *abana* | *omuntu* | *amaizi* | *eliisho* |
| **Kikurya** | *abhana* | *omonto* | *amanche* | *iliso* |

Upo mfanano katika maumbo ya majina ya umoja na wingi kama ifuatavyo:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kiswahili** | mtu | **m**-tu | watu | **wa**-tu |
| **Kikurya** | *(o)monto* | ***mo***-*nto* | *(a)bhanto* | ***bha***-*nto* |
| **Kinyaturu** | *muntu* | ***mu***-*ntu* | *antu* | ***ba***-*ntu* |
| **Kirombo** | *mundu* | ***mu***-*ndu* | *fandu* | ***fa***-*ndu* |



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 59 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Muundo wa silabi

Silabi za maneno ya Kiswahili zina ufanano mkubwa na lugha za Kibantu katika muundo na matamshi. Kwa mfano, muundo wa konsonanti na irabu (KI) katika maneno yafuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| **Kiswahili** | mama | $ma$$ma$ |
| **Kisukuma** | *mayu* | $*ma*$$*yu*$ |
| **Kiha** | *mawe* | $*ma*$$*we*$ |

Muundo mwingine ni ule wa konsonanti, konsonanti na irabu (KKI) mathalani, katika muundo wa silabi.

| | | |
|---|---|---|
| **Kiswahili** | njoo | $njo$$o$ |
| **Kipogoro** | *gwiziti* | $*gwi*$$*zi*$$*ti*$ |
| **Kinyaturu** | *njuu* | $*nju*$$*u*$ |
| **Kingoni** | *bwelayi* | $*bwe*$$*la*$$*yi*$ |

**Kazi ya 3.5**

Kusanya vitenzi kumi kutoka lugha tano za Kibantu, kisha bainisha mzizi wa kitenzi, kiambishi awali na kiambishi tamati ukilinganisha na Kiswahili.

**Kazi ya 3.6**

Zungumza na watu wa lugha tano za Kibantu, kisha andika sentensi tano kwa kila lugha na uzipange katika umoja na wingi kwa kuzihusianisha na Kiswahili.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zingatia

Kuna ufanano wa muundo wa Kiswahili na lugha zingine za Kibantu kwenye mzizi wa vitenzi, viambishi awali, viambishi tamati na mnyumbuliko wa vitenzi, mfano, katika kitenzi *anapiga*.

| | |
|---|---|
| **Kiswahili** | a-na-pig-a |
| **Kipare** | *e-bigh-a* |
| **Kinyiramba** | *u-ko-a* |



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 60 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Aidha, ushahidi wa kiisimu, unaonesha kuwa Kiswahili na lugha zingine za Kibantu zina tabia ya kupokea viambishi vya mnyumbuliko baada ya mzizi wa kitenzi, mfano, *kucheka*.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Kiswahili** | kucheka | kuchek-esh-a | kuchek-ele-a |
| **Kingoni** | *kuheka* | *kuhek-es-a* | *kuheke-lel-a* |
| **Kikaguru** | *kuseka* | *kusek-esh-a* | *kuseke-lel-a* |

Muundo wa sentensi za Kiswahili, una mfanano na miundo ya sentensi za lugha nyingine za Kibantu. Baadhi ya sentensi hizi huweza kuwa na muundo wa N+V+T.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Kiswahili** | watoto | wawili | wanaoga |
| **Kizigua** | *wana* | *waidi* | *wahaka* |
| **Kichaga** | *wana* | *wawi* | *wakesamba* |

Vilevile, kuna ufanano wa sentensi katika muundo wa upatanisho wa kisarufi wa maneno ya Kiswahili na upatanisho wa kisarufi katika maneno ya lugha zingine za Kibantu.

**Kiswahili:** Msichana mzuri amepika chakula.
Wasichana wazuri wamepika vyakula.

**Kipare:** *Mbora wedi adika kijo.*
*Vabora vedi vadika vijo.*

**Kihehe:** *Umuhinza umunofu atelike ichakulya.*
*Avahinza avanofu vatelike ifyakulya.*

FOR ONLINE USE ONLY

**Kazi ya 3.7**

1. Katika vikundi, fanya utafiti wa miundo na msamiati mbalimbali wa Kiswahili na kuhusianisha na lugha nyingine za Kibantu.
2. Chunguza lugha tano za Kibantu, kisha onesha mfanano wa maumbo ya vitenzi ukihusianisha na Kiswahili.
3. Kusanya maneno kumi ya lugha mbalimbali za kibantu, kisha bainisha miundo ya silabi katika maneno hayo, ukihusianisha na miundo ya silabi za Kiswahili.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 61 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 3.3**

1. Kiswahili ni Kibantu kwa asili yake. Fafanua kwa kutumia ushahidi wa kimsamiati na kimuundo.
2. Fafanua tofauti iliyopo kati ya Pijini na Krioli.
3. Asili ya Kiswahili ni Kiarabu. Eleza dai hili kwa kutumia kigezo cha msamiati.
4. Lugha ya Kiswahili ilikuwa inazungumzwa hata kabla ya ujio wa wageni. Thibitisha usemi huu.

## Chimbuko la Kiswahili


Chimbuko la Kiswahili ni mahali au sehemu ambapo Kiswahili kinafikiriwa ndipo kilipoanzia. Kuna mitazamo mitano inayoeleza chimbuko la Kiswahili. Mtazamo wa kwanza ni ule unaodai kuwa, Kiswahili kilianzia katika Visiwa vya Ngozi (Ngozini) (Chiraghdin, 1971; 1973 & 1974). Mtazamo wa pili unasema kwamba, Kiswahili kilianzia Lamu, (Archipelago, Nurse na Spear, 1985). Mtazamo wa tatu, unaonesha kuwa Kiswahili kilianzia Shungwaya Kuu (James der ver Allen, 1993). Nne, ni mtazamo unaosema kuwa, Kiswahili kilianzia Kaskazini Mashariki mwa Kenya (Mazrui na Shariff, 1994). Mtazamo wa tano unaeleza kuwa, Kiswahili kilianzia Pwani ya Afrika Mashariki (Massamba, 2002; 2007, 2017). Hadi kufikia sasa, mtazamo unaoelekea kukubalika na wanaisimu wengi, ni ule wa tano, unaoeleza kuwa Kiswahili kilianzia Pwani ya Afrika Mashariki.

Inadhaniwa kuwa, Wabantu waliingia nyanda za kati za Afrika ya Mashariki mnamo karne ya 1 na ya 2 BK, wakitokea eneo lililo Kusini Mashariki mwa Zaire, sehemu za Katanga. Walipokuja Afrika Mashariki, walifanya maskani yao katika mabonde ya Kaskazini mwa mto Tana ambapo walianzisha makazi yao Shupate na Shungwaya. Mnamo miaka ya 500 BK, makazi ya mto Tana yalivamiwa na kushambuliwa na kabila la Wagala. Uvamizi huu uliwafanya wenyeji wake kukimbia na kusambaa katika sehemu mbalimbali za Pwani ya Bahari ya Hindi. Huko walianzisha tena makazi yao katika sehemu mbalimbali kuanzia sehemu za Kusini mwa Somalia kwa upande wa Kaskazini mpaka sehemu za mto Pangani. Wengine walivuka bahari ya Hindi na kuishi katika Visiwa vya Pemba, Unguja na Komoro. Kote walikokwenda Wabantu hao waliendelea

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kuzungumza lugha zao zenye asili ya Kibantu. Kielelezo kifuatacho kinaonesha jinsi Wabantu walivyosambaa.




**Kielelezo Namba 3.2:** *Ramani ya Afrika kuonesha msambao wa Wabantu*

## Zingatia

Lahaja ni tofauti ndogondogo katika matamshi, maumbo na matumizi ya maneno katika maeneo mbalimbali ya lugha yenye asili moja. Tofauti hizo haziwezi kukwamisha maelewano miongoni mwa watumiaji wa lahaja hizo. Kiswahili kina lahaja mbalimbali zilizotokana na: kuhamahama kwa watu kutoka eneo moja kwenda

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

eneo lingine; umbali wa kijiografia wa jamii moja na nyingine; mwingiliano wa kijamii katika ndoa au shughuli nyingine, mfano: elimu, dini mbalimbali; tofauti za uwezo kiuchumi wa jamii moja na nyingine na kupita kwa wakati, zimechangia kutokea kwa lahaja mbalimbali za Kiswahili.

**Jedwali la 3.1:** Baadhi ya lahaja za Kiswahili na maeneo zinakozungumzwa

| Na. | Lahaja | Eneo |
|---|---|---|
| 1. | Kimiini (Mwiini, Barawa) | Kusini mwa Somalia |
| 2. | Kitikuu (Bajuni, Gunya) | Mpakani mwa Kenya na Somalia |
| 3. | Kisiu | Kisiwa cha Pate |
| 4. | Kipate | Kisiwa cha Pate Kusini-Magharibi |
| 5. | Kiamu | Kisiwa cha Lamu-Kaskazini |
| 6. | Kishela | Kisiwa cha Lamu |
| 7. | Kimatondoni | Kisiwa cha Lamu-Kusini |
| 8. | Kimvita | Mombasa na Kilifi |
| 9. | Kijomvu, Kingare | Mombasa |
| 10. | Chifundi (Kishirazi) | Mombasa na Rasi ya Funzi |
| 11. | Kivumba (Kivanga) | Mpakani mwa Kenya na Tanzania |
| 12. | Kimtang'ata (Kimrima) | Tanga |
| 13. | Kipemba | Kisiwa cha Pemba |
| 14. | Kiunguja (Kimji) | Unguja Mjini |
| 15. | Kitumbatu | Kisiwa cha Tumbatu |
| 16. | Kimakunduchi (Kikae) | Kusini Unguja |
| 17. | Kimgao | Pwani ya Kusini mwa Tanzania |
| 18. | Kimwani | Kaskazini mwa Msumbiji |
| 19. | Kingwana | Jimbo la Shaba la Zaire |

FOR ONLINE USE ONLY

**Kazi ya 3.8**

Chora ramani ya Afrika Mashariki, kisha onesha maeneo ya lahaja mbalimbali za Kiswahili.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 64 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Uchunguzi uliofanywa na baadhi ya wataalamu wa lugha kuhusu lugha na vipengele vingine vya utamaduni wa jamii mbalimbali za Wabantu, unaonesha kuwa chimbuko la watu wa jamii ya Wabantu ni huko Afrika ya Magharibi. Pia, uchunguzi huo unaonesha kwamba Wabantu walihama kutoka sehemu moja hadi nyingine, hatua kwa hatua, kwa kipindi kirefu. Matokeo yake waligawanyika. Kugawanyika huko, kulisababisha kuibuka kwa makundi mbalimbali ya Wabantu katika eneo hili. Tazama kielelezo kifuatacho cha baadhi ya lugha za Kibantu.




**Kielelezo Namba 3.3:** *Ramani ya Afrika kuonesha baadhi ya lugha za Kibantu*

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la marudio la 3

1. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

(i) Utofauti wa kimatamshi, kimaumbo na matumizi ya maneno ya lugha kuu moja katika maeneo mbalimbali huitwa ________
(a) lafudhi (b) lahaja (c) rejista
(d) msimu (e) toni

(ii) Hamsini, laki, kasri na fikiri ni miongoni mwa maneno yanayothibitisha asili ya Kiswahili ni ________
(a) Kiarabu (b) Krioli (c) Kibantu
(d) Pijini (e) Chotara

(iii) Kiisimu, upi ni mtazamo sahihi kuhusu chimbuko la Kiswahili?
(a) Ngozini (b) Shungwaya Kuu
(c) Kiarabu (e) Pijini na Krioli
(d) Pwani ya Afrika Mashariki

(iv) Lahaja ya Kishela inazungumzwa katika eneo lipi kati ya haya?
(a) Tanga (e) Kisiwa cha Lamu
(b) Mombasa (c) Unguja mjini
(d) Kisiwa cha Pemba

(v) Mtazamo unaoeleza kuwa Kiswahili kilianzia Lamu ulitolewa na nani?
(a) Massamba 2002; 2007, 2017
(b) Mazrui na Shariff 1994
(c) Archipelago, Nurse na Spear, 1985
(d) James der ver Allen, 1993
(e) Chiraghdin 1971; 1973 & 1974

(vi) Hoja za msingi za mtazamo wa Kiswahili asili yake ni Kiarabu umeegemea katika ________
(a) msamiati na dini ya Kiislamu
(b) msamiati
(c) msamiati na Waarabu kuoa Waafrika
(d) dini ya Kiislamu na biashara ya watumwa
(e) msamiati na lugha za Kibantu

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Oanisha maelezo ya kifungu A na maneno katika kifungu B.

| Kifungu A | Kifungu B |
|---|---|
| i. Lugha inayozungumzwa na watu wenye asili ya lugha mbili tofauti | A. Pijini |
| | B. Krioli |
| ii. Lugha ya Kibantu | C. Kiswahili |
| iii. Muunganiko wa lugha za makabila tofauti zenye kufanana | D. Kiarabu |
| | E. Kibantu |
| iv. Lugha iliyounganika kati ya Kiarabu na Kiswahili | F. Chotara |
| v. Lugha inayotokana na ukomavu wa Pijini | G. Lahaja |

3. Eleza namna lahaja za Pwani ya Afrika Mashariki zilivyochangia kustawi kwa Kiswahili.

4. Fafanua nadharia nne zinazoeleza asili ya Kiswahili.

5. Eleza mfanano wa kimsamiati na kimuundo wa Kiswahili na lugha zingine nne za Kibantu.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 67 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne

## Kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania wakati wa ukoloni

### Utangulizi

*Kuja kwa wakoloni wa Kiarabu na Kijerumani kulisaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania. Kiswahili kwa sasa, kimeenea na kinatumika maeneo mengi ulimwenguni. Katika sura hii, utajifunza jinsi Kiswahili kilivyokua na kuenea nchini Tanzania enzi za Waarabu na enzi za Wajerumani. Pia, utajifunza sababu zilizofanya Kiswahili kudumaa. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kubaini na kutumia mbinu mbalimbali zinazoweza kukuza Kiswahili nchini Tanzania na nje ya nchi.*

### Kazi ya 4.1

**Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Siku moja, Jurabu na wenzake walipokuwa kwenye matembezi, walijikuta wameingia katika kijiji kiitwacho Pazuri. Kijiji hicho kilikuwa kimezungukwa na maji. Watu wake waliishi kwa amani na utulivu chini ya utawala wa chifu wao aliyeitwa Suta. Kijiji hicho kilijaliwa kuwa na mazingira mazuri ya kuvutia. Chifu Suta aliwakaribisha bila hiana. Jurabu na wenzake walimkabidhi Chifu Suta vitu walivyokuwa navyo kama vile: shanga, mapambo na vito vya thamani. Chifu alifurahi sana, akaamua kuwaruhusu waishi hapo, kwa kuwa walikuwa watu wakarimu.

Kijiji cha Pazuri, kiliwavutia Jurabu na wenzake kutokana na mambo mengi mazuri yaliyopatikana humo. Waliishi kwa muda mrefu na wenyeji wa Kijiji cha Pazuri na mawasiliano yao yakawa mazuri kutokana na kuielewa vizuri lugha yao. Siku moja waliamua kurudi kwao, walipofika tu, waliwasimulia watu wa kwao kuhusu kijiji cha Pazuri na kwamba wanaweza kufanya nao

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 68 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

biashara. Wakaanzisha uhusiano na watu wa Pazuri. Uhusiano huo, uliwafanya wajue lugha ya wenyeji wao yaani lugha ya Kizuri. Jurabu na wenzake waliona fursa ya kuwafundisha wenyeji dini yao kwa kutumia lugha ya Kizuri. Bila kusita watu wa Pazuri wakaamini dini hiyo na kuifuata. Wakawa wanafanya mafundisho kwa lugha ya Kizuri kwani hata Jurabu na wenzake wakaielewa na kuitumia kila siku. Hatimaye, wakazoeana na wakaanza kuoana. Maisha yakasonga mbele.



Kutokana na udadisi waliokuwa nao, Jurabu na wenzake waliweza kuvuka mpaka kuelekea kijiji cha Ng'ambo na kubaini kuwa, kulikuwa na watu wengine walioelekeana na watu wa Pazuri. Pia, walipofika huko, walijenga uhusiano nao. Walibaini kuwa kuna malighafi nyingi za kutengenezea vito vya thamani, mapambo na shanga walizokuwa wakizileta. Aidha, walivutiwa kuona kuna watu wenye nguvu wanaoweza kuwasaidia kazi mbalimbali za huko kwao. Hivyo, waliamu kuanzisha biashara ya kuwanunua watu hao kupitia viongozi wao. Waliendelea kufanya biashara na watu wa Ng'ambo hadi mitaa ya ndani zaidi. Walijenga nyumba za ibada na vituo vya biashara. Kwa kufanya hivyo, walijikuta wamekuwa daraja la kuvutia lugha ya Kizuri. Walifanikiwa sana kwa kuwa walitumia lugha hiyo, iliyokuwa inashabihiana na lugha za watu wa Ng'ambo.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 69 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kila lenye mwanzo halikosi kuwa na mwisho, watu wa Pazuri walivamiwa na maadui waliokuja kuvuruga mipango yao. Nao, si wengine bali ni Taifa kubwa la Wajechu lililokuja rasmi kutawala kijiji cha Ng'ambo baada ya kusikia kuna mambo mazuri. Walipofika tu, wakawafukuza Jurabu na wenzake, kisha wakabaki wenyewe. Walianzisha mifumo yao ya utawala huku wakiwashirikisha watu wa Ng'ambo. Waliwapa madaraka Wanang'ambo, kwani ingekuwa vigumu wao kutawala kutokana na kutozijua vizuri lugha za watu wa Ng'ambo. Kwa wakati huo, watu wa Ng'ambo walikuwa wakiunganishwa na lugha ya Kizuri ambayo ilikuwa imekwishaenezwa na Jurabu na wenzake. Wajechu waliamua kuitumia kwa shingo upande kwa kuipa nafasi ya kutumika katika ngazi za chini za elimu ilihali lugha yao ilitumika katika ngazi za juu za elimu na maeneo mengine ya kiutawala.

Wajechu walianzisha mashamba makubwa kwa kuwa watu wa Ng'ambo walijaliwa kuwa na ardhi yenye rutuba na hali ya hewa safi. Wajechu hawakutaka shida, hivyo, waliamua kutumia kilichopo, ambapo watu wa Ng'ambo waligeuzwa vibarua katika mashamba hayo. Ili kufanikisha shughuli za mashamba, vibarua walichukuliwa kutoka mitaa ya pembezoni mwa kijiji cha Ng'ambo na kutumikishwa huko mashambani, mpaka walipomaliza kazi zao. Wakati wote walipokuwa huko mashambani, lugha iliyokuwa ikitumika ilikuwa Kizuri. Waliporejea kwao walijikuta wakitumia lugha ya Kizuri, kwani hata mawakala wa Wajechu walikuwa wakitumia lugha hiyo katika shughuli zao za utawala na mahakama. Lugha ya Kizuri ikapaa mithili ya moshi ufukao angani. Mbegu za Kizuri zikamea kila mahali kwani zilisambazwa na ndege wa masafa marefu.

## Maswali

1. Je, habari uliyoisoma inakufundisha nini?
2. Je, Jurabu na wenzake wanafananishwa na nani katika muktadha wa habari hii?
3. Unadhani nchi ya Pazuri inarejelea mahali gani?
4. Katika uhalisia wa leo, lugha ya Kizuri inarejelea lugha gani?
5. Eleza kwa kifupi mchango wa Wajechu katika uenezaji wa lugha ya Kizuri.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 70 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kukua na kuenea kwa Kiswahili

Hapo awali, Kiswahili kilikuwa kinazungumzwa na wenyeji waliokuwa wakiishi Pwani ya Bahari ya Hindi. Kufika kwa wakoloni wa Kiarabu na Kijerumani kulisababisha Kiswahili kukua na kuenea katika maeneo mengi. Ueneaji huo, ulichangiwa na shughuli mbalimbali zilizofanywa na wakoloni hao. Shughuli hizo ni: kueneza dini, elimu, biashara, utawala, harakati za kisiasa na shughuli za kiuchumi.

### Kukua na kuenea kwa Kiswahili enzi za Waarabu

Waarabu walikuwa wageni wa kwanza kufika Pwani ya Afrika Mashariki, hususani katika Visiwa vya Unguja na Pemba, ambako walikuta wenyeji wakizungumza lahaja mbalimbali za Kiswahili. Waarabu walipokuja mnamo karne ya 10BK, walizikuta lahaja hizo zikizungumzwa. Nazo zilikuwa zinafanana, waliziita "*Sawahil*" yaani "Iugha za Pwani." Neno "*Sawahil*" baadaye lilipata athari za kimatamshi na kutamkwa "*Swahili*", yaani lugha zote zilizokuwa zinazungumzwa katika mwambao wa Pwani ya Afrika Mashariki na visiwa vyake. Hatimaye jina la "*Kiswahili*" lilipatikana.

### Kukua kwa Kiswahili

Kukua kwa lugha ni kuongezeka kwa msamiati wa lugha fulani. Enzi za Waarabu Kiswahili kilikua kwa kasi, kwani kilipata msamiati mwingi wa Kiarabu uliotokana na shughuli zilizofanywa na Waarabu.

#### Biashara

Waarabu walipofika Pwani ya Afrika Mashariki, walifanya biashara mbalimbali. Maneno kama vile: *jahazi, ishirini, nahodha, rasi, hamsini, kodi, msumari, kata, furahi, rafiki, dhamiri* na mengineyo, yalitumika katika shughuli za kibiashara. Matumizi ya maneno hayo yaliongeza msamiati na kukifanya Kiswahili kikue kwa haraka.

FOR ONLINE USE ONLY

#### Dini

Kiswahili kilipata msamiati mpya wakati Waarabu walipokuwa wakifundisha elimu ya dini ya Kiislamu kwa Waswahili, ambapo walitafsiri Kurani kwa Kiswahili. Katika ufundishaji na ujifunzaji huo, Kiswahili kiliongeza msamiati kama vile: *alasiri, alfajiri, elimu, shukrani, kitabu,* na *hatari*. Aidha, maneno hayo yaliandikwa katika hati ya Kiarabu na kuingizwa katika msamiati wa Kiswahili.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Utawala**

Shughuli za utawala zilisaidia kukuza Kiswahili enzi za Waarabu. Katika kurahisisha shughuli zao, Waarabu walilazimika kutumia Kiswahili, maneno kama vile: *sultani, mwinyi, enzi, mtukufu, hakimu, sharia, Rais* na *waziri* yaliongezeka. Hivyo, ujio wa Waarabu ulikikuza Kiswahili kutokana na msamiati mpya ulioingizwa katika Kiswahili.

**Kazi ya 4.2**

Katika vikundi, jadili mambo mbalimbali yaliyosaidia kukua kwa Kiswahili enzi za Waarabu.

## Kuenea kwa Kiswahili

Kuenea kwa lugha hutokana na kuongezeka kwa watumiaji wa lugha hiyo katika maeneo mengine mapya. Kiswahili kilienea mahali pengi kutokana na shughuli mbalimbali, mfano: dini, biashara, elimu, utawala, na ndoa zilizofanywa na Waarabu.

**Dini**

Waarabu walipofika Pwani ya Afrika Mashariki, walileta dini yao ya Kiislamu, kwa lengo la kuhubiri na kueneza dini kwa watu. Walianzisha madrasa ili kueneza dini ya Kiislamu. Walilazimika kujifunza Kiswahili ili waweze kutafsiri Kurani kutoka Kiarabu kwenda Kiswahili. Hali hii, ilisababisha Kiswahili kupata wazungumzaji wengi. Pia, waliweza kusafiri kutoka Pwani mpaka bara, kueneza dini ya Kiislamu kwa watu, ambapo walipata Mashekhe na Maulamaa walioweza kuandika Kiswahili kwa kutumia alfabeti za Kiarabu. Kupitia dini ya Kiislamu, waumini walijifunza kaswida kwa Kiswahili na kufanya Kiswahili kuendelea kuenea zaidi.

**Utawala**

Sultani Seyyid Said alipotawala Zanzibar na eneo lote la Pwani ya Afrika Mashariki, alihimiza Kiswahili kitumike maeneo yote katika shughuli zote za kiutawala, pamoja na misafara ya biashara ya watumwa. Alichagua Maliwali na Maakida, ambao walikuwa Waswahili wa Pwani, akawapeleka Kilwa, Bagamoyo, Tanga, Kigoma, Mpwapwa na Ujiji. Lengo lilikuwa kuimarisha utawala wake. Katika maeneo hayo, viongozi hao walitumia Kiswahili. Hivyo, walikiwezesha Kiswahili kuenea na kuongezeka kwa idadi ya watumiaji katika maeneo tofautitofauti ya Afrika Mashariki.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 72 9/6/21 5:53 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Biashara**

Waarabu walipofika Pwani ya Afrika Mashariki, walikuja na bidhaa kutoka Uarabuni na kuanza kufanya biashara na Wabantu (Waswahili). Biashara hiyo ilifanyika kwa kubadilishana bidhaa, mfano, chumvi walibadilishana kwa dhahabu, shanga kwa watumwa au pembe za ndovu. Waarabu walifanya biashara kuanzia Pwani kuelekea bara ambako walipita katika miji ya Mpwapwa – Dodoma, Tabora hadi Ujiji. Misafara ya biashara ya watumwa, iliyoanzia Mzizima (Dar es Salaam) na Bagamoyo kuelekea Tabora na Kigoma, iliibua mawasiliano baina ya Waarabu na watu wa bara. Kwa njia hiyo, Kiswahili kilienea katika maeneo mbalimbali na kupata wazungumzaji wengi na kuibuka kwa msamiati mpya. Kiswahili kilikuwa lugha ya mawasiliano katika biashara hiyo.



**Ndoa**

Kuwapo kwa Waarabu Pwani ya Afrika Mashariki kwa muda mrefu, kuliwafanya Waarabu kuwa na uhusiano wa kindoa na wanawake wa Kiafrika. Kutokana na mwingiliano huo, walizaliwa watoto chotara na lugha yao ya mawasiliano katika shughuli zote za kijamii ilikuwa Kiswahili. Hivyo, mwingiliano huo ulichangia kwa kiasi kikubwa kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 73 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pamoja na Waarabu kueneza na kukuza Kiswahili enzi za utawala wao, kulikuwa na mambo yaliyochangia kukidumaza Kiswahili nchini Tanzania. Mambo hayo ni kama ifuatavyo:

(a) Enzi ya Waarabu, Kiswahili hakikuwekwa kwenye maandishi, yaani hakikutafsiriwa katika maandishi, mathlani, vitabu vya kidini, mfano: Kurani;

(b) Waarabu hawakujenga shule kwa ajili ya kutolea elimu kwa lugha ya Kiswahili;

(c) Hawakutilia mkazo ufundishaji wa somo la Kiswahili katika madrasa zao;

(d) Waarabu walidharau sana Kiswahili na kuiona kama lugha ya makabwela;

(e) Waarabu walieneza Kiswahili sehemu chache tu, walizofanyia shughuli zao.

**Kazi ya 4.3**

Katika vikundi, eleza jinsi Kiswahili kilivyoenea sehemu mbalimbali enzi za Waarabu.

**Zoezi la 4.1**

1. Eleza sababu za kukua kwa Kiswahili enzi za Waarabu nchini Tanzania.
2. Unafikiri kutokuja kwa wageni kama vile Waarabu kungefanya Kiswahili kisienee nchini? Eleza kwa mifano.
3. Eleza sababu zilizochangia kudumaza Kiswahili nchini enzi za Waarabu.

FOR ONLINE USE ONLY

## Kukua na kuenea kwa Kiswahili enzi za Wajerumani

**Kazi ya 4.4**

Katika vikundi, soma matini mbalimbali zinazohusu kukua na kuenea kwa Kiswahili enzi za Wajerumani, kisha eleza shughuli zilizochangia kukuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania.

### Kukua kwa Kiswahili

Wageni wengine waliofika Afrika Mashariki walikuwa Wajerumani (1884-1916). Wajerumani walipofika walikuta Kiswahili kinazungumzwa katika maeneo mengi ya Afrika Mashariki.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Ili kuweza kutawala na kuwasiliana kwa urahisi, walisisitiza matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya mawasiliano. Hivyo, ilisababisha Kiswahili kukua na kupata msamiati mpya. Vilevile, Wajerumani walitumia Kiswahili katika elimu, utawala, mahakama na shughuli za kilimo.

**Utawala**

Taarifa na ripoti zote za kiutawala ziliandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Kwa kufanya hivyo, maneno mbalimbali yaliweza kuingizwa katika Kiswahili. Mifano ya maneno hayo ni "jumbe" na "akida."

**Elimu**

Katika utawala wao, Wajerumani walijenga shule za msingi na sekondari hapa nchini. Lengo la kuanzisha shule lilikuwa kutoa elimu na kujinufaisha kwa rasilimali zilizopo nchini. Hivyo, Kiswahili kilikuwa lugha ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi kuanzia darasa la kwanza hadi la nne na sekondari kama somo. Katika muktadha huo, Kiswahili kilipata msamiati mpya, mfano: shule, mashine.

## Kuenea kwa Kiswahili

Kipindi cha utawala wa Wajerumani, Kiswahili kilienezwa kupitia shughuli mbalimbali hapa nchini. Shughuli hizo ni: utawala, elimu, dini, mahakama, na miradi mbalimbali ya kiuchumi kama vile: kilimo, ujenzi wa reli, barabara na viwanja vya ndege.

**Elimu**

Wajerumani walianzisha shule nyingi nchini Tanzania na kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia na kujifunzia. Kijerumani kilifundishwa kama somo. Kwa mfano, shule za msingi, sekondari na vyuo zilijengwa katika miji ya Tabora, Ujiji, Mpwapwa, Iringa, Bukoba, Mwanza na Moshi. Baadhi ya shule hizo ni: Sekondari ya Wavulana Tabora na Tanga. Walimu na wanafunzi walitumia Kiswahili katika ufundishaji na ujifunzaji kwa shule za msingi kwa darasa la kwanza hadi la nne.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 75 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Shughuli za kilimo**

Kilimo ni shughuli mojawapo ambayo Wajerumani waliifanya hapa nchini Tanzania. Walianzisha mashamba makubwa ya mazao ya biashara kama vile katani huko Tanga na kahawa mkoani Kilimanjaro na Kagera. Wafanyakazi wa mashamba hayo walitoka Tabora, Shinyanga, Mwanza, Ruvuma na Mara. Walilazimisha wafanyakazi hao kufanya kazi kwenye mashamba yao na lugha iliyotumika huko, ilikuwa Kiswahili. Kwa jinsi hiyo, hata baada ya kurudi kwao, wafanyakazi hao waliwashawishi ndugu zao kuzungumza Kiswahili na kusababisha Kiswahili kienee katika jamii zao.

**Mahakama**

Katika utawala wao, Wajerumani walifungua mahakama, hasa mahakama za mwanzo. Shughuli zote za kimahakama, zikiwamo kuendesha kesi na kutoa hukumu, zilitumia Kiswahili. Mahakama hizo zilijengwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini ambapo Kiswahili kilitumika katika shughuli zote, hivyo, kusababisha Kiswahili kienee katika maeneo mengi nchini.

**Utawala**


Kwa upande wa utawala, Wajerumani walipofika walikikuta Kiswahili kimekua. Hivyo, kabla ya kutawala waliamua kujifunza Kiswahili ili kuwarahisishia katika shughuli za utawala. Katika mchakato huo, walijenga ngome zao na kupeleka watu wanaojua Kiswahili katika maeneo mbalimbali nchini na huko Kiswahili kilitumika katika shughuli zote za utawala. Msisitizo ulitolewa kuwa, kupata ajira ni kwa wale tu wanaojua kuzungumza Kiswahili. Hivyo, watu walifanya jitihada za kujifunza Kiswahili. Kwa kufanya hivyo, Kiswahili kilienea katika maeneo mengi.

Pamoja na Wajerumani kusaidia katika kukuza na kueneza Kiswahili kupitia shughuli zao, kwa kiasi fulani, shughuli hizo zilichangia kukidumaza Kiswahili. Mambo yaliyochangia kudumaza Kiswahili enzi za Wajerumani nchini Tanzania ni pamoja na Kiswahili kutumika katika ngazi za chini za utumishi serikalini, kufundishia ngazi za chini za elimu kama vile shule za msingi, Wajerumani kutosanifisha Kiswahili wakati wa utawala wao, kutoanzisha chombo chochote cha kusaidia kukuza Kiswahili nchini, kutotilia mkazo kutunga vitabu kwa lengo la kukuza na kuendeleza Kiswahili. Tazama kielelezo kifuatacho cha misafara ya utawala wa Wajerumani nchini Tanzania.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 76 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




**Ufunguo**

| | | | |
|---|---|---|---|
| ---------- | Wajerumani | • | Miji |

**Kielelezo namba 4.1:** *Ramani ya Tanzania kuonesha misafara ya utawala wa Wajerumani*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kuwasili kwa Waarabu na wageni kutoka nchi nyingine, kulikuwa chanzo cha mwingiliano na utamaduni wa wenyeji wa Pwani na wageni hao. Baadhi ya matokeo ya mwingiliano huo, ni lugha za Pwani kupokea msamiati mwingi kutoka katika lugha za kigeni. Hata hivyo, uchunguzi unaonesha kuwa, lugha za kigeni hazikuleta mabadiliko katika maumbo ya maneno na miundo ya sentensi za Kiswahili. Tazama jedwali lenye baadhi ya maneno ambayo Kiswahili kiliyapokea kutoka lugha za kigeni:

**Jedwali la 4.1:** Baadhi ya maneno yaliyopokelewa kutoka lugha za kigeni

| Neno | Asili |
|---|---|
| Bendera, meza | Kireno |
| Duka | Kihindi |
| Bandari, pilau | Kiajemi |
| Chandarua | Kihindi |
| Shukurani, rasi, nahodha | Kiarabu |
| Chai | Kichina |
| Achali, bima | Kihindi |
| Shule, tai | Kijerumani |

FOR ONLINE USE ONLY

**Zoezi la 4.2**

1. Fafanua namna Kiswahili kilivyoenezwa nchini Tanzania enzi za utawala wa Kijerumani.
2. Eleza kwa mifano, jinsi Wajerumani walivyochangia kukuza Kiswahili.
3. Fafanua jinsi Wajerumani walivyochangia kudumaza Kiswahili nchini Tanzania.
4. Eleza jinsi Kiswahili kilivyoenea katika sehemu mbalimbali nchini Tanzania enzi za Wajerumani.
5. Fafanua namna Kiswahili kinavyoenezwa katika karne hii ya 21.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 78 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la marudio la 4

1. Jibu maswali yafuatayo:
   (i) Waarabu na Wajerumani pekee ndio waliosababisha lugha ya Kiswahili kukua kimsamiati. Jadili kauli hii kwa mifano.
   (ii) Inasemekana kuwa "Dini ya Kiislamu ina mchango mkubwa katika lugha ya Kiswahili inayozungumzwa kwa sasa nchini Tanzania." Jadili usemi huo.
   (iii) Kuja kwa wakoloni nchini Tanzania kulisaidiaje kukuza msamiati wa Kiswahili?
   (iv) Wajerumani walikienezaje Kiswahili katika maeneo mbalimbali nchini Tanzania?

2. Jaza nafasi zilizoachwa wazi.
   (i) Shughuli tatu ambazo Wajerumani walizifanya kueneza Kiswahili nchini Tanzania ni __________, __________ na __________.
   (ii) Dini iliyochangia kuenea kwa Kiswahili nchini wakati wa utawala wa Waarabu ni __________.
   (iii) Utawala wa __________ ulichangia kwa sehemu kubwa kukuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania kabla ya uhuru.
   (iv) Msamiati wa Kiswahili uliotokana na Kijerumani ni kama vile __________, __________, na __________.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 79 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

## Uhakiki wa kazi za fasihi andishi

### Utangulizi

*Kazi yoyote ya fasihi sharti ihakikiwe kabla ya kuifikia jamii au hadhira iliyokusudiwa. Katika sura hii, utajifunza dhana, sifa na dhima za uhakiki wa kazi za fasihi andishi ambazo ni riwaya, tamthiliya na ushairi. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kupata ujuzi na maarifa ya kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi andishi.*

### Kazi ya 5.1

**Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**






Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 80 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Unafikiri picha hiyo inahusu nini?
2. Kwa mujibu wa picha hiyo, fafanua hadhira unayoiona?
3. Mtu anayechunguza kazi za fasihi na kuzitolea uamuzi huitwa nani?
4. Kuna uhusiano gani kati ya mwandishi wa kazi ya fasihi na jamii?

### Kazi ya 5.2

**Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Wakati wa utoto wake, Kandi alikuwa binti mtundu sana. Baba yake alimpenda kwa vile alikuwa mchangamfu na mcheshi. Familia yao ilikuwa na furaha walipomwona binti yao kipenzi akiwa na siha njema. Alipokuwa Kidato cha Tatu, alijiunga na kikundi cha maigizo hapo shuleni kwao. Pia, alikuwa manju wa nyimbo mbalimbali shuleni. Kandi aliwafurahisha walimu na wanafunzi wenzake kwa tabia njema na kipaji chake alichokuwa nacho. Siku moja akiwa likizo yeye na wazazi wake walisafiri kwenda Mtwara, ambako walikaa huko kwa wiki tatu.

Jumamosi moja, Kandi alitembelea ufukweni mwa bahari, alikaa kando ya bahari akitazama mawimbi. Alifurahia kuona wimbi moja baada ya lingine, yalivyokuwa yakionesha umahiri. Siku hiyo, mawimbi yalikuwa makubwa sana. Yalionekana yakiviringika kama mpira wa miguu uwanjani. Alifurahishwa sana na mazingira hayo, yaliyomhamisha kifikra na kuzama katika mawazo mazito kuhusu rafiki yake Atu aliyekuwa naye shuleni.

Akiwa katika fikra hizo, ghafla alishtushwa na mti ulioangushwa na upepo mkali. Aliponyanyuka, alijikuta akiangukiwa na wimbi zito lililombeba mzobemzobe hadi kwenye kina kirefu cha bahari. Kwa vile hakuwa mgeni wa kuogelea, Kandi alipambana kiume na wimbi hilo zito ili kuokoa maisha yake yaliyokuwa mikononi mwa bahari. Katika kutapatapa, alikunywa vikombe kadhaa vya maji. Kufumba na kufumbua, alijikuta yumo mikononi mwa kijana mmoja, aliyembeba mpaka ufukweni mwa bahari. Kijana huyo alimpa huduma ya kwanza ya kumtapisha maji aliyokunywa, kwa kumkandamiza taratibu tumboni, huku akimpa pole.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 81 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kandi alipata ahueni na kuweza kutabasamu, alimshukuru sana kijana huyo, kwa kunusuru maisha yake. Alimwahidi kuwasiliana naye, pindi atakaporudi tena Mtwara. Aliporudi nyumbani, Kandi aliwasimulia wazazi wake yaliyompata. Wazazi walifurahi kumwona akiwa mzima na walimshukuru sana kijana huyo, kwa msaada aliotoa kwa binti yao kipenzi. Kutoka siku hiyo, Kandi akawa mwoga kutembelea fukwe za bahari, kwani "aliyeng'atwa na nyoka hata akiguswa na unyasi hushtuka."

## Maswali

1. Ukiwa kama mhakiki, bainisha wahusika wa hadithi uliyoisoma.
2. Fafanua lugha ya kisanaa iliyotumika katika hadithi.
3. Eleza dhamira zilizojitokeza katika hadithi uliyoisoma.
4. Unafikiri ni hadhira ipi iliyolengwa na maudhui ya hadithi?
5. Je, unadhani uhalisia wa maudhui unafaa kwa jamii iliyoandikiwa?

### Kazi ya 5.3

1. Fafanua dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi.
2. Fafanua sifa za mhakiki wa kazi za fasihi.

FOR ONLINE USE ONLY

### Zingatia

Mchakato wa kutafakari, kuchambua na kutathmini vipengele vya fani na maudhui katika kazi ya fasihi huitwa uhakiki. Uhakiki hufanywa na mhakiki aliyebobea katika kazi za fasihi. Mhakiki ni mtu mwenye taaluma ya kuchambua vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi. Dhima za mhakiki ni pamoja na kuchambua na kutathmini kazi ya fasihi, kumshauri mwandishi ili kuboresha kazi yake, kubainisha athari zinazoweza kutokea endapo kazi hiyo itapitishwa, na kuinua kiwango cha utunzi kwa waandishi wa kazi za fasihi.




Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 82 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zifuatazo ni sifa za mhakiki wa kazi za fasihi andishi: anapaswa kuifahamu historia ya mwandishi, kuifahamu falsafa ya mwandishi, kuwa na taaluma ya kuhakiki kazi inayohusika, kuwa msomaji wa kazi mbalimbali za watu na kuzifanyia uhakiki; awe mwadilifu na mzalendo. Mhakiki hana budi kuzingatia ukweli wa mambo yanayoelezwa, uhalisia wa watu, mazingira na matukio katika jamii na maudhui ya kazi hiyo kwa kuyahusisha na jamii inayolengwa. Pia, mhakiki azingatie umuhimu wa kazi hiyo ya fasihi kwa jamii. Uhakiki wa kazi yoyote ya fasihi hujikita katika vipengele vikuu viwili, yaani fani na maudhui.

**Kazi ya 5.4**

**Chunguza kielelezo kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**




**Kielelezo namba 5.1:** *Vipengele vya uhakiki wa kazi za fasihi andishi*



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 83 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Taja vijenzi vya umbo la kazi ya fasihi andishi.
2. Mambo yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi andishi yanaitwaje?
3. Kwa kutumia kielelezo ulichopewa, bainisha vijenzi vya maudhui.
4. Fafanua dhima za fasihi andishi katika jamii.
5. Unaelewa nini kuhusu muundo wa kazi za fasihi andishi?
6. Bainisha miundo mbalimbali ya kazi za fasihi andishi.

## Fani

Ufundi wa kisanaa unaotumika kuwasilisha ujumbe kwa jamii huitwa fani. Fani hujengwa na vipengele vifuatavyo: muundo, mtindo, wahusika, matumizi ya lugha na mandhari.

### Muundo

**Kazi ya 5.5**

Katika vikundi, kusanya mashairi kumi kutoka katika vitabu vya mashairi ulivyovisoma, kisha bainisha miundo iliyotumika.

FOR ONLINE USE ONLY

### Zingatia

Muundo ni mpangilio au mtiririko wa visa na matukio katika kazi ya fasihi.

Muundo unaweza kuwa wa moja kwa moja au msago, changamani na rejeshi. Muundo wa moja kwa moja huelezea matukio kwa mfuatano kuanzia la kwanza, hadi la mwisho, kama vile; kuzaliwa, kukua, kusoma, kuoa au kuolewa na mwisho kufa. Muundo rejeshi huelezea matukio bila kufuata mtiririko maalumu yaani hutumia mbinu ya urejeshi ya kumrudisha msomaji nyuma na kumpeleka mbele tena.

Muundo changamani huelezea matukio bila kufuata mtiririko maalumu yaani hutumia mbinu ya urejeshi na ya moja kwa moja au msago. Miundo hii hutumika katika tamthiliya na riwaya na siyo katika ushairi.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 84 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Muundo katika shairi hupambanuliwa kwa kuangalia idadi ya mistari au mishororo katika kila ubeti wa shairi. Muundo wa tathmina hujumuisha mashairi yenye mshororo mmoja katika ubeti. Muundo wa tathnia una mashairi yenye mishororo miwili tu katika ubeti wa shairi. Muundo wa tathlitha huwa na mistari mitatu katika ubeti wa shairi. Muundo wa tarbia una mistari minne kwa kila ubeti wa shairi. Muundo wa takhmisa huwa na mistari mitano katika ubeti. Muundo wa tasdisa au sudusia huwa na mistari sita inayokamilisha ubeti mmoja. Muundo wa sabilia huwa na mishororo saba na kuendelea kwenye ubeti mmoja. Muundo huo hutumiwa na waandishi kwa lengo maalumu.

## Mtindo

**Kazi ya 5.6**

Mitindo katika kazi ya fasihi hutofautiana kati ya msanii mmoja na mwingine. Onesha mifano ya mitindo katika kazi mbili za ushairi na mbili za tamthiliya ulizozisoma.

## Zingatia

Mtindo ni kipengele kimojawapo katika fani ambacho humtofautisha mwandishi mmoja na mwingine. Kwa hiyo, mtindo huonesha upekee wa mwandishi. Kuna mitindo mbalimbali inayotumika katika kazi ya fasihi kama vile: matumizi ya nafsi mbalimbali; dayalojia; barua; tanzu za fasihi simulizi ndani ya fasihi andishi, kwa mfano: nyimbo, methali, ngano na nyinginezo.

Mtindo katika shairi hutazamwa kama shairi limezingatia kanuni za utunzi wa mashairi au halijazingatia kanuni za utunzi wa shairi. Shairi linalozingatia kanuni za urari wa vina na mizani huitwa shairi la kimapokeo na lisilozingatia kanuni huitwa shairi la kisasa.

FOR ONLINE USE ONLY

**Kazi ya 5.7**

1. Tunga beti mbili za shairi, kisha eleza muundo na mtindo ulioutumia.
2. Tafuta kazi za wasanii wawili wa tamthiliya na riwaya soma, kisha onesha muundo na mtindo uliotumika, na wasilisha kazi hiyo darasani.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 85 9/6/21 5:54 PM

## Wahusika

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kazi ya 5.8

**Soma dayalojia ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

| | |
|---|---|
| **Baraka:** | Hivi bado unaendelea kuutwika tu na umri huu? |
| **Mzee Msa:** | Kwani shida nini Baraka, viwanda vya pombe vimefungwa? |
| **Mke wa mzee Msa:** | Pesa zote humalizia kwenye pombe. Hakumbuki mahitaji ya watoto shuleni? |
| **Mzee Msa:** | Mtajua ninyi wenyewe! Mimi ndo Msa bwana! Shuleni! Shuleni! |
| | Tulisoma sisi zamani bwana, siku hizi hata kulima hawalimi. Wanataka pesa tu. |
| **Kauki:** | Kweli kabisaaa! Enzi zetu kalamu na daftari tulikuwa tunapata shuleni. |
| **Mwenyekiti:** | (Anapita mwenyekiti) Kikao! Kikao! Kikao! Ninawakumbusha, kesho kutakuwa na kikao chetu cha maendeleo ya kijiji. |
| **Baraka:** | Jamani mimi nitahudhuria. Kikao hicho ni muhimu sana, ingawa nilipanga kutohudhuria. Vipi wewe Kauki! |
| **Kauki:** | Mimi nitaenda kama Msa ataenda. Asipoenda na mimi siendi, habari ndiyo hiyo mwenyekiti. |
| **Mzee Msa:** | Mimi ni mimi na wewe ni wewe! Mimi nikienda nimelewa, na wewe je utalewa? |

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

1. Mhusika yupi amebeba wazo kuu katika sehemu hii ya dayalojia?
2. Mhusika yupi anaonekana ana mawazo ya kizamani yasiyobadilika?
3. Je, kuna mhusika anayetegemea mawazo ya mtu mwingine?
4. Wahusika gani wamejitokeza mara chache?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zingatia

Vitu, watu au viumbe wanaotumiwa na msanii wa kazi ya fasihi andishi kuwasilisha ujumbe fulani kwa hadhira huitwa wahusika. Wahusika wanaweza kuwa wakuu na wasaidizi. Wahusika wakuu ni wale ambao hujitokeza kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kazi ya fasihi. Mara nyingi hubeba dhamira kuu. Wahusika wadogo hujitokeza mara chache ili kusaidia kujenga dhamira kuu katika kazi ya fasihi.

## Matumizi ya lugha

### Kazi ya 5.9

**Soma majibizano yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Mwalimu wetu wa somo la Kiswahili ni mahiri katika lugha. Siku moja katika kipindi chake alifundisha kuhusu matumizi ya lugha. Alianza kwa kusema:

**Mwalimu:** Wanafunzi, mlipokuwa wadogo mlijifunza Kiswahili kwa namna mbalimbali bila kujua usahihi wa maneno na wapi yatumike, siyo?

**Wanafunzi:** Kweli mwalimu!

**Mwalimu:** Kweli kabisa! Sasa mmoja wenu aje mbele achague karatasi mojawapo ya hizi zilizopo mezani.

**Wanafunzi:** “Mimi mwalimu,” Rehema alisimama na kuchukua karatasi moja (*huku akiitazama karatasi hiyo kwa makini*).

**Amina:** Na mimi! (*Amina naye alichukua nyingine hadi wanafunzi wanne*)

**Mwalimu:** Sasa Rehema anza kutusomea karatasi yako imeandikwa nini?

**Rehema:** Mwalimu naomba ruhusa kwenda kukojoa!

**Wanafunzi:** Hahahahahahaha! (*wote waliangua kicheko*)

**Mwalimu:** Mbona mnacheka? Nani anaweza kutuambia, je, Rehema amekosea kusema hivyo?

**Kauta:** Hapana! Sentensi hiyo ipo sahihi ila neno zuri lililopaswa kutumika badala ya kukojoa ni msalani.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 87 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Michael:** Hapana mwalimu! Neno zuri ni uani.

**Mwalimu:** Safi sana! Je, kuna mwingine anaweza kutuambia zaidi?

**Mauna:** Ndiyo mwalimu! Rehema alipaswa kusema naomba ruhusa kwenda kujisaidia.

**Mwalimu:** Wote mmejibu vema, yote ni majibu sahihi.

**Mwalimu:** Hawa, soma karatasi yako,

**Hawa:** (*Kwa sauti nyororo*) Mzee Ngombecha amekufa jana usiku.

**Mwalimu:** Nani atuambie, sentensi hii ipo sawa?

**Wanafunzi:** Hapana mwalimu, haipo sawa!

**Sikitu:** Hii ingefaa iwe, Mzee Ngombecha alifariki jana usiku.

**Taona:** (*Alinyoosha mkono*) Mwalimu, pia unaweza kusema Mzee Ngombecha ameaga dunia jana usiku.

**Mwalimu:** Vizuri sana. Ehe! Amina sentensi yako imeandikwaje?

**Amina:** Mti ulitoa machozi kwa kupoteza uhai uliosababishwa na wachoma mkaa.

**Wanafunzi:** Mh! Inakuwaje mwalimu, mti kutoa machozi?

**Mauna:** (*Alijaribu kujibu*) Ndiyo inawezekana, wakati mwingine katika fasihi viumbe visivyo na uhai huweza kupewa uwezo wa kutenda kama binadamu.

**Mwalimu:** Vizuri sana Mauna! Sasa mmeelewa kuhusu matumizi ya tamathali za semi na misemo?

**Wanafunzi:** Ndiyo mwalimu!

*(Mwalimu na wanafunzi waliendelea kuangalia maneno mengine.)*

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

1. Mwalimu alikuwa anafundisha kuhusu nini?
2. Ni aina ipi ya lugha ya kisanaa uliyojifunza katika tamthiliya hiyo?
3. Taja semi zilizojitokeza katika majibizano hayo?

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya 5.10**

1. Katika vikundi, tumia tamthiliya mbili ulizozisoma, kuonesha jinsi wasanii walivyotumia taswira katika kuipamba kazi yao.
2. Katika vikundi, chagua tamthiliya na riwaya moja ulizozisoma darasani, kisha onesha namna lugha ilivyotumika katika kazi hizo.

## Zingatia

Lugha ni nyenzo muhimu katika kazi ya fasihi. Lugha hujumuisha matumizi ya nahau, misemo, methali, vitendawili, taswira, na tamathali za semi. Aidha, lugha ya picha au taswira ni uwasilishaji wa dhana au ujumbe kwa kutumia picha kwa lengo la kumfikirisha msomaji au msikilizaji. Matumizi ya taswira huifanya kazi ya fasihi ipendeze na kuvutia. Tazama mfano wa taswira katika sentensi hizi:

(a) *Embe limeiva mtini* na kutamanisha wapita njia;
(b) *Njiwa wangu amekonda*;
(c) *Papai limeiva mtini* ila siruhusiwi kulichuma.

Hizo zote ni taswira zinazomaanisha binti au msichana mrembo katika miktadha tofautitofauti.

Tamathali ya semi inayotumiwa kuonesha dharau kwa mtu au kwa mhusika fulani kwa kutumia mbinu ya mafumbo huitwa *dhihaka*.

Mfano: (a) *Taigo ni msichana mwenye heshima kubwa sana kwa majirani hasa kwa wale wenye rika sawa na wazazi wake. Anastahili pongezi kwa jinsi alivyomsukuma Bibi Kizee na kumgalagaza chini pale kisimani waking'ang'ania nafasi ya kuchota maji.*

(b) *Mzee Machenje ndiye anayetoa hotuba leo, itabidi tubebe mablanketi.*

Katika mifano hiyo hapo juu, Taigo kupewa sifa ya heshima na kubebewa mablanketi kwa Mzee Machenje ni dhihaka.

Tamathali ya semi inayotumia lugha ya uficho ili kupunguza ukali wa maneno huitwa *tasifida/tafsida*.

Mfano: (a) Amina *alifariki dunia* wakati akijifungua watoto pacha ("alifariki" badala ya "alikufa", "alijifungua" badala ya "alizaa").

(b) Mama wa mtoto anayelia amekwenda *uani* ("uani" badala ya "chooni").

Tamathali ya semi inayotumiwa kuleta maana kinyume na hali halisi au ukweli huitwa *stihizai* au *kejeli*.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mfano: (a) Rafiki kipenzi wa ndugu Mangara hapa mtaani ni bwana Nchugu, kila wanapokutana mmoja wao hubadili uelekeo. (Ukweli: Nchugu ni adui wa bwana Mangara).

(b) Wewe una nguvu sana, umewezaje kupigwa? (Ukweli ni kwamba hana nguvu ya kupigana).

Usemi wa kimafumbo unaomsema mtu vibaya katika simulizi au hadithi huitwa *kijembe*.

Mfano: (a) Mwaka huu, Joni umevuna mahindi gunia hamsini kwenye shamba ambalo halikupaliliwa.

(b) Kijana yule ni msafi, kila apitapo nzi humshangilia.

Tamathali ya semi inayolinganisha matendo au vitu vyenye maumbile tofauti bila kutumia viunganishi huitwa *sitiari*. Mara nyingi sifa zinazolinganishwa huwa haziko wazi au kufanana kiuhalisia na kinacholinganishwa.

Mfano: (a) Mwakingi ni nyoka mwenye sumu kali.

(b) Bahati ni mkaa.

Tamathali ya semi inayotumika kulinganisha vitu viwili au zaidi kwa kutumia viunganishi kama vile: mithili ya, kama, kuliko, sawa na, mfano wa, hujulikana kama *tashibiha* au *mshabaha*.

Mfano: (a) Noge ana shingo ndefu *kama* twiga.

(b) Alizurura ovyo mtaani *mithili ya* mbwa koko.

Tamathali ya semi inayovipa vitu uwezo wa kutenda kama binadamu wakati havina uwezo huo huitwa *tashihisi*.

Mfano: (a) Jogoo alitoa wosia kwa watoto wake.

(b) Shoka linalia msituni.

Tamathali ya semi ambayo mtu huuliza swali ambalo tayari anafahamu jibu lake huitwa *tashtiti*.

Mfano: (a) Hata wewe umekuja?

(b) Hivi wewe ni mwanafunzi?

Tamathali ya semi inayoonesha msisitizo kwa kutumia ukinzani wa maneno bila kubadilisha maana iliyokusudiwa huitwa *tabaini*.

Mfano: (a) Maziwa si maziwa.

(b) Roho inacheka, macho yanalia.

*Taashira* hutumia neno kuwakilisha dhana fulani.

Mfano: (a) Mvi – mzee, (b) Sungura - laghai/ mjanja

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mbinu ya takriri huonesha urudiaji wa maneno katika kutilia mkazo jambo fulani. Mfano: (a) Na leo wamekuja wale wale!
(b) Maji! Maji! Mama majii!

*Nidaa* hutumika kuonesha mshangao.
Mfano: (a) Kumbe! Ameng'olewa jino!
(b) Ala! Anaumwa!

Mbinu ya kisanaa ambayo mwandishi hutumia maneno yanayofuatana bila viunganishi huitwa *mjalizo*.
Mfano: (a) Dada alinunua, akabeba, akapeleka nyumbani.
(b) Alichanja, akafunga, akajitwisha, akaondoka.

Hali ya kuongeza sifa za ziada au kutia chumvi katika mazungumzo ya jambo fulani ili kumvutia msikilizaji huitwa *mubalagha*.
Mfano: (a) Alikula wali sufuria lile kubwa peke yake.
(b) Alikunywa maji pipa zima.

Tamathali ya semi ambayo huigiza sauti au milio ya vitu au hali mbalimbali huitwa *tanakali sauti*.
Mfano: (a) Bunduki ilipiga tutututuuuu!
(b) Alianguka chini puuuu!

Tamathali ya semi ambayo sifa ya mtu au kitu hutumika kurejelea tabia au mwenendo wa watu wengine huitwa *taniaba*.
Mfano: (a) Magufuli alikuwa ni Nyerere wa serikali ya awamu ya tano.
(b) Maimuna ni Kezilahabi mpya.

Mbinu ya kisanaa ambayo maneno huandikwa kwa kuacha nafasi bila kukamilishwa kwa neno, sehemu ya neno au kifungu cha maneno ni *mdokezo*.
Mfano: (a) Alikula, akashiba, kisha …..
(b) Mwalimu alifundisha somo lake kwa ….. akapewa zawadi.
(c) ……., baada ya chakula cha mchana.

FOR ONLINE USE ONLY

## Mandhari

**Kazi ya 5.11**

Katika vikundi, chagua riwaya na tamthiliya mbili ulizozisoma, kisha jadili mandhari iliyotumika kwa kila kazi ya fasihi.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 91 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Zingatia

Mahali, eneo au mazingira ambayo yamechaguliwa na mwandishi ili kuwasilisha visa na matukio katika kazi ya fasihi, huitwa mandhari. Mandhari yaweza kuwa halisi au ya kubuni, mfano: porini, baharini, ziwani au nchi kavu.

## Maudhui

Maudhui ni jumla ya mambo ambayo mwandishi anakusudia kuyafikisha kwa hadhira, yaani mambo ambayo mwandishi anayazungumzia katika kazi ya fasihi. Vipengele vya maudhui hujumuisha dhamira, migogoro, ujumbe, mtazamo na falsafa.

### Dhamira

**Kazi ya 5.12**

Diwani mbalimbali za ushairi ni muhimu sana kwa jamii ya leo. Thibitisha dai hili kwa kutumia diwani mbili ulizozisoma darasani.

### Zingatia

Dhamira ni lengo au wazo ambalo mwandishi huibua katika jamii. Dhamira zimegawanyika katika sehemu mbili, dhamira kuu na dhamira ndogondogo. Dhamira hufahamika kutokana na upeo wa wasomaji. Dhamira ndicho kiini cha kazi yoyote ya fasihi. Katika kazi ya fasihi, dhamira huweza kuwa: umuhimu wa elimu, uzalendo, usaliti, na nyinginezo.

FOR ONLINE USE ONLY

### Migogoro

**Kazi ya 5.13**

1. Katika vikundi, eleza namna waandishi wa kazi za tamthiliya wanavyotumia kipengele cha migogoro kuwasilisha dhamira zao.
2. Katika vikundi, kwa kutumia tamthiliya moja uliyoisoma, fafanua migogoro iliyojitokeza ndani ya tamthiliya hiyo.

### Zingatia

Migogoro ni hali ya kuvutana au kukinzana inayotokea ndani ya nafsi ya mtu, kati ya mtu na mtu au kundi la watu. Mhakiki hana budi kuangalia migogoro au



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 92 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ukinzani unaoweza kujitokeza ndani ya kazi ya fasihi na jamii husika. Migogoro hiyo yaweza kuwa ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Vilevile mhakiki anatakiwa kuonesha suluhisho la migogoro iliyojitokeza kwa kutoa fundisho chanya na kuwatia moyo wasomaji au jamii.

### Ujumbe

**Kazi ya 5.14**

Fafanua jinsi waandishi wa riwaya mbili ulizozisoma walivyofanikiwa kutoa ujumbe kwa hadhira yake.

### Zingatia

Ujumbe ni funzo au mafunzo yapatikanayo ndani ya kazi ya fasihi. Ujumbe unaweza kuwa: umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji, rushwa ni adui wa haki, asiyesikia la mkuu huvunjika guu na maonyo mengine.

### Mtazamo

**Kazi ya 5.15**

Katika vikundi, jadili mtazamo wa mwandishi wa kazi ya fasihi andishi katika tamthiliya mbili ulizozisoma darasani.

### Zingatia

Mtazamo ni uwezo wa binadamu katika kuyaona mambo mbalimbali. Kila mwandishi huwa na mtazamo tofauti kwa jinsi anavyoyaona mambo. Mtazamo huo huweza kuwa hasi au chanya (kiyakinifu au kidhanifu) kuhusu mambo fulani ya kijamii.

### Falsafa

**Kazi ya 5.16**

Kila mwandishi wa kazi ya fasihi andishi huwa na falsafa yake bainifu. Thibitisha dai hili, kwa kutumia kazi mbili za riwaya ulizozisoma darasani.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 93 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zingatia**

Falsafa ni imani ya mwandishi kuhusu mambo anayoyaandikia. Falsafa ya mwandishi huathiriwa na mazingira alimozaliwa, alimokulia, alimosomea au anamofanyia kazi. Aidha, falsafa ya mwandishi hujidhihirisha baada ya kuzisoma kazi zake, mfano msanii kuamini katika ukale, usasa, mila na desturi, udini au upagani.

### Kufaulu na kutokufaulu kwa mwandishi

**Kazi ya 5.17**

Kwa kutumia riwaya na tamthiliya moja uliyoisoma, onesha namna mwandishi alivyofaulu kuonesha uhalisia wa dhamira zake kwa jamii.

**Zingatia**

Mhakiki anapaswa kuangalia namna jina la kitabu linavyoweza kusadifu maudhui yaliyomo kwenye kitabu. Kufaulu kwa mwandishi ni namna mwandishi alivyoweza kuonesha uhalisia wa dhamira zake, ujumbe uliokusudiwa na lugha iliyotumika kwa jamii yake (hadhira yake). Kutofaulu kwa mwandishi ni mwandishi kushindwa kufikisha ujumbe uliokusudiwa hata kupotosha jamii, au kutoweza kutumia lugha vizuri.

### Uhakiki wa riwaya

**Kazi ya 5.18**

**Soma kipande cha riwaya, kisha jibu maswali yanayofuata:**

Nilipozinduka usingizini nilijikuta nikizomewa na miti mirefu, iliyoshuhudia kushindwa kwangu. Nilijaribu kujigeuza upande kuangalia labda nitamwona mtu. Walionekana mbu waliokuwa wakishangilia chakula kitamu, walinizunguka huku wakiwa na siha njema. Nilijaribu kujivuta, angalau niinuke lakini mwili ulikuwa mzito na wenye maumivu makali. Hapo nilitambua kuwa nilikuwa nimejeruhiwa vibaya. Bila kufikiria nini kilichonifikisha hapo msituni, nilifurukuta kutaka kunyanyua miguu yangu. Miguu ilikuwa mizito sana, lakini uzito huo ulichangiwa na kamba zilizokuwa zimefungwa kiustadi na mchanja kuni aliyetaka kuufikisha mzigo uliosheheni kuni bila kupungua hata moja.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Basi, nilijisemea moyoni, "endapo nimelala usiku wote huku sikudhurika, inawezekana hakuna wanyama wenye uchu kama simba."

Niliendelea kutafakari sababu ya kupata mateso hayo, "kijana niliyekuwa na kazi nzuri, nyumba na gari la thamani." Nikakumbuka siku niliyotumiwa ujumbe mzito kwenye simu yangu, ulionitaka kuachana kabisa na msichana Maiona. Binti huyo aliumbika mithili ya malaika na aliwavutia vijana kwa wazee pale mtaani. Maiona alikuwa binti mrefu wa Kimaasai, mwenye rangi ya kahawia na umbo la namba sita. Kifuani pake palikuwa na dodo mbili ambazo kila moja ilionesha kutaka kumshinda mwenzake.

Siku hiyo kulikuwa na jua lililonipa matumaini ya usalama wa afya yangu. Mara nikasikia sauti zikizungumza kwa mbali, nilitulia ili kuzipata sauti hizo pengine hata nisikie majina ya watu hao, lakini haikuwa hivyo. Walitokea vijana wawili waliovalia kininja. Huku mmoja wao, akiwa amebeba mguu wa kuku aliokuwa akiuzungusha kidoleni mwake. Nilihisi pengine utakuwa mwisho wa maisha yangu, ila kimoyomoyo niliendelea kumsihi Mungu anusuru uhai wangu.
Vijana hao walinitazama, kisha wakasema, "We fisi mwenye uchu, kama unataka kuishi, achana na mali za watu."

Baada ya mwezi mmoja, nikiwa ofisini, simu yangu ya mkononi iliita. Nilipoangalia vizuri, kumbe Maiona alikuwa ananipigia. Mwili wangu ulisisimka mithili ya mtu aliyemwagiwa maji ya barafu. Nilipunguza sauti na kuifunika simu kwa gazeti lililokuwa pembeni mwangu, huku nikisema, "kama nilinusurika siku ile, basi mimi si Moses, siwezi kupoteza uhai kwa sababu ya Maiona. Sitaki kuwaumiza wazazi wangu walionisomesha kwa shida kwa kuuza mihogo, eti Maiona, Maiona achana na mimi." Nilijisemea kwa sauti ya chini.

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

1. Bainisha muundo uliotumika katika kipande hicho cha riwaya.
2. Onesha matumizi ya lugha jinsi yalivyojitokeza katika kipande cha riwaya ulichokisoma.
3. Fafanua dhamira tatu zilizojitokeza kwenye kipande hicho cha riwaya.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 95 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Onesha migogoro iliyojitokeza katika kipande hicho cha riwaya.
5. Eleza ujumbe uliojitokeza katika kipande hicho cha riwaya.
6. Kwa kutumia mifano, bainisha vipengele vya fani vilivyojitokeza katika kipande hicho cha riwaya.
7. Kwa mifano, bainisha vipengele vya maudhui vilivyojitokeza katika kipande hicho cha riwaya.

**Kazi ya 5.19**

Soma hadithi au matini yoyote ya kifasihi, bainisha dhamira na ujumbe uliojitokeza, kisha fanya uwasilishaji darasani.

**Kazi ya 5.20**

1. Tembelea maktaba ya shule au mahali popote unapoweza kupata vitabu vya riwaya, kisha chambua fani za riwaya tatu ulizozisoma.
2. Tembelea maktaba ya shule au mahali popote unapoweza kupata vitabu vya riwaya, kisha chambua maudhui ya kila riwaya.
3. Katika vikundi, chagua riwaya moja, kisha hakiki kufaa au kutokufaa kwa vipengele vya maudhui.
4. Katika vikundi, linganisha na linganua miundo ya riwaya mbili ulizozisoma.

FOR ONLINE USE ONLY

**Zoezi la 5.1**

1. Eleza vipengele vikuu vya uhakiki wa kazi za riwaya.
2. Onesha migogoro inayoweza kujitokeza ikiwa uhakiki wa kazi fulani ya fasihi haukufanyika vizuri.
3. Uhakiki wa riwaya umepitwa na wakati katika zama za sayansi na teknolojia. Jadili.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 96 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya 5.21**

Katika vikundi, chagua riwaya mbili ulizozisoma, kisha linganisha na linganua matumizi ya lugha ya riwaya hizo.

## Uhakiki wa tamthiliya

**Kazi ya 5.22**

**Soma sehemu ya tamthiliya, kisha jibu maswali yanayofuata.**

*(Nyumbani kwa mwalimu Majaliwa. Mama Uyanjo, Uyanjo na Tumaini wanaonekana. Mama yuko mezani anakunywa chai. Uyanjo amekaa kwenye meza ndogo anasoma, na Tumaini anazunguka sebuleni akikimbiza gari lake la maboksi.)*

**Uyanjo:** We, Tumaini, acha kelele, nitalitupa boksi lako nje! Tulia.

**Mama Uyanjo:** Acha mwenzako acheze, mbona wewe ulicheza, hakuna aliyekuzuia.

**Uyanjo;** Mama, si wewe ulikuwa ukitupa makopo yangu nje?

**Mama Uyanjo:** Ndiyo, Lakini huo si ulikuwa uchafu ndani ya nyumba?

**Uyanjo:** Sasa huoni huyu naye anapiga kelele wakati mimi nasoma?

**Mama Uyanjo:** Sawa, hebu nenda ukachochee moto mboga iive halafu ubandike chungu motoni, kabla mlevi huyu hajarudi.

**Uyanjo:** Mama huoni mimi nasoma, si uende wewe!

**Mama Uyanjo:** Tunabishana ee, nenda haraka. Kusoma, kusoma nini, wewe mtu wa shule kweli? Hebu fanya haraka *(Uyanjo anainuka.)*

**Mama Uyanjo:** Tumaini njoo baba nikupe chai.

**Tumaini:** Mimi sitaki chai nataka maziwa.

**Mama Uyanjo:** Maziwa tutayatoa wapi, baba yako ananywea pombe hela zake zote. Na leo atanitambua.

**Tumaini:** Utamchapa? Na mimi nitamchapa, mama. *(Uyanjo anaingia kutoka jikoni.)*

**Mama Uyanjo:** Hivi Uyanjo baba yako alitoka saa ngapi hapa?

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 97 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Uyanjo:** Sijui.

**Mama Uyanjo:** Tumaini, baba alienda dukani saa ngapi?

**Tumaini:** Duum! Duu. Duuu. Duum, pipipii! Vuuum! Unaona breki ya gari yangu, mama!

Mghanga (2007:20-21)

## Maswali

1. Chagua mhusika mmoja, kisha eleza namna mwandishi alivyomchora katika sehemu hii ya tamthiliya.
2. Bainisha matumizi ya lugha katika sehemu ya tamthiliya uliyoisoma.
3. Vitendo vya wahusika "Mama na baba Uyanjo" vina athari gani katika malezi ya watoto?
4. Eleza kwa kifupi dhamira nne zilizojitokeza katika tamthiliya uliyoisoma.

## Kazi ya 5.23

1. Katika vikundi, chagua tamthiliya mbili ulizozisoma, kisha linganisha na linganua matumizi ya fani ya tamthiliya hizo.
2. Kwa kutumia tamthiliya mbili ulizozisoma, chambua maudhui ya kila tamthiliya.
3. Katika vikundi, chagua tamthiliya mbili, kisha hakiki kufaa au kutokufaa kwa vipengele vya maudhui vilivyotumika.

## Zoezi la 5.2

1. "Mhakiki wa tamthiliya ni mwanajamii halisi." Jadili kauli hii.
2. Kwa kutumia tamthiliya mbili ulizozisoma, onesha migogoro iliyojitokeza na namna ilivyotatuliwa ukihusianisha na hali halisi ya jamii yako.
3. Kwa kutumia tamthiliya mbili ulizozisoma, jadili kufaulu na kutokufaulu kwa waandishi wa tamthiliya hizo.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 98 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Uhakiki wa ushairi

### Kazi ya 5.24

**Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

A. Charuka ndugu usome, uijue na dunia,
Charuka kaka kiume, mambo usijekosea,
Charuka dada kwa shime, vitabu kuvipekua,
Safari yaendelea, charuka chacharukaka.

B. Malengo kuyafikia, jamani si maongezi,
Hasa litotuinua, ni kuwa wachapakazi,
Jukumu kutumikia, raia na viongozi,
Tuyazingatie haya, wala tusirudi nyuma.

C. Akunyanyuae, unapoanguka,
Akupangusae, kiingia vumbini,
Akujaziae, uwapo kasoro,
Hisani hulipwa.

D. Japo yeye anawake, sheriani,
Ni ladhaye, amshike, wa fulani,
Shukuruye, ni mateke, kwa wandani,
Kwa nini?

TAKILUKI (2001:33)

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

1. Chunguza beti za shairi A na B, kisha eleza mtindo uliotumika.
2. Bainisha dhamira zilizojitokeza katika beti hizo.
3. Eleza muundo uliotumika katika beti za shairi C na D.
4. Mshairi anaposema hisani hulipwa katika shairi C anamaanisha nini?

### Kazi ya 5.25

1. Katika vikundi, tumia vitabu viwili vya ushairi kuonesha miundo mbalimbali iliyotumika.
2. Chagua beti tatu za shairi lolote, zisome, kisha bainisha dhamira zilizojitokeza na kufanya uwasilishaji darasani.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 99 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya 5.26

1. Tembelea maktaba ya shule, chagua kazi moja ya ushairi, soma kisha, eleza vigezo vilivyotumika kuihakiki.
2. Soma kazi mbili za ushairi, kisha onesha namna mwandishi alivyofanikiwa kutumia mandhari ya kila kazi uliyoisoma.

## Zoezi la 5.3

1. "Wasanii wa diwani nyingi wamepuuza kuzungumzia suala la maadili." Thibitisha dai hilo kwa kutoa hoja tano kwa kutumia diwani mbili ulizozisoma darasani.
2. Jadili nafasi ya mwanamke katika kazi mbili za ushairi ulizozisoma.
3. Fafanua sifa za mhakiki wa kazi za ushairi.
4. "Mhakiki wa ushairi ni mzalendo na mwanajamii halisi." Jadili kauli hiyo.
5. Ufisadi ni sumu ya maendeleo katika jamii. Kubali au kataa kwa hoja madhubuti, tumia kazi moja ya ushairi uliousoma kujibu swali hili.

FOR ONLINE USE ONLY

## Zoezi la marudio la 5

1. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

   (i) Katika kubaini mtindo wa riwaya, tunazingatia ______
   - (a) urari wa vina na mizani
   - (b) utoshelevu wa maudhui
   - (c) mpangilio wa visa na matukio
   - (d) hali ya wahusika
   - (e) urefu wa visa

   (ii) Ufundi wa kupangilia maneno, visa, matukio pamoja na uchaguzi wa namna bora ya uwasilishaji bila kuichosha hadhira huitwa ______
   - (a) usomi

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) maudhui
(c) utoshelevu
(d) Mandhari
(e) fani

(iii) Mashairi yenye mishororo miwili katika ubeti huitwa ______
(a) tasdisa
(b) tathmina
(c) tathnia
(d) tarbia
(e) tathlitha

(iv) Muundo katika shairi hujulikana kwa kuangalia ______
(a) idadi ya beti katika mshororo
(b) ubora wa dhamira
(c) idadi ya mistari katika ubeti
(d) mpangilio wa silabi katika shairi
(e) idadi ya mikarara katika shairi

(v) Ifuatayo ni moja ya sifa ya mhakiki wa kazi ya fasihi.
(a) Awe anamfahamu mwandishi kwa undani.
(b) Awe amesoma kazi nyingi za fasihi.
(c) Hapaswi kumpa mwandishi ari ya kuendelea na uandishi.
(d) Awe zao la jamii iliyoandikiwa.
(e) Awe ameandika kazi moja tu.

2. Eleza dhima ya uhakiki.

3. Fafanua umuhimu wa fani katika kazi ya fasihi.

4. Hakiki vipengele vya fani katika ubeti huu.
"Kulibeba nimechoka, pendo nilifanye nini?
Halitaki kunishuka, limenikaa moyoni,
Nataka kupumzika, laumiza kifuani."

5. Taja methali unazoweza kutumia kuadilisha watu wenye tabia zifuatazo:
(a) Mtu mwenye tabia ya wizi.
(b) Mtu asiyejali jeraha dogo mwilini mwake.
(c) Mtu anayerukia magari na hakubali ushauri wa katazo la anachofanya.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

6. Eleza sababu mbili za kufanya uhakiki wa kazi za fasihi.

7. Katika riwaya mbili ulizozisoma, bainisha dhamira zinazofanana, kisha eleza mazingira ya utokeaji wa kila dhamira.

8. Jadili nafasi ya mwanamke shuleni au kijijini kwenu ukihusianisha na riwaya mbili ulizozisoma.

9. Ukiwa kama mhakiki na mchambuzi, jadili majukumu ya kijinsia yanayojitokeza katika jamii yenu.

10. Oanisha maswali ya sehemu A na majibu yake katika sehemu B.

| Sehemu A | | Sehemu B |
|---|---|---|
| i. | Mambo ambayo msanii wa kazi ya fasihi anayawasilisha katika jamii yake ________ | Tashtiti |
| ii. | Tamathali ya semi ambayo mtu huuliza swali ambalo tayari ana jibu lake _________ | Fasihi |
| iii. | Watu au wanyama anaowatumia mwandishi kubeba ujumbe fulani katika kazi ya fasihi ________ | Maudhui |
| | | Riwaya |
| iv. | Hali ya pande mbili kukinzana katika masuala ya kijamii _________ | Mhakiki |
| v. | Kazi ya sanaa inayotumia lugha ya mazungumzo au maandishi kufikisha ujumbe kwa hadhira ________ | Tashihisi |
| | | Fani |
| vi. | Silabi za mwisho au za kati ambazo hufanana katika shairi. ____________ | Wahusika |
| vii. | Tamathali ya semi ambayo vitu au viumbe wasio binadamu hupewa nafasi ya kutenda kama binadamu ________ | Vina |
| viii. | Mtu anayechambua kazi za fasihi kwa kutumia weledi ________ | Migogoro |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Sita

## Utungaji wa kazi za fasihi andishi

### Utangulizi

*Fasihi andishi inahitaji ufundi na ubunifu katika kutunga na kuwasilisha mawazo kwa jamii. Katika sura hii, utajifunza kutunga hadithi, riwaya na tamthiliya kwa kuzingatia misingi mbalimbali. Pia, utabaini sifa zitakazokusaidia katika utunzi wa kazi za fasihi andishi. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutunga kazi mbalimbali za fasihi andishi kwa masilahi yako na taifa katika miktadha mbalimbali.*

### Utungaji wa hadithi fupi

**Kazi ya 6.1**

**Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Hapo zamani za kale, kulikuwa na mji mmoja uliokuwa na watu wengi wenye utajiri wa vito na vitu vingine vya thamani. Mji huo ulikuwa miongoni mwa kisiwa kilichomo kwenye Bahari ya Wapendanao. Siku moja tetemeko kubwa lilitokea katika mji huo na kusababisha ardhi kumeza watu wote. Zimwi pamoja na binti mrembo aliyeitwa Ziolela walinusurika. Tetemeko hilo, lilisababishwa na malkia wa majini mwenye kijicho aliyetaka aolewe na mwana wa mfalme.

Baada ya kukataliwa, alisababisha tetemeko ambalo halikumuua kijana huyo bali lilisababisha mji kupotea. Ziolela alikuwa ni mtoto pekee kwa wazazi wake. Alikuwa akijishibisha kwa matunda mawili ya komamanga ambayo yalikuwa yakitokea kila siku katika mti uliokuwa karibu na gofu alilokuwa akiishi. Zimwi lilikuwa likiishi mbali na binti huyo na hakuna aliyejua uwapo wa mwingine.


FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 103 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Asubuhi moja, Ziolela alishikwa na bumbuazi kuona tunda la tatu, katika mti wa mkomamanga na hakuelewa maana yake. Baada ya muda mfupi, Zimwi lenye pembe ndefu, meno manne marefu, kucha ndefu na manyoya mwili mzima, lilitokea kwa kishindo karibu na mahali alipokuwa amesimama Ziolela. Hapo ndipo paliposalia baada ya kasri lao kumezwa na ardhi. Kwa mshtuko na hofu kubwa ya kishindo hicho na ngurumo, Ziolela alipoteza fahamu na kuanguka. Zimwi lilimchukua Ziolela hadi kwenye jumba lake ambapo lilimlaza kwenye kitanda kizuri, likakaa pembeni yake, likimwangalia. Uzuri wa Ziolela, ulilifanya lizame kwenye mahaba mazito kwa siku nzima na kusahau kabisa kuwa Ziolela atazinduka wakati wowote. Wakati likiwa kwenye raha ya kumpata binti, ghafla Ziolela alizinduka usingizini. Ziolela alipofumbua macho, alijikuta akitazamana na Zimwi ana kwa ana. Alipiga yowe za kuomba msaada, kisha akazimia tena.



Baada ya muda mfupi kupita, Ziolela aliamka na kujikuta yumo kwenye chumba kingine kizuri kilichosheheni kila aina ya mapambo na harufu nzuri ya marhamu ilikijaza chumba hicho. Alipopepesa macho yake hakuona mtu yeyote ila meza ndogo yenye chakula kizuri kilichomvutia kwa harufu nzuri. Kutokana na njaa aliyokuwanayo, bila kujali alikula chakula hicho. Aliendelea kuishi kwenye chumba hicho kwa muda wa wiki nzima bila kuonana na mwenyeji wake. Aliendelea kushangaa kila siku kukuta chakula kitamu kimewekwa mezani na mpishi asiyemjua.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 104 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Jioni moja, jua lilipozama, Ziolela akiwa kwenye bustani ya maua akiburudishwa na sauti nzuri za ndege na vipepeo waliokuwa wakiruka kutoka ua moja hadi lingine, alisikia sauti nzuri ya mlio wa zeze kutoka juu ya jengo hilo. Taratibu, akiwa na shauku ya kutaka kujua itokako sauti hiyo, kwa hofu alifungua mlango akanyatia kama vile simba anyatiavyo swala. Hatimaye, kupitia tundu dogo la kitasa cha mlango aliliona Zimwi likipiga zeze hilo kwa weledi mkubwa. Aligeuka polepole na kurudi chumbani kwake huku akifikiria hatima ya kuwapo katika jumba hilo.

Usiku ule, Ziolela hakupata usingizi pamoja na kwamba alipata huduma zote kutoka kwa Zimwi. Akiwa ameelemewa na usingizi, alijikuta katika ruya, akiwa juu ya farasi mwenye mbawa angani na nyuma ya farasi huyo likiwa limekaa Zimwi lenye rangi ya kuvutia na kumeremeta. Wakiwa angani, Ziolela aliliona Zimwi likibadilika likawa kijana mzuri mwenye miraba minne na alionekana mfua uji aliyefanana na mwana wa mfalme. Ziolela alivutiwa sana na kijana huyo. Kijana huyo alipotaka kumbusu, Ziolela alishtuka usingizini huku mapigo ya moyo yakienda mbio. Alipiga moyo konde, akalala.

Kulipokucha, alikaa akitafakari ndoto hiyo na asijue cha kufanya. Ghafla alishtushwa na Zimwi lililoingia likiwa na sura ya furaha na kumsalimia kwa sauti nzito "Umeamkaje mrembo" kwa hofu alijibu "Si-si- sijambo." Zimwi likamwambia "Usiogope mrembo," kisha liliondoka na kumwacha Ziolela akiwa ameshikwa na bumbuazi.

Kadri siku zilivyoenda, Ziolela alizidi kuwa karibu na Zimwi hilo na hatimaye wakawa marafiki. Zimwi lilimsimulia Ziolela ni kwa namna gani malkia wa majini aliligeuza mpaka likawa katika hali ya uzimwi. Kisa hicho kilimhuzunisha sana Ziolela, alilionea huruma Zimwi. Katika utulivu huo, Zimwi liliona ni wakati pekee wa kurusha ndoano yake kwa binti mrembo. Liliamua kumuuliza Ziolela, "Mrembo unanipenda, tuoane?" Ziolela alishtuka kwani hakutegemea kuulizwa swali hilo. Siku hiyo, alishindwa kujibu kwa kuhofia usalama wake. Alifikiri, kwa uzuri alionao, atawezaje kuolewa na kiumbe wa ajabu namna hiyo? Zimwi halikukata tamaa. Siku nyingine lilimkuta Ziolela akiwa amegubikwa na mawazo lukuki huku akitiririsha machozi. Zimwi lilimbembeleza, kisha likamuuliza "Mrembo una nini?" Kwa uchungu na majonzi, Ziolela alilisimulia Zimwi mkasa wote wa tetemeko na jinsi mji wao ulivyomezwa na udongo na kubaki yeye peke yake. Zimwi lilimwonea huruma na likamwahidi litamsadia kuurudisha mji na familia yake, endapo atakuwa tayari kuolewa nalo. Kwa shauku ya kutaka kuwaona wazazi wake, Ziolela alikubali kwa shingo upande.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Usiku wakiwa wamelala, kulitokea upepo mkali ulioleta vumbi jingi na giza nene katika mji huo. Ziolela akihofia kuwapo kwa tetemeko alitoka chumbani, akaelekea kwenye chumba cha Zimwi. Baada ya muda mfupi, kupitia dirishani, kwa mbali aliona mji wa kwao unawaka taa za rangi nyingi. Ghafla Ziolela aligeuka na kulirukia Zimwi. Akalikumbatia na kulibusu kwa shukurani. Kwa kitendo hicho, Zimwi lilibadilika na kuwa kijana mzuri mwenye miraba minne aliyefanana na mwana wa mfalme. Ziolela alifurahi kumwona kijana wa ndoto yake siku hiyo. Kijana huyo akasema, mimi ninaitwa Kaifu, ni mwana wa mfalme wa Sokete. Ninakushukuru sana kwa kuniokoa kutoka hali ya uzimwi. Wewe ni mke niliyekuwa nikikusubiri siku nyingi sana, kesho tutakwenda kwa wazazi wako. Kulipokucha walikwenda kwa mfalme, walikaribishwa vizuri na kila mmoja alisimulia mkasa wake uliomkuta, pamoja na mji uliopotea kurudishwa. Mfalme alifurahi na kumshukuru sana Kaifu kwa kuwaokoa. Kutokana na furaha hiyo, mfalme alipiga mbiu kuwaita watu wote na kuwaeleza, jinsi kijana alivyowaokoa. Kaifu na Ziolela wakaamua kuoana, na Mfalme akawafanyia sherehe nzuri isiyo kifani. Wakaishi kwa raha mustarehe.

## Maswali

1. Kisa hicho kinahusu nini?
2. Ni dhoruba gani iliwakuta watu wa mji unaozungumziwa kwenye habari?
3. Kwa nini mfalme alifurahi?
4. Mhusika mkuu katika kisa hicho ni nani?
5. Bainisha wahusika wa kisa hicho, kisha onesha uhusika wa kila mmoja.

### Kazi ya 6.2

1. Tafuta visa au matukio mbalimbali kuhusu kijiji au mtaa wenu kwa kuuliza wazee au watu wengine unaofikiri watakuwanayo, ulizia jinsi kilivyoanza na hatua kiliyopitia hadi sasa. Andika hadithi fupi kuhusu kijiji au mtaa huo kwa kuzingatia taratibu na kanuni za uandishi.
2. Andika kisa ukipendacho kwa kuzingatia kanuni za utunzi wa hadithi fupi, kisha simulia darasani.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 6.1**

1. Eleza dhamira zilizojitokeza katika hadithi ya Ziolela na Zimwi.
2. Fafanua vipengele vya fani ulivyovibaini katika hadithi ya Ziolela na Zimwi.
3. Ugomvi na migogoro ni sehemu ya maisha ya jamii yoyote ile. Fafanua migogoro iliyojitokeza katika hadithi ya Ziolela na Zimwi.

### Zingatia

Utungaji ni namna au jinsi ya kupangilia visa na matukio katika maandishi kwa lengo la kuburudisha, kuelimisha na kuakisi hali halisi ya maisha ya jamii inayohusika. Msanii hana budi kutumia ubunifu wa hali ya juu katika lugha kwenye utunzi wa kazi za fasihi andishi.

Masimulizi ya kubuni yanayosawiri tukio, tabia, mgogoro au kipengele cha maisha kwa ufupi huitwa hadithi. Hadithi fupi huwa na tukio moja au mawili na hutumia mawanda finyu. Hadithi fupi huwa na wahusika wachache na huandikwa kwa muda mfupi. Baadhi ya fani zilizochangia kuibuka kwa hadithi fupi ni ngano, hekaya, visasili, michapo na tendi. Katika kutunga hadithi fupi, sharti upendekeze visa vya kutungia. Mfano wa visa hivyo ni kisa cha jogoo kuwa na kishungi au kisa cha twiga kuwa na shingo ndefu.

## Utungaji wa riwaya

**Kazi ya 6.3**

**Soma kipande kifuatacho cha riwaya, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Baada ya muda mrefu kupita bila kupata kazi, Bela na Shida walikuwa wamekaa kitandani wanatafakari hatima ya maisha yao, kwani hawakuona dalili za kupatiwa kazi. Kila siku waliagana na Matokeo usiku, na kumfungulia mlango alfajiri. Wakiwa bado kwenye dimbwi la mawazo, yalikuja magari mawili ya kifahari yenye vioo vyeusi. Shida na Bela walinyanyuka na kuchungulia dirishani na kuona watu kadhaa ndani ya gari. Halafu waliona Matokeo akishuka na kuwaacha wale watu wengine kwenye gari. Matokeo alimwita Bela kwa sauti ya juu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Bela aliitika huku akiwa anamfuata kutaka kujua kuna nini? Alimwambia abadilishe nguo wakaoshe macho kidogo mjini.

"Twende nikakuoneshe jiji mdogo wangu unakaa ndani tu kama filigisi," Matokeo alimwambia Bela. Uso wake ulijaa bashasha na shauku kubwa. Alikuwa na haraka kama kuku anayetaka kutaga. "Hujaenda tu kubadili nguo?" Matokeo alisema huku akimkodolea macho Bela ambaye alikuwa bado amesimama mbele ya Matokeo. Bela alimtazama Shida machoni na kumkonyeza ishara ya kufurahi kutoka na Matokeo. Shida alimwonea huruma Bela maana hakuwa anaelewa kinachoendelea.

Aliingia ndani akatafuta haraka haraka nguo aliyoona ina afadhali kidogo kuivaa mbele za watu. Hakuwa amenunuliwa nguo mpya toka afike kwa Matokeo, alivaa mojawapo ya zile alizotoka nazo kijijini. Alitoka nje haraka, alikuwa na shauku kubwa ya kuliona hilo jiji. Kiwewe cha kuingia kwenye gari zuri kilimfanya asahau hata kumpungia mkono Shida. Aliingia kwenye gari, gari likawashwa moto wakaondoka, ilikuwa ni majira ya saa kumi na moja jioni hivi.

Shida alicheka kimoyomoyo, kwani alijua yote yanayoenda kutendeka. Alitamani amwambie Bela, ila alijisemea kimoyomoyo kuwa utamu wa ngoma uingie ucheze. Nimekuwa nikiwaeleza kila siku hawaniamini, acha akajionee kwa macho. Shida alijilaza kitandani na kuendelea kuwaza na kuwazua juu ya maisha yake.

Ndani ya gari Bela alikuta kuna wasichana na wavulana wengine waliovalia maridadi. Safari iliendelea bila yeye kujua walikoelekea. Alikuwa mpole, muda mwingi akichungulia majengo dirishani. Walipita makutano ya Moroko, wakaingilia mitaa ya ubalozi wa Marekani kuelekea Masaki. Huko walifika kwenye moja ya klabu maarufu jijini Dar es Salaam iitwayo *Tanzanite One* ambako kila siku wasanii hukutana hapo na watu mashuhuri jijini.

Alishangaa kuona gari linasimama na wao kuingia kwenye jengo hilo kubwa, ambalo lilikuwa ni jengo la kifahari lenye kila kitu ndani. Kulikuwa na sehemu ya kuogelea na michezo mingi mbalimbali. Mle ndani kulitandazwa kila aina ya vinywaji; vingi alikuwa hajawahi kuviona tangu azaliwe. Waliingia wawili wawili, kila mtu akiwa na mpenzi wake, isipokuwa Bela. Walianza kuzifakamia pombe huku wakitaniana. Kila mmoja alionekana kuwa na furaha sana, Bela ambaye alishangaa kila kitu, alionekana mgeni wa kila



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 108 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kilichokuwa kinaendelea pale. Wakati wenzake wakikata vinywaji vya kila aina, Bela alibugia soda, alizinywa kwa pupa hadi alikinai. Alitia huruma kwa jinsi alivyoonekana mgeni wa maisha ya mjini.

Matokeo na wenzake waliendelea kunywa na kucheza kwa muda mrefu. Ilipofika majira ya saa sita usiku walianza kuondoka wawiliwawili kama walivyoingia, akabaki Matokeo, mzee Kisuda, Bela, pamoja na Ben ambaye alikuwa karibu na Bela muda wote. Matokeo alinyanyuka na kumkonyeza Ben, kisha Ben akatoa noti kadhaa za msimbazi na kumkabidhi Matokeo. Matokeo alimshika mzee Kisuda mkono na kuondoka naye, huku wakiwa wanayumbayumba kutokana na pombe kuwakolea. Bela akanyanyuka alipokuwa amekaa na kuanza kuondoka. Matokeo akamwambia, "Usinifuate, utapelekwa nyumbani na Ben." Bela alibaki ameduwaa. Kila kilichokuwa kinatokea tangu walipotoka nyumbani kilikuwa ni kitendawili kwake. "Ama kweli ukistaajabu ya Musa, utaona ya Firauni," alijisemea kimyakimya.

Ben alishika bilauri, akamiminia kinywaji chote kilichokuwa kwenye hiyo bilauri kinywani mwake, kisha akamwambia Bela waondoke. Bela alikuwa wa kwanza kupanda kwenye gari baada ya Ben kulifungua kwa mbali, alitaka kuwahi kurudi nyumbani. Ben aliendesha gari kuelekea Mikocheni ambako ndiko alikokuwa anaishi. Walifika kwa kudra za Mungu maana aliendesha gari akiwa amelewa chakari. Bela alikuwa hatambui njia, wala mitaa waliyokuwa wanapita kutokana na ugeni. Ben alisimamisha gari mbele ya nyumba yake. Alimkaribisha Bela ndani.

Mbijima (2019:36-39)

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

1. Bainisha wahusika katika kipande cha riwaya ulichokisoma.
2. Fafanua dhamira zilizojitokeza katika kipande cha riwaya ulichokisoma.
3. Kipande cha riwaya ulichokisoma, kipo katika mkondo gani?
4. Eleza kwa ufupi ujumbe uliopata katika kipande cha riwaya ulichokisoma?
5. Taja vipengele vya lugha vilivyojitokeza katika kipande cha riwaya ulichokisoma.
6. Andika hadithi uipendayo kwa kuzingatia kanuni na taratibu za utunzi wa Riwaya. Hadithi iwe na maneno kati ya 250 – 300.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 109 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya 6.4**

Soma magazeti na vitabu mbalimbali vilivyosheheni hadithi katika maktaba ya shule yenu, kisha bainisha vipengele vya fani na maudhui kwa kila kazi.

## Zingatia

Hadithi ndefu ya kubuni yenye mawanda mapana, lugha ya kinathari, mchangamano wa visa, dhamira, wahusika wengi na matukio yaliyosukwa kimantiki huitwa riwaya. Riwaya inaweza kuwa ya masimulizi ya kubuni au ya kweli, na masimulizi hayo yanaweza kumhusu mtu mmoja au watu wengi. Wakati mwingine, mwandishi huandika visa kwa kutumia wanyama au viumbe wengine wanaobebeshwa uhusika wa binadamu. Wahusika hawa hupewa sifa na tabia za binadamu. Mifano ya riwaya za Kiswahili ni *Joka la Mdimu* (2007), *Mama Ntilie* (2002), *Takadini* (2004), *Mtenda Hutendwa* (2019) na nyingine.

Riwaya hupambanuliwa kwa kutumia mikondo. Mikondo ya riwaya ni mwelekeo ambao mwandishi anaufuata katika utunzi wa kazi yake ya kifasihi. Ifuatayo ni mikondo ya riwaya ambayo mwandishi huitumia katika utunzi wa Riwaya:

Mkondo wa kiwasifu, huhusu hadithi zinazosimulia maisha ya watu au mtu kutoka kuzaliwa kwake hadi wakati anapoandika riwaya hiyo, mfano, Riwaya ya *Wasifu wa Sitti binti Saad* (1991).

Mkondo wa kitawasifu husimulia maisha ya mtu binafsi yaani mwandishi mwenyewe, mfano, Riwaya ya *Maisha yangu baada ya Miaka Hamsini* (2003).

Mkondo wa kipelelezi huzungumzia upelelezi wa uhalifu fulani kama vile ujambazi, wizi, rushwa, na mauaji, mfano, *Riwaya ya Njama* (1986).

Mkondo wa kihistoria huhusu matukio ya kweli ya kihistoria yaliyowahi kutokea. Matukio kama vile Vita vya Idd Amin Dadah wa Uganda dhidi ya Tanzania. Mfano Riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* (1934) na Riwaya ya *Zawadi ya Ushindi* (1992).

Mkondo wa kijasusi huhusu hadithi ya upelelezi wa ngazi ya kimataifa au ujasusi ambao unahatarisha maisha na maslahi ya taifa fulani, kwa mfano, Riwaya ya *Kufa na Kupona* (1976); Riwaya ya *Njama* (1986) na Riwaya ya *Kikosi cha Kisasi* (1979).

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


Mkondo wa kimapenzi (mahaba) huzungumzia masuala ya mapenzi ya wazi kati ya mwanamke na mwanaume, mfano, Riwaya za: *Rosa Mistika* (1971), *Barua Ndefu kama hii* (1994), *Zawadi ya Ushindi* (1992) na *Hiba ya Wivu* (1997).

## Utungaji wa tamthiliya

**Kazi ya 6.5**

**Soma sehemu ya tamthiliya ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

*(Nyumbani kwa Baba Pazi. Tweve ameingia na mama Pazi akiwa jikoni. Pazi anaonekana akitokea ndani).*



**Pazi:** Shikamoo! (*anamsalimia Tweve*)

**Tweve:** Oh! Marahaba bwana! Habari za masomo?

**Pazi:** Nzuri tu baba.

**Mama Pazi:** Basi huyo msomi wako katuletea vioja leo.
(*Akionesha kijitabu*) Kitabu hiki kimejaa matusi. Mimi nashindwa kuelewa walimu, sijui madakitari. Kutulundikia matusi shemeji.

**Tweve:** Aa (*Anakisoma*) Jihadhari na Ukimwi. Kwani kaletaje huyu mtoto?



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 111 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Baba Pazi:** Aha! Ni hivi: Pazi huko shuleni kwao walikuja waganga kueleza huu ugonjwa na wakawapa vitabu hivi. Yeye Pazi katuletea tusome……

**Mama Pazi:** Katuletea matusi huyu mwana! Sauti kutoka nje: Hodi! Hodi! Shoga nipe dawa ya jiko miye. Mama Pazi: Na wewe Mama Wini huingii, mbona hatujaona uso wako! Karibu ndani shoga.

*(Anaingia taratibu).*

**Tweve:** Jamani! Nitakuwa yule mwomba jamvi. Maana nimekuja wa kwanza lakini mwenzangu kawahi kusema. Baba Pazi kesho saa kumi ndio ule mkutano wetu wa ulinzi shirikishi. Uje bwana.

**Baba Pazi:** Ahaa! Sawa nitakuja. *(Vikombe vya chai vinagongana mezani)*

**Mama Wini:** Hamjambo wanangu?

**Pazi na Kivuko:** Hatujambo shikamoo mama Wini!

**Mama Wini:** Marahaba! Sasa shoga hiyo dawa ya jiko, himahima maana nimeishiwa bwana wee!

TET (1996:22-23) ikimnukuu Mvungi (1990).

## Maswali

1. Katika sehemu ya tamthiliya uliyoisoma, unafikiri hii ni aina gani ya tamthiliya?
2. Orodhesha wahusika waliojitokeza katika sehemu hiyo ya tamthiliya.
3. Hakiki fani iliyotumika katika sehemu ya tamthiliya uliyoisoma.
4. Kwa mifano dhahiri, onesha migogoro ndani ya sehemu ya tamthiliya, kisha pendekeza suluhisho kwa kila mgogoro.
5. Katika vikundi, jadili dhamira zilizojitokeza kwenye sehemu ya tamthiliya uliyoisoma.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya 6.6**

Katika vikundi, tunga igizo fupi kuhusu suala mojawapo mtambuka, kisha wasilisha igizo hilo darasani.

## Zingatia

Mchezo wa kuigiza unaoandikwa ili utendwe jukwaani au usomwe kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa jamii, huitwa tamthiliya. Aidha, mchezo huu huandaliwa na kutendwa kiufundi ili kuiteka hadhira. Katika tamthiliya, matendo ya kijamii huoneshwa kwa njia ya kuigiza. Tamthiliya huwa na sifa za kawaida za sanaa za maonesho ambazo ni: kusudi maalumu, waigizaji, jukwaa au mahali pa kuigizia, watazamaji (hadhira), ubunifu, mpangilio wa matukio, mtindo wa majibizano, na dhana inayotendeka. Tamthiliya ina dhima mbalimbali kama vile kuelimisha, kuburudisha, kusisimua, kuonya na kuadabisha, kuhamasisha shughuli za kimaendeleo na kutunza kumbukumbu (amali) za jamii.

Mtunzi wa tamthiliya anatakiwa azingatie mambo yafuatayo: kuchagua jambo au kisa anachotaka kuandikia, kupanga visa na matukio, kubuni wahusika sahihi, kuchagua mandhari inayofaa, kugawa matukio na kutoa maelekezo ya jukwaa kwa kila kipande cha maonesho.

## Tanzia

**Kazi ya 6.7**

Fikiria umekutana na mtu ambaye ni maarufu katika uongozi lakini kutokana na kulewa sifa, mwishowe akapata anguko au janga? Tunga kisa hicho kwa kifupi.

## Ramsa

**Kazi ya 6.8**

Chukulia wewe ni mchekeshaji katika darasa lako. Igiza mbele ya darasa na wanafunzi wenzako kuhusu kupinga ajira za watoto. (Igizo lako liwachekeshe wasikilizaji).

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 113 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya 6.9**

1. Katika vikundi, andaa tamthiliya kuhusu utanzu mmojawapo wa tamthiliya na kuiwasilisha darasani.
2. Katika tamthiliya uliyoiandaa:
   (a) Bainisha wahusika na wasifu wao.
   (b) Eleza mandhari yake.
   (c) Fafanua maudhui yake.
   (d) Eleza kuhusu lugha iliyotumika katika tamthiliya hiyo.
3. Tamthiliya uliyoitunga ipo katika utanzu gani? Fafanua jibu lako.

**Zoezi la 6.2**

1. Tago alipewa kazi ya kutunga tamthiliya. Unafikiri aliitunga kwa kuzingatia sifa zipi?
2. Ramsa inakusaidiaje katika maisha ya kila siku?
3. Je, kuna haja ya kujifunza tamthiliya katika jamii ya sasa? Kwa nini?

## Zingatia

Tanzu ya tamthiliya yenye kusikitisha au kuhuzunisha ambayo inagusa hisia za watazamaji (hadhira) huitwa tanzia. Hadhira inayoangalia huweza kuogopeshwa na kumwonea huruma mhusika mkuu ambaye mwishowe huishia kupata janga. Mhusika huyo huwa na msimamo na tabia njema au mwenendo bora na jamii humkubali. Mfano wa tamthiliya ya tanzia ni *Orodha* (2006), *Kilio chetu* (1995) *na Mfalme Edipode* (1971).

Tanzu ya tamthiliya ambayo visa na matukio hujengwa katika kuchekesha na kufurahisha huitwa ramsa. Visa vya ramsa hujikita katika maisha na uwepo wa kifo. Hivyo, mhusika mkuu hutumia njia rahisi katika kukabiliana na maisha bila kujali njia itakayotumika ni halali au siyo halali. Mara nyingi ramsa hailaani uovu bali hukejeli ujinga wa binadamu na haioni huruma kwa wahusika wake wanapoumbuka au kuaibika. Mwisho, wahusika wakuu huibuka na mafanikio. *Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe* (1988) na *Mfalme Juha* (1971) ni mojawapo ya mfano wa tamthiliya za Ramsa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la marudio la 6

1. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

(i) Hadithi inayokuwa na wahusika wachache huitwa:
   (a) Riwaya
   (b) Tungo
   (c) Hadithi fupi
   (d) Kisa
   (e) Utenzi

(ii) Tamthiliya ambayo mwishoni wahusika wake wakuu huonesha kufanikiwa inaitwa:
   (a) Tanzia
   (b) Ramsa
   (c) Kilio chetu
   (d) Ngoswe
   (e) mikondo

(iii) Tamthiliya ipi huambatana na masikitiko pamoja na huruma?
   (a) Vichekesho
   (b) Ramsa
   (c) Ngoswe
   (d) Tanzia
   (e) Mfalme juha

(iv) Riwaya ambazo husimulia maisha ya mtu binafsi huwa katika mkondo upi?
   (a) Kihistoria
   (b) Kimapenzi
   (c) Kitawasifu
   (d) Kiwasifu
   (e) Kimaadili

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 115 9/6/21 5:54 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Oanisha maelezo ya orodha A na maneno yake katika orodha B.

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| i. Kupangilia visa na matukio katika maandishi kwa lengo la kuburudisha, kuelimisha, na kuakisi hali halisi ya jamii. | A. Riwaya |
| ii. Masimulizi ya kubuni yanayosawiri tukio, tabia, na migogoro katika maisha. | B. Utungaji |
| iii. Mambo ya kubuni yenye mawanda mapana, lugha ya kinathari mchangamano wa visa, dhamira na wahusika kadhaa. | C. Tamthiliya |
| iv. Mchezo wa kuigiza unaoandikwa ili utendwe jukwaani. | D. Hadithi |
| | E. Visa |
| | F. Masimulizi |

3. Je, unafikiri ni changamoto zipi atakazokutana nazo mwandishi endapo hatakuwa mzawa wa eneo hilo?

4. Eleza sababu za mtunzi kuielewa jamii kabla ya kuiandikia kazi ya fasihi.

5. Andika hadithi fupi kuhusu dhima za fasihi andishi.

6. Eleza mambo ya kuzingatia katika utunzi wa riwaya.

7. Eleza mambo ya kuzingatia katika utunzi wa tamthiliya.

8. Onesha uhusiano uliopo baina ya utunzi wa riwaya na tamthiliya.

9. Kuna tofauti gani kati ya utunzi wa riwaya na tamthiliya?

10. Tamthiliya yenye kusikitisha inaitwaje?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Saba

## Uandishi wa insha na matangazo

### Utangulizi

*Kuandika ni stadi inayojengwa na kutumika katika maisha ya kila siku ya mwanadamu. Sura hii inahusu uandishi wa insha na matangazo. Katika sura hii, utajifunza kuandika insha za wasifu za kisanaa na insha za hoja za kisanaa. Pia, utajifunza kuandika matangazo rasmi na yasiyo rasmi kwa kuzingatia misingi ya uandishi. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuwa mbunifu katika kuandaa matangazo kuandika vitabu na makala mbalimbali magazetini.*

### Kazi ya 7.1

**Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Kijiji cha Maringo kinajulikana sana katika kata ya Kambakwale. Kijiji hicho kilikuwa kinadumisha mila na desturi za kipekee, ukilinganisha na vijiji vingine. Watu wake hawakuchangamana na jamii yoyote katika kata hiyo, waliishi kwa kufuga na kula nyama. Wakazi wa kijiji hicho, walikuwa wakarimu sana kwa wageni. Waliweza kumkirimu kila mtu na hata mtu wasiyemjua wakiamini kuwa "Mgeni aje mwenyeji apone." Methali hiyo kwa wakazi wa kijiji hicho ilikuwa na maana kubwa sana, kama wasemavyo wahenga kuwa "Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti." Kila aliyepita kijijini hapo, ulikuwa mwisho wa maisha yake.

Siku moja, Damasi na mdogo wake walipotea njia wakiwa wanawinda ndege kwa ajili ya kitoweo cha jioni. Ghafla, ndege mkubwa mithili ya tai alionekana

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 117 9/6/21 5:55 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

akinyiririka karibu yao. Nao bila kujua hili wala lile, walijikuta wakimfuatilia ndege huyo wakiamini watapata kitoweo cha kutosha. Hatimaye, walijikuta kwenye tundu bovu ambamo waliwekwa chini ya ulinzi. Hilo lilikuwa pango kubwa, nao walijikuta wameingia humo. Siku hiyo, Damasi aliogopa sana kwani ilikuwa mara yake ya kwanza kukutana na mkasa kama huo. Kwa vile alikuwa kijana shujaa, alipiga moyo konde na kumwonesha ishara mdogo wake kuwa atapigana kiume ili waokoke. Damasi alikuwa kijana mrefu kiasi, jasiri na mwenye hekima.

Akiwa amezama kwenye dimbwi la mawazo mazito, akakumbuka mbinu zote za mapambano alizojifunza kupitia kikundi chao cha Taikondo. Alijiunga na kikundi hicho akiwa Kidato cha Tatu katika shule ya sekondari ya Mjimwema. Alikumbuka jinsi alivyoweza kukwea ukuta mithili ya nyoka akweavyo mtini, pamoja na kuviringika kama mpira kukwepa mikuki na mishale iliyokuwa inarushwa mazoezini. Tena alikumbuka jinsi alivyomwokoa bibi Chausiku alipovamiwa na chui mla watu. Kutokana na ujuzi huo, kukosa silaha ilikuwa si kisingizio cha kushindwa kwani aliweza kutumia mwili wake uliojengeka mithili ya mbogo aliyejaza kifua tayari kukabiliana na adui.

Usiku ule, Damasi alimfundisha mdogo wake namna watakavyojiokoa. Kupitia tundu dogo alilotoboa, waliweza kupata walau hewa. Usingizi wao ulipaa kwa vile walishasikia habari na tabia za watu wa kijiji hicho. Hivyo, kila kishindo kilichosikika nje, Damasi na mdogo wake walijitayarisha kwa mapambano.

Jogoo wa kwanza alipowika, wale maadui waliingia kwa kushtukiza katika chumba hicho, wakiwa wameshika sime na panga tayari kwa kupata kitoweo. Damasi alimpa mdogo wake ishara ya mapambano. Panga la kwanza liliporushwa, Damasi alibonyea chini na panga la adui lilipitiliza na kuikatilia mbali shingo ya adui mwenzake. Katika mapambano hayo, Damasi alifanikiwa kumdondosha chini kiongozi wa maadui wake na kumjeruhi vibaya kwa lile panga lililopitiliza. Mdogo wake naye alishika silaha nyingine kuendeleza mapambano. Wote wawili walijibanza nyuma ya mlango kuangalia endapo kutatokea mtu yeyote.

Walijaribu kutoka nje ili watoroke, mara Damasi akaona mshale ukitokea upande wa pili, kwa ustadi alijiviringisha kumsukuma mdogo wake ili asidhurike. Walitumia mbinu ya kijeshi ya kutambaa kwa tumbo. Damasi na mdogo wake walipambana kufa na kupona ili kuokoa maisha yao. Walipambana mpaka kulipokucha na kuwashinda maadui wao.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 118 9/6/21 5:55 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mpaka kufikia asubuhi, maadui wengi walikuwa wamelala kwa majeraha na wengine walikuwa wamekwishakufa. Toka siku hiyo, hakuna unyama tena ulioendelea katika kijiji hicho. Damasi na mdogo wake wakaitwa mashujaa wa kijiji cha Maringo na hata katika vijiji vya jirani katika kata ya Kambakwale.

## Maswali

1. Katika kifungu cha habari ulichokisoma, Damasi alikuwa kijana wa namna gani?
2. Bainisha lugha ya kisanaa iliyotumika katika kifungu cha habari.
3. Unafikiri ndege mkubwa alikuwa wa heri kwa Damasi na mdogo wake? Kwa nini?
4. Eleza maana ya methali hii "Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti" kama ilivyotumika katika kifungu cha habari ulichokisoma.
5. Eleza mambo matano uliyojifunza kutokana na kifungu cha habari hiyo.
6. Pendekeza kichwa cha kifungu cha habari ulichokisoma.

## Uandishi wa insha

### Insha ya wasifu ya kisanaa

**Kazi ya 7.2**

Chunguza kwa makini mazingira ya shule yako, kisha andika insha ya wasifu ya kisanaa kuhusu mazingira ya shule hiyo.

**Kazi ya 7.3**

**Soma insha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**PAKA NA BINADAMU**

Katika kuimarisha maisha yao, wanyama hujenga uhusiano wa wao kwa wao na wa wao na binadamu. Binadamu huwatumia wanyama hao kwa shughuli kadha wa kadha, kwa mfano, utumbuizaji wa nyimbo na wengine kwa ajili ya



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 119 9/6/21 5:55 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

utunzaji wa muda. Wanyama wengine wana jukumu la kuleta burudani kwa binadamu kama vile gwaride, nyimbo, ngoma na vichekesho. Kutokana na mwenendo wake, Paka ni mmoja wa wanyama wenye urafiki na binadamu. Binadamu amekuwa akimwamini na kumpa kiti cha kushughulikia mambo mengi ofisini mwake.

Sauti nyororo isikikayo mithili ya kinanda humpatia Paka upekee wa ajabu. Akimwona mgeni huimba kwa sauti nyororo, nyau! nyaau! nyaaau! nyaaaau! Mlio wake hupendwa na kila mtu ndani ya familia. Sauti yake ni ulinzi wa kutosha dhidi ya wapangaji wasio rasmi, wanaosumbua na kudokoa vitu vya binadamu.

Rangi nzuri inayovutia pamoja na macho yake kama gololi ni baadhi ya sifa zinazompa upekee. Paka ni doli na kitulizo murua cha watoto dhidi ya maadui wao. Kiumbe huyo huficha kucha zake vizuri ili zisimdhuru mtoto aliyembeba. Adabu hii amefundishwa na mama yake, ndiyo maana wahenga wanasema, "Samaki mkunje angali mbichi."

Paka wetu ni mwaminifu na mlinzi bora, kwake udokozi ni mwiko. Hana tabia ya kula chakula isipokuwa anapowekewa kwenye chombo maalumu. Chakula chake ni maziwa, michuzi na mifupa ya samaki.

Paka amekirimiwa weledi wa kijasusi. Huweza kuwapigisha kwata maadui aliowateka. Hawa ni wale wenye mipango ya kumpora binadamu. Paka huwaona, kisha hutembea kwa kunyata taa! taa! taa! taa! huwarukia na kuwakamata. Paka awapo vitani, ni nadra kupata ngeu kisogoni. Ni jasiri ajabu! Asikiapo mlio wa nyoka siii! siiii! siiii! Hujipanga haraka kwa ajili ya kumdaka mithili ya golikipa.

Siku moja, tulisikia vurugu kali darini, kumbe alikuwa nyoka aliyekuwa akipambana na paka. Paka alifanikiwa kumuua nyoka mkubwa na kushuka naye kutoka darini. Usalama wa mali zetu upo mikononi mwa paka. Paka ana mbinu nyingi za kumdhibiti rafiki yake aitwaye Panya. Wakati mwingine humwimbia nyimbo kama vile:
"Njoo tule nyama, njoo ×2 nyama hiyooo! Kimbiaaa! Njoo tufurahi."

Paka hutumia mbinu hizo kuwahadaha panya na hatimaye kuwakamata. Mali zetu ambazo ni nguo, vitabu, daftari na viatu, vina usalama wa kutosha kutokana na uwapo wa paka.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 120 9/6/21 5:55 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Paka hukwea miti kwa maringo mithili ya kinyonga afukuzaye mawindo. Hapa hunoa mikuki yake tayari kwa mawindo na maadui. Wakati wa burudani, hufanya mazoezi ya kupanda juu ya miti mirefu.

Ninawashauri watu wasiwadhuru paka, badala yake wawajali na kuwapatia mahitaji yao kama vile: mchuzi, maziwa, nyama na maji. Paka ni mfalme kwa watu wenye busara ya kujali viumbe. Urafiki wa mwanadamu na paka unapaswa kuwa wa kudumu. Wanyama wengine hawana budi kuiga matendo ya paka kwa binadamu.

## Maswali

1. Toa wazo kuu la insha uliyoisoma.
2. Katika insha uliyoisoma hitimisho ni lipi?
3. Mambo yapi yamezingatiwa katika uandishi wa insha uliyoisoma?
4. Eleza ni kwa nini insha uliyoisoma huitwa insha ya wasifu ya kisanaa?

## Insha ya hoja ya kisanaa

### Kazi ya 7.4

Jumbi hakuhudhuria darasani kwa siku tatu mfululizo. Abdalla aliamua kwenda nyumbani kwao, kujua kinachoendelea. Alipofika, alimkuta mama yake Jumbi ni mgonjwa mahututi. Baada ya wiki moja, Jumbi alirejea dasarani. Mwalimu alitaka kumpatia adhabu ya kuwa mtoro.

FOR ONLINE USE ONLY

## Swali

Chukua nafasi ya Abdalla uandike insha yenye maneno yasiyozidi 250 na yasiyopungua 200, ili kumtetea Jumbi asiadhibiwe.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya 7.5**

**Soma insha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

## UFUGAJI WA NYUKI

Nyuki ni miongoni mwa viumbe waliopo duniani kwa manufaa ya binadamu. Nyuki hupatikana katika kundi la wadudu. Wadudu wengine katika kundi hilo ni panzi, nzi, mende, mbu na wengineo. Nyuki ni rafiki kipenzi wa binadamu kutokana na uhusiano wao wa muda mrefu. Nyuki huleta faida mbalimbali katika maisha ya binadamu.

Kwanza, uchavushaji wa maua ni moja ya faida zinazotokana na nyuki. Binadamu hupanda mimea shambani bila kuwa na uwezo wa kuchavusha mimea hiyo. Kazi hii hufanywa na nyuki. Viumbe hawa huweza kuhamisha chavua na kuzipeleka sehemu za kike za ua. Mazao ya mimea hufanikishwa kutokana na shughuli mbalimbali za nyuki.

Pili, nyuki hutengeneza asali na nta. Kutokana na uhodari wao, wadudu hawa huweza kutalii mamilioni ya maua kukusanya malighafi za kutengenezea asali na nta. Wanapokuwa kazini, wadudu hawa hufanya kazi kama vichaa, kwani utawaona wakizurura kwenye majalala ya takataka na mifereji ya maji kukusanya malighafi. Wadudu hawa huchakata taka na chavua kutoa asali na nta. Ukiitazama asali na nta hiyo, huwezi kuamini kama imetokana na malighafi hizo, kweli wahenga walisema "Ukiona vyaelea vimeundwa." Asali na nta huwapatia binadamu fedha. Fedha hizo huzitumia kununulia mahitaji mbalimbali kama vile chakula, mavazi na malazi. Pia, asali hiyo hutumika kama tiba ya magonjwa mbalimbali kwa jamii nyingi duniani. Nta nayo hutumika kama malighafi viwandani, kwa mfano, kutengeneza gundi ambayo hutumika kutengeneza viatu, mikoba na vitu vingine vya thamani. Pia, nta hutumika kutengeneza mishumaa.

Hakuna kizuri kisichokuwa na kasoro. Licha ya kuwa na faida, nyuki huweza kusababisha madhara kwa binadamu na mifugo. Wadudu hawa huwa na hasira kama morani. Nyuki huweza kuwashambulia maadui wao, binadamu na mifugo kama jeshi lishambuliavyo maadui kutoka pande zote. Mashambulizi ya nyuki huweza kusababisha vifo kwa maadui wao. Aidha, utengenezaji wa mizinga ya nyuki huchangia uharibifu wa mazingira kutokana na ukataji miti kwa ajili ya kutengenezea mizinga.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 122 9/6/21 5:55 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Pamoja na kwamba nyuki huweza kuleta hasara, hatuna budi kuwafuga na kuwapenda, kwani manufaa yao ni makubwa kuliko hasara. Ufugaji wa nyuki huleta heshima kubwa kwa familia, jamii na taifa. Tahadhari kubwa inapaswa kuchukuliwa kulinda usalama wa maisha ya watu na mifugo.

## Maswali

1. Insha uliyoisoma imegawanyika katika sehemu ngapi?
2. Insha uliyoisoma ni ya aina gani? Kwa nini?
3. Pendekeza kichwa kingine kinachofaa cha insha uliyoisoma.

### Zingatia

Uandishi wa insha huzingatia yafuatayo: kuwa na wazo au mada ya kuandikia; dondoo au hoja zinazonyumbua mada; kupangilia insha katika vipengele vinne muhimu (kichwa, utangulizi, kiini na hitimisho); kuzingatia matumizi sahihi ya viakifishi; kuandika utangulizi mzuri unaotambulisha mada; kupangilia hoja katika mtiririko wa aya kutegemeana na uzito wa hoja; kuthibitisha hoja kwa mifano, lugha fasaha na sanifu; hitimisho zuri kwa kutoa maoni, mapendekezo au suluhisho; muumano wa hoja na kuzingatia usafi wa kazi kwa kuepuka kufutafuta.

Insha ya hoja ya kisanaa huandikwa kwa kujenga hoja zenye uzito, sambamba na mifano ya kuthibitisha hoja hizo.

FOR ONLINE USE ONLY

### Zoezi la 7.1

1. Chagua mada uipendayo, kisha uiandikie insha ya wasifu ya kisanaa. Maneno yasipungue 250 na yasizidi 300.
2. Andika insha ya hoja ya kisanaa yenye maneno yasiyopungua 250 na yasiyozidi 300 kuhusu mada mojawapo ya hizi zifuatazo:

   UKIMWI, unyanyasaji wa watoto, au watoto waishio katika mazingira magumu.


## Uandishi wa matangazo

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kazi ya 7.6

**Chunguza michoro ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

1.



2.



FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Maswali**

1. Umebaini nini katika michoro hiyo?
2. Michoro hiyo inakusaidiaje katika maisha ya kila siku?
3. Bainisha matumizi ya alama za usalama barabarani katika mchoro namba 1.
4. Bainisha matumizi ya kila alama ya barabarani katika michoro namba 2.

## Wiki ya usalama barabarani

**Kazi ya 7.7**

**Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Shule yetu ipo katikati ya Jiji la Mwanza. Siku moja tulipokuwa darasani, tulisikia kelele za nyimbo na ngoma zikitumbuiza. Wanafunzi wote tulikuwa na shauku ya kufahamu nje kuna nini. Kumbe! yalikuwa maadhimisho ya wiki ya usalama barabarani. Wanafunzi wa Kidato cha Pili waliteuliwa kushiriki kilele cha siku hiyo. Maandamano yalipambwa na nyimbo, tarumbeta na ngoma zilizoamsha ari ya watu kutaka kujua kinachoendelea. Maandamano yaliishia katika viwanja vya CCM Kirumba ambapo mgeni rasmi alikuwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

Vikundi mbalimbali vilitumbuiza nyimbo za kuisifia serikali na jitihada za Jeshi la Polisi kuwaelimisha wananchi kuhusu sheria mbalimbali za usalama barabarani. Madereva nao walionesha mbwembwe kwa kuingia na magari yaliyosheheni mabango yaliyoandikwa, "kuwa mstari wa mbele kukemea ajali za barabarani."

Wanafunzi wa shule mbalimbali walitia fora, kwani walionekana wachangamfu na walikuwa wamebeba mabango mbalimbali ya usalama barabarani. Kikundi cha shule yetu kilighani ngonjera iliyosisimua kadamnasi hiyo. Pia, kulikuwa na igizo murua lililowaliza baadhi ya watu waliohudhuria siku hiyo.

Hotuba ya mgeni rasmi ilianza kwa kuwaasa madereva kuwa makini wawapo barabarani, kwani uhai wa watu uko mikononi mwao. Iliendelea kusema kuwa, madereva walevi au wasiozingatia sheria za usalama barabarani na kusababisha ajali wachukuliwe hatua kali ili iwe funzo kwa madereva wengine wasiozingatia sheria hizo. Aidha, Waziri alilipongeza Jeshi la Polisi kusimama

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kidete na kuwaelimisha wananchi kuhusu sheria za usalama barabarani. Pia, aliwasihi wasichoke kutoa elimu ya mara kwa mara kwa madereva na wananchi kupitia vyombo vya habari na matangazo mbalimbali.

Mwisho, aliwasihi wananchi kuwa macho wanapotembea au kutaka kuvuka barabara kuzingatia alama za barabarani. Kwa ujumla, siku hiyo ilimvutia kila aliyeshiriki.

## Maswali

1. Je, unafikiri ni mabango gani yalibebwa na wanafunzi? Taja matatu.
2. Unafikiri siku hiyo uwanja wa CCM Kirumba ulisheheni mabango gani? Taja matano.
3. Ungekuwa wewe, ungeandaa bango lipi kwa ajili ya wiki ya usalama barabarani?
4. Je, shuleni kwenu kuna matangazo yapi?

### Kazi ya 7.8

Tengeneza bango au tangazo moja kuhusu usalama barabarani.

### Kazi ya 7.9

Chunguza matangazo yafuatayo, kisha andika sifa za kila tangazo.

**Tangazo A**




FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Tangazo B**




**Tangazo C**

## HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

CITY OF DAR ES SALAAM

BANDARI YA SALAMA

### TANGAZO

**WANANCHI WOTE WA JIJI LA DAR ES SALAAM, MNAARIFIWA KUWA, KUTAKUWA NA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI LA HALMASHAURI YA JIJI, UTAKAOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA KARIMJEE SIKU YA JUMANNE, TAREHE 05 MEI 2020 KUANZIA SAA NNE KAMILI (4:00) ASUBUHI KWA AJILI YA KUJADILI TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KILA SIKU NA ZA MIRADI YA MAENDELEO KWA ROBO YA TATU (JANUARI-MACHI) YA MWAKA WA FEDHA 2019/2020.**

**N.B: TAFADHALI UPATAPO UJUMBE HUU, MJULISHE NA MWINGINE KWA UFAHAMU.**

**UTAWALA**

**29 APRILI 2020**

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Ainisha sifa za matangazo uliyopewa yenye herufi A, B, na C.
2. Eleza ujumbe unaotolewa kwa kila tangazo.
3. Tangazo lipi linaweza kubandikwa bila kufuata utaratibu?

### Kazi ya 7.10

**Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Tangu kuzaliwa kwangu, sikuwahi kuona jiji zuri linalovutia kama lile. Ushamba wangu ulinifanya nishindwe kuvuka barabara, na kusababisha nichelewe kupata staftahi. Nikikumbuka, siku ya kwanza nilipoingia jijini, niliona taa zimejipanga kuwaangazia wapita njia ambao kwa hakika hawakujali kuwapo kwa taa hizo. Kila mtu alionekana kuwa na hamsini zake. Kadiri siku zilivyoenda, nilijaribu kupita maeneo tofautitofauti, ilimradi nijionee ndani ya jiji kuna nini. Kwa hakika, nilijuta siku hiyo, kwani msururu wa magari uliokuwa unafukuza upepo, ulinifanya nigote mithili ya mlingoti wa bendera pembeni mwa barabara. Cha ajabu, katika kutalii huko, niliona mabango ya kila aina. Mabango hayo yalibeba matangazo mbalimbali yaliyoning'inizwa kwenye milingoti, madaraja na mengine kubandikwa kwenye mawe makubwa. Matangazo hayo yaliniweka mguu sawa, kila nilipokutana nayo, niliyasoma na kuendelea na safari.

Siku hiyo, jua lilikuwa kali sana. Nilikaribia kwenye mti mmoja ili angalau nitulize nafsi kwa kuuzimua mwili ambao ulikuwa unachemka kama uji kwenye sufuria. Kumbe! chini ya mti huo, kulikuwa na jiwe kubwa lililonifanya nifurahie kuketi juu yake. Nilipolisogelea, nilishangaa kuona tangazo murua lililoandikwa kiustadi na kuwekwa mahali hapo. Kama ilivyo ada, nilisoma ujumbe uliokuwapo, nikagundua kuwa, siruhusiwi kukalia jiwe hilo, endapo sitakuwa na pesa ya kulipia. Kwa uchovu huo niliokuwa nao, nilijikuta nimekaa chini huku kichwa kikiwa kimebebwa na jiwe hilo.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mjini kuna mambo! Asubuhi moja, nilijihimu kwenda mjini kutafuta kibarua. Kama ilivyo ada, kuuliza si ujinga, na aulizaye ataka kujua. Nilimsogelea jamaa mmoja ili nimuulize kama kuna uwezekano wa kupata kazi. Bila majibu alinyoosha kidole chake akaelekeza kwenye mti ambako kulikuwa na bango dogo lililosomeka "kuuliza shilingi 500/=, na kupelekwa shilingi 1000/=." Nilishikwa na bumbuazi kutokana na bango hilo. Kwa kuwa sikuwa na pesa, ilinibidi niendelee na safari. Nilirudi jioni, nikiwa nimechoka bila mafanikio. Nilijitupa kitandani, nikitafakari usemi usemao, "mjini shule."

Wiki iliyofuata sikukata tamaa, mdogomdogo, nilishika njia kutoka Buguruni kuelekea Kariakoo. Nilifika kwenye ofisi moja ambayo nilisalimia, kisha nikauliza kama nitaweza kupata kazi yoyote pale. Dada huyo alinishangaa, akaniuliza "unajua kusoma?" Nikamjibu "ndiyo." "Hebu angalia hapo mlangoni, hujaona tangazo?" Niliinua macho yangu, nikaona pameandikwa "hapa hakuna kazi." Polepole, niliondoka na kushika njia kuelekea eneo lingine.

Katika pitapita zangu huku na huko, mara nikasikia kelele za matangazo kwenye kipazasauti. Nilisimama kusikiliza kwa makini kinachotangazwa. Kumbe kulikuwa na gari la matangazo ya bendi kubwa, itakayotumbuiza katika viwanja vya Keko Barafu. Mtangazaji huyo, alikuwa na sauti ya kumtoa nyoka pangoni. Nilipofika Kariakoo, nilistaajabu mno. Niliona matangazo ya kila namna yamewekwa pembezoni mwa barabara, juu ya milango na hata katikati ya barabara kutoka upande mmoja kuelekea mwingine. Ama kweli! Tembea uone!

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

1. Kulingana na mwandishi ni mahali gani panafaa kuweka matangazo?
2. Je, shuleni au mtaani kwenu, matangazo hubandikwa wapi?
3. Umejifunza nini katika kifungu hiki cha habari?
4. Unafikiri ni mahali gani pengine sahihi panapofaa kuwekwa matangazo, mbali na mahali palipotajwa katika kifungu cha habari ulichokisoma?
5. Vyombo gani vya habari hutoa matangazo?



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 129 9/6/21 5:55 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Zingatia

Katika uandishi wa matangazo, huna budi kuzingatia mambo yafuatayo: Kichwa cha tangazo kibebe kiini cha tangazo; anwani au mawasiliano; matumizi ya picha, michoro na vielelezo; matumizi ya rangi katika michoro au maandishi; mwonekano mzuri wa picha na michoro; mahali sahihi pa kutolea au kubandika tangazo; na lugha yenye ushawishi. Vilevile, liwe fupi na la kueleweka; lugha fasaha na yenye mvuto kwa msomaji; na lijitosheleze kimaudhui.

## Matangazo rasmi na yasiyo rasmi

**Kazi ya 7.11**

Tembelea mbao za matangazo katika shule yako, kisha bainisha tofauti ya matangazo utakayoyakuta.

**Zoezi la 7.2**

**Chunguza mifano ya matangazo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Tangazo A**

**KUMEKUCHA BUCHA**

**PATA NYAMA YA NG'OMBE NA MBUZI, NA KUKU, NA SAMAKI AINA ZOTE KWA BEI NAFUU YA SAIZI YAKO**

**KARIBUNI SANA**

**0245567890**

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 130 9/6/21 5:55 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Tangazo B**

**TANGAZO** TCAA

**MAMLAKA YA USAFIRI WA ANGA TANZANIA (MUATA)**

**MAMLAKA YA USAFIRI WA ANGA TANZANIA INAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA, KUANZIA TAREHE 25 MACHI 2020, KUTAKUWA NA SAFARI ZA NDEGE ZETU KATIKA MIKOA YOTE YA TANZANIA. WAHI TIKETI USAFIRI NI WA UHAKIKA NA WA HARAKA.**

**IMETOLEWA NA MKURUGENZI**

**MAMLAKA YA USAFIRI WA ANGA TANZANIA.**

## Maswali

1. Bainisha aina za matangazo uliyoyachunguza.
2. Eleza sifa za tangazo za A na B.
3. Tangazo lipi limezingatia sifa za matangazo?

## Kazi ya 7.12

1. Andika matangazo mawilimawili yanayotoa taarifa za: Ilani, biashara, na maelekezo.
2. Tembelea maeneo mbalimbali, chunguza matangazo yaliyotolewa, kisha onesha ubora na upungufu wa kila tangazo.
3. Andika tangazo linaloonesha mabadiliko ya siku ya kufungua shule utakalotuma kwenye vyombo vya habari.
4. Andaa bango kuhusu mahafali ya shule yako.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zingatia

Matangazo yasiyo rasmi hutolewa bila kufuata taratibu za mamlaka zinazohusika. Baadhi ya matangazo hayo ni mabango yanayobandikwa kwenye nyumba za watu au maduka bila kibali maalumu, mabango ya tiba za asili yasiyokuwa na kibali maalumu na matangazo ya shughuli binafsi za mtu. Mara nyingi matangazo ya aina hii hutolewa kupitia maandishi, ngoma, kengele, pembe ya mnyama, na vipaza sauti.

Matangazo rasmi hutolewa baada ya kuratibiwa na mamlaka inayohusika na kupewa idhini ya kuufikia umma. Matangazo hayo hayatolewi kiholela bali hufuata taratibu maalumu kabla ya kuidhinishwa. Mfano wa matangazo hayo ni yale yanayotolewa na serikali, mashirika ya umma, binafsi, na ya kidini.

Watu binafsi, taasisi na mashirika ya umma hutoa matangazo kwa njia ya magazeti. Matangazo ya magazetini huweza kuwa na sifa hizi: huwa na kichwa cha tangazo; hutumia lugha fasaha; huonesha kiini au kusudi; hutumia maneno machache; na ubunifu katika uandishi. Matangazo hayo huhusu mambo kadhaa, mfano: ajira, elimu, kazi, pembejeo za kilimo, michezo na mengine mengi.

FOR ONLINE USE ONLY

### Zoezi la marudio la 7

1. Jibu maswali yafuatayo:

    (i) Eleza kwa mifano mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha.

    (ii) Andika insha yenye maneno yasiyozidi 150, inayohusu "siku ambayo hutaisahau."

    (iii) Fikiria unataka kuanzisha biashara ndogondogo, andika bango la kutambulisha biashara yako.

    (iv) Taja vigezo vitano katika kuandika tangazo rasmi.

    (v) Orodhesha mifano ya matangazo ambayo si rasmi.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 132 9/6/21 5:55 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(vi) Tangazo la kupeleka gazetini linatakiwa liwe na sifa zipi?

(vii) Fikiria kwenye kijiji chenu kuna uhaba wa maji unaotokana na ukataji wa miti. Andika insha kuwahamasisha wananchi "kuhusu utunzaji wa miti."

(viii) Bainisha aina za matangazo.

2. Oanisha maelezo ya sehemu A na maneno ya sehemu B.

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| i. _________ ni moja ya vigezo vya uandishi wa tangazo rasmi. | A. Hutolewa kiholela bila kupitia mamlaka zinazohusika. |
| ii _______________ ni sifa ya matangazo yasiyo rasmi. | B. Insha |
| iii. ______________ ni mojawapo ya vigezo vya uandishi wa insha ya kisanaa. | C. Mstari bahari |
| | D. Tangazo |
| iv. ___________ huandikwa kwa mtiririko wa mawazo yaliyo katika mpangilio wa aya. | E. Liwe fupi na la kueleweka |
| | F. Huratibiwa na kuhaririwa kabla ya kuufikia umma |
| v. __________ ni moja ya sifa za uandishi wa matangazo. | G. Sanaa |

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 133 9/6/21 5:55 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nane

## Ufahamu na ufupisho

**Utangulizi**

*Ufahamu na ufupisho ni miongoni mwa vipengele muhimu katika ujifunzaji wa lugha. Katika sura hii, utajifunza kusoma na kufupisha habari bila kupotosha ujumbe. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kusoma kwa uelewa, kufupisha habari, kuandika matini na kuwasilisha taarifa mbalimbali katika maisha ya kila siku.*

### Kusoma kwa ufahamu

### Ufahamu: 1

**Kazi ya 8.1**

**Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

1. Fahari ya kila mtu, kwanza taifa lake,
Ataingia misitu, na bahari azivuke,
Kutimiza wake utu, afe ama aokoke,
Pasipo hofu ya kitu, halipendi liondoke.

2. Fahari ya kila mtu, ya pili ni nchi yake,
Mtu hakubali katu, kutawaliwa pake,
Hilo haliwi kuntu, halina heshima kwake,
Pasipo hofu ya kitu, halipendi liondoke.

3. Fahari ya kila mtu, ya tatu ni nchi yake,
Kuwaye chini ya watu, wageni wa nchi yake,
Ni jambo gumu kwa mtu, japo vipi aridhike,
Pasipo hofu ya kitu, halipendi liondoke.

Haya ni maneno ya Shaaban Robert, gwiji wa ushairi na fasihi nchini, hasa zama hizi za ukoloni mamboleo na utandawazi unaoangamiza mataifa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kusalimika kwa nchi kunataka kiongozi mzalendo mwenye kujitoa asiye mamluki wala wakala wa ubepari na ubeberu wa kimataifa. Asiwe kiongozi mwenye kukaribisha ukoloni mamboleo, mahusiano hasi ya kimataifa na uwekezaji wa kigeni wenye kupora rasilimali za taifa, demokrasia na kuihujumu nchi. Ukiacha utawala wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na pengine utawala wa awamu ya tano…, Kwa maneno ya mwalimu Nyerere, tulimeza kila kitu cha kigeni kama dodoki na kwa kupagawa na "usasa" wenye sumu.

Mara nyingi imenipa taabu sana kufikiri kwamba, viongozi na wasomi wetu wa Elimu ya Chuo Kikuu ambao kwa somo la Elimu ya Maendeleo lilikuwa la lazima juu ya masomo yote kama nyenzo ya kuwawezesha kuichambua dunia ya migongano, wameweza kuruhusu kirahisi haya kutokea!

Sasa naanza kupata jibu kwamba, walikosa uzalendo na ujasiri ambao Rais wa awamu ya tano, alielekea kuufufua. Yeye alijikita kwa watu wake badala ya kurandaranda nje; hakuuza sura wala nchi ili kujitafutia umaarufu bandia kimataifa, bali alipanga maendeleo kwa ustawi wa nchi. Kwake, ni nchi ya watu kwanza, "mdundiko" na anasa za kimataifa baadaye.

Nchi tajiri zimetushauri tuchukue mfumo wa maendeleo kwa kufuata njia zilizopitia zikafanikiwa "kuushinda" umasikini; nasi… tumekubali kumeza ndoano na chambo bila kuhoji.

*(Joseph Mihangwa, Gazeti la RAI, Toleo Na.1441, Alhamisi, Aprili 2-8, 2020. Ukurasa 8.)*

## Maswali

1. Habari uliyoisoma inahusu nini?
2. Kwa mujibu wa habari, wanaosifiwa ni akina nani?
3. Unafikiri ni kwa nini wanasifiwa?
4. Mwandishi wa habari hii, ana mtazamo gani kwa jamii aliyoiandikia?
5. Unafikiri ni kwa nini mwandishi ameanza na beti za shairi, kisha habari?
6. Mwandishi alinukuu beti hizo kutoka wapi?
7. Unapata funzo gani kutokana na beti hizo hapo juu?
8. Kwa upande wako kama mzalendo, utaifanyia nini nchi yako ukiwa shuleni na baada ya shule?
9. Pendekeza kichwa cha habari uliyoisoma.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Ufahamu: 2

### Kazi ya 8.2

**Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Kila aliyesikia, alitamani afike, ajionee mwenyewe. Si mahali pengine bali ni katika Pori la Kebose ambapo unyonyaji na uporaji vilitawala. Hili ni pori lenye wanyama wa aina mbalimbali na wenye rangi za kuvutia. Pori hilo lilielea angani kwa kushikiliwa na nguvu za asili zilizotokana na mto mkubwa upitao katikati ya pori. Nguvu za asili zilizotokana na mkondo wa mto huo, zililipaisha angani kimo cha maili sabini kutoka usawa wa mto. Kimo hicho katu hakikubadilika, licha ya upepo mkali na tetemeko lililopita ndani ya pori. Kwa nini maili sabini? Ni swali jepesi ambalo kila mnyama alitazamia kusikia majibu mepesi. Hata hivyo, majibu yake yalitegemea majira na nyakati. Mnyama kikongwe aliyejaribu kutoa jibu kwa kubahatisha, ghafla alipaishwa na radi, kisha akashushwa na kuzamishwa mtoni.

Habari za pori hilo zilisikika masikioni mwa wengi. Wageni kutoka mapori ya mbali waliingia Kebose kama siafu mawindoni. Wanyama wa kigeni walizuru pori hilo kila mwezi wa saba kwa kuwa ndicho kilikuwa kipindi chenye uhakika wa usalama wao.

Pori la Kebose lilikuwa na mito midogo midogo iliyotokana na mto mkuu wenye mhimili uliolipaisha pori kutoka usawa wa ardhi. Maji ya mto yaliingia Kebose kinyume cha mkondo. Badala ya kuteremka, yalipanda juu mithili ya nyoka apandaye kwenye mti mrefu ili kuepuka dhoruba ya moto mkali uteketezao misitu bila huruma. Wanyama wa mapori jirani walilitamani pori la Kebose kutokana na utajiri na maajabu yake ya maji kupandisha mlimani.

Kutokana na maendeleo ya teknolojia yaliyofikiwa na wanyama kutoka pori la Ustaarabu, waliweza kuingia katika pori la Kebose kwa usafiri wa ndege zilizotoa milio mithili ya simba wenye njaa kali. Wanyama hao waliweka mifereji iliyotiririsha maji safi kutoka pori la Kebose kuelekea pori la Ustaarabu.

Mito mitatu iliyojulikana kwa majina ya Nginaro, Mesongo na Mingisi, ilitiririsha madini ya aina zote kama kimiminika kizito kuelekea kwenye mapori ya wanyama wa kigeni. Bila kusita, wanyama hao waliachama midomo na kumeza utajiri wa pori la Kebose kwa kasi ya ajabu. Unaweza kujiuliza, waliwezaje? Hili ni swali lenye jibu rahisi! Ni kwamba, walikuwapo wanyama


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mithili ya fisi lakini si fisi, vinyonga wakubwa lakini si vinyonga. Wanyama hao walibadilika sura na mitazamo kila kulipokucha. Mchana walivaa mavazi meupe na usiku mavazi meusi. Wanyama wengine walikuwa na rangi kama ya nyoka waishio kwenye minyaa.

Tangu awali, wanyama wa Kebose hawakuwa na ufahamu kuhusu msamiati wa umaskini. Kama wahenga wasemavyo, "Ukicheka na nyani utavuna mabua." Umaskini katika pori la Kebose ulianza taratibu kama wimbo wa kitoto, hatimaye, ukawa kibwagizo hata kwa wanyama wakubwa. Ombaomba wakaongezeka, ngozi za miili ya wanyama katika pori hilo zilizidi kuchakaa. Kadiri muda ulivyopita, wanafunzi walianza kunung'unikia wazazi kwa kukosa maziwa, chakula, ada, na sare za shule. Waliishiwa kiasi cha kuvaa malapulapu.

Vituo vya afya vya jamii ya wanyama katika pori la Kebose vilikosa dawa na wahudumu hawakulipwa stahiki zao kwa muda mrefu. Wanyama wenye mimba walitamani kujifungulia mapangoni kutokana na ukosefu wa huduma na vifaa kwenye vituo vya afya vya jamii hiyo. Baadhi ya wazazi katika pori hilo, walizikimbia kaya zao na watoto wakabaki kulalama.





Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 137 9/6/21 5:55 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mjukuu wa Nungunungu aitwaye Ikindya, hakufurahishwa na hali hiyo. Yeye na wanafunzi wenzake wa Kidato cha Tatu katika Shule ya Sekondari Jitambue, waliishuhudia na kuiishi adha hiyo. Walikata shauri la kuleta mabadiliko katika pori lao, punde watakapohitimu masomo. Siku zilisonga, miaka ikasogea, hatimaye majira yakawadia, wakahitimu.

Ikindya aliongea na kuweka mikakati na viongozi wa pori la Kebose. Waliitisha mkutano mkubwa sana uliowashangaza Nyani wajawazito na Ngedere vikongwe. Hakika ilikuwa patashika. Halaiki ya wanyama ilihudhuria, hoja zikawekwa mezani, mjadala ukaendelea. Wanyama wote walipata nafasi ya kuzungumza. Wote waliazimia kushikamana ili kutafuta suluhisho la pori lao.

Mkutano ulimalizika kwa matumaini makubwa. Baada ya siku chache yaliibuka makundi pinzani. Wahenga hawakukosea waliposema, "Lisemwalo lipo kama halipo linakuja." Ikindya alikumbuka maneno ya babu yake, Mzee Nungunungu kuwa, ukiona watu wanakupigia makofi, chukua tahadhari. "Si kila makofi yanaashiria kukushangilia." Babu alimwambia kwamba, kamwe asikubali kukatishwa tamaa na wanyama wachache. Daima wenye kutengeneza njia huwa ni wachache, ila wapitaji ni wengi. Ili kufikia malengo, hauna budi kupuuza vitu vya kukutoa kwenye njia sahihi.

Ikindya aliogelea ndani ya mto wa pori kinyume cha mkondo, ndani ya maji ya mto uliofurika na kutapika vyura na samaki wadogo. Watu walifurahishwa na hoja zake, na wengine walisema haiwezekani. Ikindya na wanyama wenzake wachache hawakurudi nyuma, licha ya vibaraka kufanya juu chini kuwaingiza ndani ya mdomo wa mamba. Ikindya alidhamiria kujenga jamii mpya yenye kuheshimika ndani ya pori kwa kutumia rasilimali za ndani zilizokuwa zinachukuliwa kwa mabavu.

Licha ya Ikindya kutokuwa na msaada, upepo wa asili uliipaza sauti iliyorindima na kutetemesha matumbo ya vibaraka waliojifanya marafiki wa wageni na kuwapatia tunu zetu. Ikindya aliijua siri ndogo ya pori la Kebose. Pori hilo lilikuwa na mto mdogo ulioibuka kipindi cha kiangazi na kutoweka wakati wa masika. Maji ya mto huo hayakunyweka ovyoovyo. Kila mwenye nia mbaya, aliumbuka baada ya kugusa maji ya mto huo. Ikindya alikata shauri kuwapitisha wazee katika mto huo ili kubaini vibaraka, wala rushwa na wapiga dili.

Siku ya kwanza, aliongozana na wanyama wote wa pori la Kebose kwenda mtoni kunywa maji ya heri. Ghafla, mto ulihama na eneo kubaki kavu. Hali hii ilimfanya akumbuke kwamba "Kwenye msururu wa mamba na kenge nao hawakosekani." Si wanyama wote waliokwenda mtoni walikuwa na nia thabiti na uzalendo.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 138 9/6/21 5:55 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Siku iliyofuata, waliazimia kupiga kura. Baadhi ya wanyama waliokuwa vibaraka wa adui walijidhihirisha wenyewe. Sharti la mto ule ni kwamba, hakuna mgeni aliyeruhusiwa kuonja maji yake. Siku ya tatu, wazawa wote waliteremka mtoni, walikuta maji yenye rangi mithili ya maziwa. King'ora kikapigwa, masharti yakawekwa. Kila mnyama alipaswa kupiga funda la maji kwa kutumia mkono wake.

Hapa ndipo penye hekima na uzalendo. Kila aliyewahi kuchukua au kula rushwa, kupiga dili, kuonea na kupotosha ukweli aligeuka kuwa chura. Idadi kubwa ya wanyama waligeuka kuwa vyura. Ndio maana ukienda kwenye mito na mabwawa, utakuta vyura wanalalamika na kujutia matendo yao. Vibaraka wa wageni nao bila kujua, kama kawaida yao, walivunja masharti na kuchota maji mengi kwenye majagi ili kuwazidi wenzao. Hao nao waligeuka kuwa samaki.

Hatimaye, pori zima la Kebose likabaki na wanyama sabini tu waliokuwa na uzalendo wa kweli. Hawa walishirikiana na Ikindya kuleta ukombozi wa kiuchumi, kifikra, kiroho, na kisiasa katika pori. Wanyonyaji wote walifukuzwa na mifereji iliyokuwa imewekwa kufyonza rasilimali za wazawa ikazibwa. Hapa unaweza kujiuliza, ni nani awezaye kwenda kinyume cha mkondo pale mkondo unapochafuka? Hili ndilo jibu la swali lililosumbua watu kuhusu kimo cha maili sabini.

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

1. Taja jina la pori linalosimuliwa kwenye habari uliyoisoma.
2. Orodhesha mito iliyotiririsha vimiminika vya madini katika pori la Kebose.
3. Unafikiri ni akina nani walimeza utajiri wa Kebose kwa mujibu wa habari uliyoisoma?
4. Eleza kwa ufupi, tukio lililomkuta kikongwe katika habari uliyoisoma.
5. Kauli isemayo "Kinyume cha mkondo" inamaanisha nini?
6. Mhusika mkuu katika habari hiyo ni nani?
7. Wanyama waliyapokeaje mawazo ya Ikindya na wenzake? Fafanua.
8. Kwa mawazo yako, unafikiri kuna jamii isiyokuwa na wasaliti? Kwa nini?
9. Ukiwa unaishi kwenye jamii kama ya Ikindya utafanya nini katika kutetea na kuendeleza rasilimali za jamii yako?
10. Ikiwa wewe ni kiongozi au unatarajia kuwa kiongozi, eleza hatua utakazochukua kukabiliana na vikwazo kama vya Kebose.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 139 9/6/21 5:55 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya 8.3**

1. Fupisha habari uliyoisoma kwa maneno yasiyopungua 80 na yasiyozidi 100.
2. Katika vikundi, tafuta habari au matini kuhusu masuala ya uhusiano wa kijinsia, kisha isome na kuifupisha.

## Kufupisha habari

**Kazi ya 8.4**

**Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Maendeleo katika uchumi ni muhimu kwa taifa lolote lile. Masuala ya uchumi yana nyanja nyingi ikiwa ni pamoja na elimu, utamaduni, sayansi na teknolojia. Mathalani, maendeleo ya uchumi, hayawezi kusonga mbele kama jamii ya watu wanaohusika haina maendeleo mazuri kielimu. Hali kadhalika, imani mbovu katika utamaduni wa jamii zikishamiri katika fikra za watu wake, maendeleo ya kiuchumi yataathirika. Elimu hufuta ujinga na ndiyo nguzo ya kwanza ya maendeleo. Kiswahili kimetumika na kinaendelea kutumika kama nyenzo kuu ya kuwaunganisha wananchi katika shughuli mbalimbali za kiuchumi kwa sababu lugha kuu ya Watanzania ni Kiswahili.

Ukifuatilia kwa makini historia ya Kiswahili nchini Tanzania, utaona kuwa ni lugha ambayo inakwenda sambamba na mabadiliko ya kisiasa yanayotokea nchini. Kiswahili kilikuwapo wakati wa ukoloni na kilipambana na mazingira ya wakati huo.

Baada ya kupatikana kwa uhuru, Kiswahili kiliendelea kuwapo lakini kilibadili sura kwa maana ya kukidhi jukumu lake katika Tanzania huru nchini, chini ya mfumo wa chama kimoja cha siasa. Kiswahili kinaendelea kuwa nyenzo kuu katika maendeleo ya Tanzania chini ya mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Wakati wa utawala wa kikoloni tumeona juhudi zilizokuwapo katika kuikuza lugha ya Kiswahili. Aidha, tumejadili matatizo yaliyosibu maendeleo ya lugha hii. Wakati wakoloni walipoivamia nchi yetu, walifanya kila lililowezekana kuiheshimu na kuijenga lugha ya Kiingereza katika makoloni yao.



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 140 9/6/21 5:55 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Baada ya kupata uhuru na kuwa chini ya mfumo wa chama kimoja, juhudi zaidi zilifanywa kuikuza lugha ya Kiswahili, si katika kuijenga tu bali pia katika kulihimiza taifa kuitumia na kuiheshimu kama lugha yake ya taifa na nyenzo ya kufanyia kazi.

Maendeleo ya Kiswahili nchini ni ya kutia moyo. Lugha hii sasa imeingia katika uwanja wa sayansi na teknolojia. Huu ni wakati muhimu sana katika maendeleo ya lugha hii. Kwanza, ni wakati ambapo kunahitajika kuwapo na mikakati kabambe yenye upeo wa mbali ya kuiendeleza lugha hii kitaaluma. Sayansi na teknolojia ni uwanja wa taaluma. Pili, kunahitajika kutumia utaalamu wa hali ya juu katika kuijenga lugha hii ili iweze kubeba mahitaji katika mazingira hayo. Bila hiyo hatuwezi kusonga mbele.

*(Mawazo ya Profesa G. Mhina - BAKITA, Gazeti la Uhuru la Julai 31, 92 uk. 7, Kiswahili na Vyama vingi).*

FOR ONLINE USE ONLY

## Maswali

1. Andika kichwa cha habari kinachofaa katika habari uliyoisoma.
2. Bainisha wazo kuu la habari uliyoisoma.
3. Fupisha habari hiyo kwa maneno yasiyozidi 100 na yasiyopungua 50.

### Kazi ya 8.5

**Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Kiliku alihudhuria mafunzo ya uandishi wa visa na matukio kwa muda wa mwezi mmoja. Aliporejea nyumbani, alimsimulia mjomba wake mafunzo yote kwa dakika kumi. Aliandika muhtasari wa mafunzo kwa muda wa dakika ishirini na kubandika mbele ya darasa ili kila mmoja asome.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maswali

1. Kiliku aliwezaje kusimulia mafunzo ya mwezi mzima kwa dakika kumi?
2. Unafikiri ni mbinu gani Kiliku aliitumia kusimulia mafunzo?
3. Kiliku aliwezaje kuandika kwenye karatasi mafunzo yote ya mwezi mzima kwa dakika ishirini?
4. Kiliku alizingatia mambo gani kufupisha habari kwa mazungumzo na kwa maandishi?

### Kazi ya 8.6

Tafiti historia ya kaya yenu, kisha iandike kwa maneno yasiyozidi 70 na yasiyopungua 50 kwa kuzingatia kanuni za uandishi.

### Zingatia

Katika kufanya ufupisho wa habari yoyote, unapaswa kuzingatia yafuatayo:

(a) Kufupisha habari kuwa fupi kuliko ya mwanzo.

(b) Kubakiza maana ileile katika habari iliyofupishwa.

(c) Kuwa na mtiririko mzuri wa mawazo yenye mantiki.

(d) Kutumia maneno yako mwenyewe.

Hatua za kufuata wakati wa kufupisha habari.

(a) Soma habari yote kwa umakini.

(b) Bainisha mawazo makuu au taarifa muhimu kutoka kwenye habari uliyoisoma.

(c) Andika habari kwa lugha fasaha kwa mtiririko mzuri wa mawazo.

(d) Hakikisha idadi ya maneno imekamilika kulingana na maelekezo, kama hukupewa idadi ya maneno, fupisha habari hiyo katika theluthi moja ya habari ya mwanzo.

(e) Husianisha taarifa muhimu na habari ya awali kama zinaendana.

(f) Zingatia taratibu za uandishi, mfano matumizi ya viakifishi na matumizi ya herufi kubwa na ndogo.

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 142 9/6/21 5:55 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la marudio la 8

**Soma shairi hili, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Cheti hutoa jasho, miilini tukanata,
Cheti tunataka mwisho, kila mtu kukipata,
Cheti hutukausha, usingizi hukauka,
Cheti hunyonya afia, mwisho tukadhoofika,

Cheti hukausha damu, tukabaki tu wakavu,
Cheti huondoa hamu, kula twaona uchovu,
Cheti kinatuchafua, na maji hatuyagusi,
Cheti uchi twatembea, hatushangai utusi,
Cheti hubagua watu, ujamaa ukavia,

Cheti hutufanya butu, twakata kwa kusinzia,
Cheti hutukomeshea, raha zilizo azizi,
Cheti hutia upaa, na nywele ukatushika,
Cheti huleta na fujo, katika zetu ratiba,
Cheti hututia chujo, tutafutapo kwa huba.

Cheti hutupunguzia, ibada zetu kwa Mola,
Cheti hutunyima saa, tukaacha zetu sala,
Cheti huvuruga wito, ukaitika kusiko,
Cheti hutuweka shoto, kwenye nyingi sokomoko,
Cheti huleta utundu, matobo ukatoboa.

Cheti ni kama utandu, twatanda na kutandia,
Cheti hutumainisha, katika yetu maisha,
Cheti ndio hudhihirisha, elimu tumeiisha,
Cheti husahaulisha, yale tuliyojifunza,
Cheti hutuzubaisha, tukazubaa kuanza.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Cheti kweli ni amana, katika hii dunia,
Cheti huwa kina maana, kwa yule mwenye kujua,
Cheti ni kitambulisho, chatambulisha upesi,
Cheti ndio ukumbusho, ni nyepesi karatasi,
Cheti watu twazozana, wengine twaibiana,
Cheti tunafarakana, karatasi yenye jina.

*(Mtihani wa Kiswahili kidato cha nne,* 1986*)*

Maswali

1. Chagua jibu sahihi katika maswali yafuatayo:

   (i) Cheti hufanya nini?
   - (a) Husumbua akili za watu.
   - (b) Hukatisha tamaa.
   - (c) Hujenga uvumilivu.
   - (d) Hujenga ubaguzi wa rangi.
   - (e) Huvutia wasomaji.

   (ii) Mwandishi anasema __________
   - (a) "Cheti hunyoa kama wembe."
   - (b) "Cheti huvuruga mipango."
   - (c) "Cheti huleta elimu kubwa."
   - (d) "Cheti hujipendekeza kwa watu."
   - (e) "Cheti hufurahisha watu."

   (iii) "Cheti hutuingilia katika mapenzi" maana yake __________
   - (a) hufanya wapendanao wafarakane
   - (b) hupunguza ugomvi
   - (c) huzuia watu wasifanye watakayo
   - (d) hufanya wapenzi wasionane
   - (e) hukutanisha wapenzi

   (iv) Mwandishi anasema, "Cheti watu twazozana, wengine twaibiana" kwa sababu __________
   - (a) ni utambulisho wa elimu
   - (b) ni ukumbusho wa tabu

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 144 9/6/21 5:55 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) ni chujo ya huba
(d) hakina mwisho
(e) huleta raha maishani

(v) Mwandishi anaposema, "Cheti ndio hudhihirisha, elimu tumeiisha" ana maana cheti __________
(a) hudhihirisha kuwa tumeisha kielimu
(b) hudhihirisha kuwa tumeiva kielimu
(c) hudhihirisha kuwa tumebobea kielimu
(d) hudhihirisha kuwa tumehitimu vidato
(e) hudhihirisha kuwa tumemaliza elimu

(vi) "Cheti hutunyonya damu tukabaki tu wakavu" ana maana gani?
(a) Tunapungukiwa damu mwilini kwa sababu ya cheti.
(b) Tunapungukiwa damu kwa sababu hatuli chakula bora.
(c) Tunapungukiwa damu kwa sababu ya uchovu mwingi.
(d) Tunapungukiwa damu kwa sababu tunakosa hamu ya kula.
(e) Tunapungukiwa damu kwa sababu ya kazi nyingi.

2. Fafanua maana ya mshororo ufuatao "cheti ni kama utandu, twatanda na kutandia."

3. Ni kwa nini mtunzi wa shairi anasema kuwa "Cheti hubagua watu, ujamaa ukavia?"

4. Kwa maneno yasiyozidi 50, eleza shida zinazowapata watu kwa sababu ya cheti.

5. Fupisha shairi hilo kwa maneno yako mwenyewe katika ubeti mmoja wenye mishororo minne.

6. Eleza maana ya ufahamu.

7. Mambo yapi unapaswa kuyazingatia wakati wa kusoma habari?

8. Ufahamu unakusaidiaje katika maisha yako ya kila siku?

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 145 9/6/21 5:55 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Faharasa

**ambatani** mfuatano wa sentensi kwa kutumia viunganishi au alama ya mkato

**chagizo** sehemu ya sentensi inayokaliwa na kielezi

**changamani** yenye kuambatana na o-rejeshi na huhitaji maelezo mengine ili kukamilisha ujumbe

**dayalojia** majibizano ya watu wawili au zaidi katika mazungumzo

**dhihaka** tamathali inayotumika kumdunisha mhusika fulani kwa kutumia mafumbo

**falsafa** imani ya mtunzi kuhusu ukweli wa maisha

**fasihi andishi** kazi ya sanaa inayowasilishwa kwa maandishi

**fasihi** sanaa inayotumia lugha kiufundi kuwasilisha masuala mbalimbali yanayomhusu binadamu na maisha yake

**hadhira** ni wasikilizaji, watazamaji au wasomaji wa kazi ya fasihi

**hakiki** chambua, tathmini na fafanua vipengele vya fani na maudhui katika kazi ya fasihi inayohusika

**hekaya** hadithi au visa vya kubuni (simulizi)

**istilahi** neno linalowakilisha dhana fulani katika uwanja maalumu wa maarifa

**kiambajengo** kipashio ambacho hushirikiana na vipashio vingine katika kuunda kipashio kikubwa zaidi kwenye sentensi

**kiambishi** mofu zinazopachikwa kwenye mzizi wa neno

FOR ONLINE USE ONLY



Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 146 9/6/21 5:55 PM

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**kijalizo** Kiambajengo muhimu cha sentensi au kishazi ambacho kimechukuliwa kuwa na kazi ya kukamilsha maelezo yaelekezwayo na kitenzi

**kirai** neno au mpangilio wa maneno wenye neno kuu moja

**kisasili** hadithi fupi ya kubuni inayoelezea chanzo cha maumbile au tabia fulani ya kiumbe

**kishazi** tungo yenye kitenzi inayotoa taarifa kamili au isiyo kamili

**maudhui** mambo yote yanayozungumzwa katika kazi ya fasihi inayohusika

**mdokezo** tamathali ya semi ambayo katika muktadha fulani jambo au kitu huandikwa bila kukamilishwa kwa kuacha nafasi wazi

**mhakiki** mtaalamu mwenye uwezo wa kuchambua fani na maudhui ya kazi ya fasihi na kutoa ushauri, mapendekezo au uamuzi

**michapo** masimulizi yanayoongezewa chumvi ili kuvuta usikivu wa wasikilizaji

**mizani** idadi ya silabi zinazopatikana kwenye mshororo wa shairi

**mtindo** kipengele cha kifani kinachoonesha upekee wa msanii katika usukaji wa kazi yake

**mubalagha** tamathali ya semi inayotia chumvi, mfano: alilia hadi moshi ukamtoka puani, alisoma hadi kitabu kikatoa moshi

**muundo** kipengele cha kifani kinachohusu umbo au mwonekano wa kazi ya sanaa

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**nathari** utungo unaotumia lugha ya mjazo

**ngano** hadithi fupi zinazohusu mambo ya kale ambazo watu wazima waliwasimulia watoto wao

**riwaya** hadithi ndefu ya kubuni yenye kusimulia kisa au matukio fulani

**ruya** ndoto au njozi

**sanaa** ufundi wa kuwasilisha hisia na mawazo ya binadamu kwa maandishi, michoro, uchongaji, ufumaji au mazungumzo

**shairi** utanzu wa ushairi ambao hutumia lugha ya mkato, sanaa ya vina na mizani katika kuwasilisha ujumbe

**shamirisho** sehemu ya sentensi upande wa kiarifu inayokaliwa na nomino

**sitiari** tamathali ya semi inayoonesha ulinganishaji wa moja kwa moja bila kutumia maneno ya ulinganishi

**sudusi** moja ya sita

**taashira** tamathali ya semi inayoashiria hali ya kitu au jambo fulani

**tabaini** tamathali ya semi inayosisitiza jambo kwa kutumia maneno au kauli pinzani

**takhmisa** shairi lenye mishororo mitano

**tathmina** mashairi yenye mshororo mmoja katika ubeti

**tamthiliya** mchezo unaoandaliwa kwa lengo la kuigizwa jukwaani

**tanakali sauti** sauti za kuigiza milio ya vitu, wanyama au wadudu

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| | |
|---|---|
| **taniaba** | tamathali ambayo jina la mtu hutumika kwa watu wengine wenye tabia au mwenendo sawa na wa mtu huyo |
| **tarbia** | mashairi yenye mishororo minne katika ubeti |
| **tashibiha** | tamathali ya semi inayotumika kuonesha ulinganishaji wa vitu kwa kutumia maneno ya ulinganishi mfano kama, mithili ya, kuliko, sawa |
| **tashihisi** | tamathali ya semi ambayo wanyama, ndege, wadudu au vitu hupewa nafasi ya kutenda kama binadamu. |
| **tashtiti** | tamathali ambayo mtu huuliza swali ambalo tayari anafahamu jibu lake |
| **tasifida/tafsida** | tamathali ya semi inayotumika kupunguza ukali wa maneno |
| **taswira** | picha au jazanda inayojengwa akilini mwa mtu au hadhira |
| **tathilitha** | mashairi yenye mishororo mitatu kwa kila ubeti |
| **tathnia** | mashairi yenye mishororo miwili katika ubeti |
| **utanzu** | tawi au kipengele cha fasihi |
| **utendi** | shairi lenye beti nyingi na mistari mifupi yenye vina vya mwisho pekee, huelezea matukio ya kihistoria na ya kishujaa |
| **vina** | silabi za kati na za mwisho katika mshororo wa shairi ndani ya ubeti |
| **visa** | simulizi za kweli au za kubuni zinazoambatana na mafunzo fulani |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Bibliografia


BAKITA. (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

BAKITA. (2016). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers.

Besha, R.M. (2007). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Macmillan Aidan.

Chraghdin, J. & Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.

Massamba, D.P.B. Kihore Y.M. na Msanjila Y.P. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA),* Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B. KihoreY.M. na Msanjila Y.P. (2012). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA),* Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B. (2016). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TATAKI.

Mbijima, R. (2019). *Mtenda Hutendwa*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Mdee, J.S. (2007). *Sarufi ya Kiswahili, Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: DUP.

Mghanga, A.F. (2007). *Mwalimu Rose*. Dar es Salaam: Macmillan Aidan.

Mgullu, R.S. (2010). Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University.

Mulokozi, M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.

OUT. (1997). *Tamthiliya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: OUT Press.

Saffari, A. (2007). *Joka la Mdimu*. Dar es Salaam: Huda Publishers.

TAKILUKI. (2001). *Malenga Wapya*. Dar es Salaam: Oxford University Press (OUP).

TET. (1996). *Kiswahili Kidato cha Tatu*. Dar es Salaam: Oxford University press

TET. (2019). *Kiswahili Shule za Sekondari, Fasihi*. Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

TET. (2019). *Kiswahili Shule za Sekondari, Lugha na Sarufi*. Dar es Salaam: Taasisi ya Elimu Tanzania.

TUKI. (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.

TUKI. (2005). *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. TUKI.

TUKI. (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wesana-Chomi, E. (2013). Kitangulizi cha Sarufi Maumbo: Chuo Kikuu cha Sebna.

Wesana-Chomi, E. (2017). Kitangulizi cha Muundo Viambajengo wa Sentensi za Kiswahili. Dar es Salaam: TUKI.




Kiswahili Kidato cha Tatu (FINAL) 13/07/2021.indd 150 9/6/21 5:55 PM

ISBN 978-9987-09-269-7

9 789987 092697